**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 28 Juni, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:**

Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Nchi kwa Mwaka 2004 *(The National Drug Situation for the year 2004).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 97

**Ujenzi wa Uzio kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitumia zaidi ya Shilingi milioni mia moja ishirini na tano (125milioni) kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Ofisi ya Makamu wa Rais, lakini baadaye ukasimamishwa:-

(a) Je, kufanya hivyo si matumizi mabaya ya fedha za Serikali?
(b) Je, watendaji waliotumia fedha hizo za Serikali kabla ya kupata ushauri wa kiusalama wamechukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) ningependa kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Kama nilivyojibu swali Na. 108 katika Mkutano wa Nne lililoulizwa na Mheshimiwa Haji Juma Sereweji Mbunge wa Mwanakwerekwe, fedha zilizotumika kujengea uzio ikiwa ni mojawapo ya maandalizi ya awali ya kujenga Ofisi ya kudumu ya Makamu wa Rais zilitumika kufanya uchunguzi wa udongo *(Soil Analysis),* kuhamisha mtandao wa simu, kuhamisha laini ya umeme, kulipia gharama za upimaji wa kiwanja, kugharamia ushauri wa kitaalam (*consultancy services*) na kumlipa mkandarasi. Kwa hiyo, shilingi zaidi ya milioni 125 anazozihoji Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud hazikutumika kujenga uzio peke yake na nia ya gharama hizo ilikuwa njema kabisa.Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Soud kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa nia ilikuwa njema na kwa vile eneo husika limerejeshwa kwa Benki Kuu Tawi la Zanzibar, ambao wataendeleza eneo hilo kwa manufaa ya umma matumizi ya fedha za Serikali hayakuwa mabaya.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mtendaji aliyechukuliwa hatua yeyote kwa sababu waliofanya kazi hawakuiba wala kufuja fedha hizo kwani walifuata taratibu zote za kisheria za ujenzi kwa jengo la Serikali. Tatizo lilikuwa kuchelewa kuwahusisha Idara ya Usalama wa Taifa mapema. Jambo hili limerekebishwa katika kiwanja kipya kilichopatikana. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nashangazwa kidogo kutokana na unyeti wa Ofisi ya Makamu wa Rais, leo tunasema mambo yetu yote tunafanya upembuzi yakinifu na mambo mengine yote, leo Ofisi ya Makamu wa Rais, imeamuliwa kujengwa mahali halafu inaahirishwa. Je, tulikuwa tunafikiria nini? (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba taratibu zote zilifuatwa tatizo ilikuwa ni kucheleweshа au kutowasiliana na Idara ya Usalama wa Taifa mapema. Baada ya shughuli hizo kuanza ndipo Idara ya Usalama wa Taifa, iliposema kwamba eneo hilo halifai. Kwa kweli tunakiri kwamba tumekosea katika hilo, lakini tunachoweza kuhakikisha ni kwamba kiwanja kipya kimeshapatikana eneo la Tunguu na wahusika wote wakiwemo Idara ya Usalama wa Taifa wamehusishwa na ujenzi utaanza mwaka huu 2006 kwa sababu fedha zipo katika Bajeti ya mwaka huu 2006. (*Makofi*)

Na. 98

**Tatizo la Ujambazi Maeneo ya Ziwa Tanganyika**

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA** aliuliza:-

Kwa kuwa ujambazi katika nchi yetu umekuwa ni tatizo sugu katika Ukanda wa Ziwa Tanganyika na kwa kuwa tatizo hilo limewawia vigumu wananchi wanaojishughulisha na uvuvi kuchukua mikopo ya kununua vifaa vya kuendeleza kazi zao, kama injini za boti zao ambazo zimekuwa zikiibiwa mara kwa mara na wanajeshi kutoka Kongo na kwa kuwa, wananchi wanapofuatilia mashine hizo huko Kongo, hutakiwa kulipa kiasi fulani cha fedha ili warudishiwe injini zao:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kufanya mazungumzo na Serikali ya Kongo juu ya namna ya kulitatua tatizo hilo?

(b) Kwa kuwa hakuna ulinzi wa kutosha katika maeneo ya maziwa yetu, jambo linalosababisha matatizo mengi yakiwemo ya ujambazi kama nilivyoeleza kwenye swali hili. Je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuimarisha ulinzi hasa kwenye maeneo hayo ili kukabiliana kikamilifu na tatizo sugu la ujambazi pamoja na matatizo mengine yanayowapata wananchi wa maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge Mhonga Ruhwanya, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa matukio ya ujambazi wa kutumia silaha na kupora mali za wananchi yameendelea kutokea katika maeneo ya mwambao wa Ziwa Tanganyika katika kipindi cha mwaka 2000/2005 na kwa wakati mwingine ujambazi huu hufanywa na watu wanaovaa nguo zinazofanana na sare za askari wa Jeshi la Kongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, kwamba kuna haja ya kufanya mazungumzo na Serikali ya Kongo, juu ya namna ya kulitatua tatizo hilo. Aidha tayari Serikali imeshachukua hatua za awali kwa kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Rukwa, ambayo imepanga kukutana na viongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, ili kuzungumzia namna ya kutatua tatizo hili na pia kuboresha hali ya usalama katika mipaka yetu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyojibu tarehe 23 Juni, 2006 katika swali Na. 77 lililoulizwa na Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, Serikali imeanza kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yenye matatizo kwa kuongeza askari katika vituo vya polisi wanamaji Kipili, Kituo cha Polisi Kirando, Kabwe, Namasi na Karema. Serikali pia imefungua kituo kipya cha Polisi Ikova. Mpango wa muda mrefu wa Serikali ni kununua mashua mpya za doria.

(c) Aidha vifaa kama magari na *radio* za mawasiliano vitanunuliwa katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2006/2007 ili kuimarisha ulinzi katika eneo hilo na sehemu nyingine nchini. Aidha Waziri Mkuu, ameanzisha operesheni maalum ya kupambana na uhalifu mipakani unaoshirikisha vyombo vyote vya dola hapa nchini.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ujambazi unaofanywa katika Ziwa Tanganyika hauishii katika kupora maboti na nyavu peke yake. Je, Serikali inasema nini kuhusu Watanzania ambao walichukuliwa wakapelekwa Kongo na mpaka sasa hivi hawajarudishwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa siku zote Serikali yetu inafanya kila jitihada kutafuta makubaliano mazuri baina yetu na nchi jirani hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kuhakikisha wale wote ambao wamekwenda kinyume na taratibu matatizo yatatuliwe kwa kufuata taratibu za nchi.

Na. 99

**Sera ya Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** alijibu:-

Kwa kuwa sera ya maendeleo ya watu wenye ulemavu ilikwishapitishwa tangu mwaka 2004:-

Je, Serikali inaendelea vipi katika mchakato wa kuhakikisha kuwa sera hiyo sasa inaanza kutekelezwa kikamilifu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Maendeleo na huduma kwa watu wenye ulemavu ya mwaka 2004, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mikakati ya utekelezaji wa sera hiyo. Pamoja na mikakati hiyo, Wizara imeanza taratibu za kukaa na vyama vya watu wenye ulemavu, Wizara mbalimbali na pia Halmashauri za Wilaya/Miji kwa lengo la kuhamasisha na kuelekeza utekelezaji wa sera hii. Wizara kadhalika imetenga Bajeti ya shilingi 160 milioni katika mwaka 2006/2007 kwa ajili ya utekelezaji wa mikakati ya sera hiyo. Pamoja na hatua hii, Wizara yangu imeendelea na taratibu za kawaida za utekelezaji wa sera hii ikiwa ni pamoja na kufanya yafuatayo:-

- Kuichapisha sera (pamoja na breli kwa wasioona) na kuisambaza kwa wadau na wananchi.
- Kuingiza sera kwenye tovuti ya Serikali.
- Kufanya mapitio makubwa na kuingiza maudhui ya sera hiyo katika sheria za ajira na matunzo kwa watu wenye ulemavu.
- Kuandaa mkakati wa utekelezaji.
- Kwa kushirikiana na Halmashauri kuhamasisha wananchi katika utekelezaji wa sera hii.

- Kusambaza sera kwa wasanifu majengo na wajenzi kupitia bodi zao ili majengo wanayojenga yaweze kutumiwa kwa wepesi na watu wenye ulemavu.

**MHE. BENEDECT K. LOSORUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, napenda kuuliza swali kwa Naibu Waziri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Je, ni Idara ipi inayoshughulikia suala la walemavu katika ngazi ya Wilaya ili tuweze kujua?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Kama Wizara yangu inavyoitwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, watu wenye ulemavu wako chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na katika ngazi ya Wilaya wanashughulikiwa na watu wa ustawi wa jamii. Lakini kwa sababu suala walemavu ni suala la walioko katika jamii. Suala la walemavu ni mtambuka kwa hiyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Elimu na Wizara zote zinawahudumia hawa. Naomba ifahamike hivyo. (*Makofi*)

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa walemavu walio wengi hasa huko vijijini ndani, watoto wanaozaliwa na ulemavu na wananchi hawawezi wakajua namna ya kuwahudumia. Je, ni mkakati gani hasa umewekwa ili kuelimisha wananchi na kujua namna ya kuwahudumia au huduma zinazoweza kutolewa kwa watoto wanaozaliwa na ulemavu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao wako vijijini na ambao wanasema hawawezi kupata hizi taarifa kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, tunaendelea na sera ambazo tutazipeleka sehemu zote nchini ili ziweze kusomwa na wananchi na wanajamii wote kwa ujumla. Lakini vile vile kama watoto watazaliwa wakiwa na ulemavu, Wizara pamoja na kushirikiana na sisi viongozi tuweze kuwashauri siyo suala la kuhusiana na ulemavu tu lakini watakapokuwa wana matatizo yoyote watatakiwa kwenda katika huduma za afya ambapo kule watapewa maelekezo. Kwa hiyo, ningeomba kumwambia Mheshimiwa Mbunge, kwamba iwapo kule vijijini wananajifungua watoto wenye ulemavu, lakini vijijini kuna Zahanati na kuna wataalam mbali mbali. Kwa hiyo, ningeomba wananchi wote kuwaambia kwamba yeyote yule atakayeona kwamba amezaa mtoto ambaye ana ulemavu wa aina moja au nyingine basi asisite kwenda kwenye vituo vya huduma za afya na kama hataweza basi anaweza akamwona mtu yeyote yule ambaye anayehusika na mambo ya Ustawi wa Jamii ili aweze kumsaidia vilivyo. *(Makofi)*

Na. 100

**Tiba ya Magonjwa ya Moyo nje ya Nchi**

**MHE. LUCY F. OWENYU (K.n.y. MHE. SUZANA A. J. LYIMO)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wengi hasa watoto wanasumbuliwa na maradhi ya moyo na kwa kuwa tiba ya maradhi hayo hupatikana zaidi nje ya nchi na kwa gharama kubwa na kwa kuwa Watanzania walio wengi hawana uwezo wa kugharamia matibabu hayo na

kwa kuwa Serikali pia haina uwezo wa kuwapeleka wote nje kwa matibabu, hivyo kuchukua jukumu la kupeleka baadhi ya wagonjwa kutibiwa.

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kufanya kazi na taasisi ya moyo, *Tanzania Heart Institute?*

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kujenga kitengo cha kushughulikia ugonjwa huo?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kupeleka wagonjwa hao kutibiwa nje ya nchi ni gharama kubwa na kwamba hali hiyo inawavunja moyo watalaam wetu wa ndani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo yafuatayo kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Suzana Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuwapeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi ni gharama kubwa na kwa sababu ya ukosefu wa fedha za kutosha ni wagonjwa wachache wenye hali mbaya ndiyo hupelekwa kutibiwa. Serikali inaendelea kufanya jitihada za makusudi ili matibabu yanayopatikana nje ya nchi yaweze kupatikana hapa hapa nchini. Tayari kuna matibabu kwa mfano yale ya kuweka nyonga bandia (*Hip Replacement)* yanatolewa hapa hapa nchini kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suzan Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na sekta binfasi katika kutoa huduma za afya na kuna mkakati mahsusi katika mabadiliko ya sekta ya afya wa kukuza ushirikiano uliopo kati yake na sekta binafsi ikiwemo taasisi ya moyo *(Tanzania Heart Institute).* Serikali kupitia Wizara yangu inaendelea kuimarisha ushirikiano na taasisi hii katika maeneo yafuatayo:- 1. Kupunguza kodi kwa vifaa vinavoingizwa kwa ajili ya taasisi hii. 2. Wizara yangu ina mjumbe katika Bodi ya Taasisi hii.3.Kutoa ushauri wa kitaalamu pale unapohitajika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa sasa inafanya maandalizi ya kuanzisha kitengo cha matibabu ya moyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Kiasi cha shilingi bilioni 4 kimetengwa kwa ajili ya kuanzisha huduma hii katika mwaka ujao wa fedha 2006/2007. Wizara imepeleka timu ya Watalaam 29 nchini India kwenda kujifunza upasuaji wa moyo wakiwemo mabingwa wa upasuaji, wauguzi na watalaam wa dawa za usingizi.

(c) Ni kweli kabisa kupeleka wagonjwa kutibiwa nje ya nchi ni gharama kubwa sana. Hata hivyo Wizara hupeleka wagonjwa nje ya nchi kupata matibabu ambayo hapa

hayapatikani kwa sababu ya kukosekana watalaam, vifaa au vyote viwili. Kwa hali hiyo, kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa sababu hizi si kuwavunja moyo watalaamu bali kuwapa changamoto wajitahidi kupata ujuzi unaotakiwa na changamoto kwa Serikali. Aidha Wizara itaendelea kuziwezesha hospitali za rufaa kutoa huduma ambazo kwa sasa hazipatikani hapa nchini ikiwa ni pamoja na watoa huduma toka sekta binafsi kadri itakavyowezekana.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri sana. Kwa kuwa watoto wengi ambao wamezaliwa katika hali ya matatizo ya ugonjwa huu ambao ni thakili sana mara nyingi wale wanaokuweko vijijini si rahisi kuweza kuja kwenye matibabu katika hospitali hata kikiwekwa hicho kitengo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali itakuwa na mkakati gani wa kuandaa ili wale ambao wako vijijini na pengine hata gharama za kufika hapo Hospitalini inakuwa ni ngumu kitu kinachowapelekea kuathirika na hatimaye kupoteza maisha?

**NAIBU WAZIRI, AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna watoto ambao wanazaliwa na matatizo ya moyo wakiwa vijijini na kwamba pengine hawana uwezo wa kuweza kufika katika zile hospitali za rufaa. Ninachoomba kushauri ni kwamba katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kuna utaratibu wa rufaa ambao mgonjwa anapofika mahali alipo kunakuwa na utaratibu kama tatizo lake linashindikana katika ngazi ya zahanati anatakiwa apate rufaa ya kwenda kwenye Wilaya, kama Wilaya inashindikana anakwenda kwenye ngazi ya Mkoa, Mkoa inafika hadi rufaa. Kwa hiyo, ningependa kushauri kwamba iwapo mtoto au mgonjwa yeyote ataona kwamba kule kwenye ile ngazi husika inashindikana basi wale watalaam ambao wanawaona hawa wenye matatizo haya waweze kuwapa rufaa mara moja ili waweze kufika kwa watalaam wanaohusika na kuwafanyiwa vipima na hatimaye kufanya uamuzi. Aidha waweze kutibiwa hapa hapa au waweze kupelekwa nje ya nchi kama inastahili.

**MHE. JANET B. KAHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kuridhisha nina swali moja kama ifuatavyo:-

Pamoja na kuwa amesema wanatoa ushauri kwa hospitali binafsi na kwa kuwa wakati huu wamejitokeza baadhi ya madaktari na watu kuanzisha hospitali mbili zinazojulikana za moyo ikiwemo Hospitali ya *Heart Institute* na ya Motie Mengi. Je, Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuzisaidia hospitali hizi kifedha ili ziweze kukidhi matatizo ya wagonjwa wa moyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Janet Kahama, kama ifuatavyo: Ni kweli kuna taasisi nyingine za binafsi alivyotaja za *Tanzania Heart Institute* na za *KCMC* ambao wanatibu wagonjwa wenye matatizo haya. Serikali kama nilivyosema inaendelea kushirikiana nao katika mambo mengi kama nilivyotaja katika swali langu la msingi. Lakini pale inapojitokeza kwamba inahitajika kutoa fedha sisi huwa hatuna matatizo, kama fedha inaturuhusu huwa tunatoa. Tumekuwa tunawasaidia watu wa taasisi binafsi

kwa mfano *KCMC* tunashirikiana nao vizuri sana, tunaushirikiano kama nilivyosema na watu *Tanzania Heart Institute* na pale wanapohitaji msaada au wa madaktari wa kwetu au madaktari wengine kuweza kuwa-*support* kwa upande wa fedha sisi hatuna tatizo ili mradi tu Bajeti yetu inaturuhusu. (*Makofi*)

Na. 101

**Kukwamua Akina Mama Kimaendeleo**

**MHE. FATMA MIKIDADI (K.n.y. MHE. MARIAM R. KASEMBE)** aliuliza:-

Kwa kuwa akina mama wa Mkoa wa Mtwara wako nyuma kimaendeleo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi katika kutoa kipaumbele kutoa mafunzo mbalimbali ya kujikwamua kiuchumi na kutoa mikopo nafuu ili waweze kumudu mahitaji ya pembejeo za kilimo?

(b) Je, Serikali inatoa msukumo gani kwa *NGOs* mbalimbali ili zielekeze Kusini ambako kuna umaskini uliokithiri kuliko kutoa huduma katika miji mikuu tu?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, Mbunge - Viti Maalum, naomba kwa ridhaa yako nitoe pole nyingi sana kwa kufiwa na baba yake mzazi jana usiku. Naomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Mariam Kasembe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea kutekeleza mipango ya kuwawezesha wanawake hususan waliomo katika Mkoa wa Mtwara kwa kuwapatia mikopo na mafunzo mbalimbali ili kuwainua kiuchumi na kuwaongezea ajira na kipato.

(b) Katika kulipa kipaumbele suala hili Serikali katika mwaka huu wa fedha 2006/2007 imetenga wastani wa shilingi milioni 500 kwa kila Mkoa ili kuwawezesha wananchi kwa ujumla na wanawake kiuchumi na kuwaongezea ajira. Aidha, Serikali inaendelea na mchakato wa kuwawezesha wanawake kiuchumi kupitia Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake. Mfuko huu unaratibiwa katika ngazi ya Halmashauri na

unatoa mikopo kwa vikundi vya wanawake baada ya kuwapatia mafunzo ya ujasiliamali. Hata hivyo tunakiri kuwa mikopo hii haitoshelezi mahitaji ya wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi za Serikali, zipo pia taasisi ambazo zinaendelea kutoa mafunzo na mikopo kwa wanawake ili wajikwamue kiuchumi. Taasisi hizo ni kama vile *Promotion of Rural Initiaties and Development Enterprises (PRIDE), Mtwara Small Scale Enterprises Development Associations (MSEDA),* Kikundi Mwavuli Mtwara (KIMWAM), Chama cha Ushirika cha Kuweka na Kukopa cha Wafanyabiashara Soko Kuu Mtwara, *Masasi Women Development Association* na Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO*).

Aidha, katika kipindi cha Aprili – Juni, 2006 *SIDO* imeweza kufanya mafunzo mbalimbali kwa akina mama wa Mtwara. Mafunzo hayo ni kama vile utafutaji wa masoko na masuala ya uendeshaji wa kibiashara, usindikaji wa vyakula na kilimo cha uyoga.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuziwezesha *NGOs* mbalimbali kutoa huduma katika Mikoa ya Kusini kama ilivyoulizwa katika swali la (b) la Mheshimiwa Mariam Kasembe, Serikali inaendelea kuhimiza *NGOs* za Kitaifa na Kimataifa kuanzisha miradi yenye kuwaongezea wanawake kipato na ajira ili waondokane na umaskini.

Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la *NGOs* zitaendelea na jitihada za kuelekeza na kuhamasisha *NGOs* kupitia Mtandao *NGOs* wa Kusini kuweza kuhakikisha kwamba *NGOs* za Kimataifa zinashirikiana na Mikoa ya Kusini katika programu mbalimbali za kuwajengea uwezo *NGO* hizo kupitia mitandao ya kiraia kama *The Foundation for Civil Society. (Makofi).*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mikoa ya Kusini ilikuwa nyuma si kwa sababu tu ya uvivu wao ni kwa sababu ya sera za Kikoloni ambazo ziliwekwa kuifanya Mikoa ya Kusini kuwa ni watu wao wa kuwachukua na kuwafanya manamba. Kwa hiyo, walizuia barabara na wawekezaji wasiende Mikoa ya Kusini pamoja na Lindi. Je, kuna mpango mwingine kwa ajili ya Lindi vile vile? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Chama chake cha Mapinduzi katika Ilani yetu tunatambua kwamba kuna Mikoa ambayo kutokana na Historia au sababu za kijiografia haiko katika usawa mmoja wa kimaendeleo.

Kwa hiyo, utambuzi huo unajulikana na kupitia mipango yetu ambayo tumeianisha katika Ilani ya Uchaguzi na maazimio yetu na hasa azimio ambalo tumelitoa

katika Mkutano Mkuu ambao tumemaliza juzi tumeelekeza kwamba tutahakikisha kwamba tunapeleka nguvu katika Mikoa ile ambayo kutokana na historia hizo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge na kutokana na sababu za kijiografia Mikoa kama vile Mtwara, Lindi, Rukwa, Kigoma na Mikoa mingine ambayo inahusiana na mambo hayo tutapeleka nguvu zetu na kuhakikisha kwamba wanapata misaada na maendeleo kama Mikoa mingine. (*Makofi*)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika na majibu ya Naibu Waziri, lakini hizi asasi alizozitaja bado nyingi ziko mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, kwa kuwa wanawake wengi vijijini Tanzania wana hali mbaya, Serikali itabadilisha mwelekeo wake kwanza kwa kuhakikisha kuwa zile Halmashauri ambazo hazijalipia asilimia kumi ya mapato yao zinalipa na pia hizi hela ambazo Waziri Mkuu, amezisema kwenye hotuba yake zitaelekezwa zaidi vijijini ili akina mama nao wajikomboe kiuchumi*? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu tayari imeshafanya mawasiliano na Wizara ya TAMISEMI kuhusu suala la kuziwezesha Halmashauri kuhakikisha kwamba Halmashauri zinalipa asilimia 10 kama ilivyopendekezwa na tulivyokubaliana ili basi Mfuko ule wa *WDF* kwa ajili ya akina mama uweze ukawa na manufaa na ukawafikia akina mama wengi zaidi. Jitihada kubwa zitaelekezwa kule kule vijijini.

Lakini vile vile Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge na hasa sisi Wabunge wa Viti Maalum, tutashirikiana kwa karibu na Halmashauri na Madiwani wenzetu katika maeneo yetu kuhamasisha na kuhakikisha kwamba tunawashirikisha akina mama katika vijiji kubainisha matatizo yao na kero zao na kupanga mikakati ili basi tuweze tukawa na mkakati mzuri na patakapokuwa na fedha tukaendeleza mipango ambayo tayari yametokana na kero za wananchi wenyewe. *(Makofi)*

Na. 102

**Kipengele cha Uzoefu wa Kazi**

**MHE. GRACE S. KIWELU** aliuliza:-

Kwa kuwa muda mrefu umepita Tanzania ikiwa inateseka na ukosefu wa ajira kwa vijana na kwa kuwa, moja ya sababu ni ile dhana ya kwamba, vijana ni Taifa la

kesho hivyo kuajiriwa kwa wazee wastaafu kwa mikataba hata kama kuna vijana wenye sifa:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo hilo kwa kazi ambazo vijana wanabanwa na kipengele cha uzoefu wa kazi?

(b) Je, ni lini kipengele hiki cha uzoefu kitaondolewa katika sifa za mwombaji ili vijana nao wapate nafasi ya kutumia usomi na ujuzi walio nao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mhesihmiwa Grace S. Kiwelu, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mikakati madhubuti wa kuongeza ajira kwa Watanzania wasio na ajira, hususan vijana ili waweze kuajiriwa katika sekta mbalimbali hapa nchini. Vijana ni kundi ambalo limeathirika na ukosefu wa ajira ya kuajiriwa hasa baada ya mabadiliko ya kiuchumi yanayoendelea duniani kote. Serikali kwa kutambua hilo, imeweka mikakati maalum wa ajira kwa vijana ili waweze kuajiriwa au kujiajiri wao wenyewe.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mikakati hiyo ni kuwajengea uzoefu vijana kwa kuwaandaa wakiwa mashuleni na vyuoni ili kuwa na stadi zinazohitajika kwenye soko la ajira ili waweze kuajiriwa katika nafasi za kazi zinazopatikana hapa nchini.

Serikali itatilia mkazo katika kuwahamasisha na kuwashauri waajiri, kupitia Chama chao cha Waajiri *(ATE)* wapende kuwaajiri vijana wengi zaidi wasio na uzoefu ili waweze kupata uzoefu wakiwa kazini. Njia nyingine ni kuweka mazingira mazuri ili vijana waweze kufanya kazi za kujitolea ambazo zinaendana na kazi wanayotarajia kuzifanya pindi nafasi za ajira zitakapopatikana.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha uzoefu ni muhimu kwa baadhi ya waajiri, hasa inapotokea kuwa mwajiri anataka kujaza nafasi inayohitaji mfanyakazi ambaye amebobea katika taaluma na mwenye uzoefu wa muda mrefu.

Mfanyakazi anapohesabiwa kuwa amebobea katika fani yake kama vile uhasibu, ualimu, upishi ni baada ya kazi hiyo kuisomea na kupata mafunzo mbalimbali, mara nyingi akiwa kazini na pia anakuwa amepata mafunzo mengi yanayoendana na kazi hiyo. Suala la uzoefu, hasa katika ngazi za kati na za juu ni ukweli kwamba huongeza ufanisi na faida kwa mwajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako tukufu kuwa si kazi zote zinazohitaji wazoefu. Katika utafiti mdogo

tuliofanya mwezi wa pili na wa tatu mwaka 2006 katika Kituo cha Ajira cha Dar es Salaam yaani *Dar es Salaam Employment Survey* tuliyoifanya ilionekana baadhi ya Ofisi za Serikali, Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Mabenki, Makampuni ya Bima na Makampuni binafsi hazihitaji vijana ambao wana uzoefu. Wanahitaji tu vijana ambao wamemaliza vyuoni na mashuleni na ambao hawana uzoefu wowote.

Kwa msingi huo basi, tutaendelea kuhimiza sekta binafsi kuwa na mawasiliano ya karibu na vyuo mbalimbali ili kujiandaa kuwapokea wahitimu wa fani mbalimbali.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa vijana hawa wanapita katika vyuo na kabla ya kumaliza vyuoni huwa wanapita kwenye mazoezi ya vitendo. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuna kazi ambazo zinahitaji uzoefu. Kwa nini sasa uzoefu ule wanaoupata kwenye mazoezi ya vitendo isiwe ni kigezo kimojawapo cha kuwapatia ajira?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika swali langu la msingi, tunachokifanya sasa hivi ni kuwajengea stadi za kazi wakiwa mashuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili eneo la mazoezi kwa vitendo huwa ni sehemu ya mitaala wanafunzi wanapokuwa katika vyuo. Ni kweli inaongeza uzoefu wao lakini haitoshelezi mahitaji ya waajiri wanapotaka kuwaajiri watu ambao wanawaita wamebobea katika shughuli zao. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Vijana wengi hukosa ajira Serikalini kwa sababu mfumo wa wafanyakazi wa Sekali kustaafu kufuatana na kigezo cha umri. Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuwaajiri wafanyakazi wake kwa njia ya mikataba ili ukiisha vijana wengine wachukue nafasi zao?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA (MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zilizoko Serikalini ni kwamba hawa wafanyakazi wa mikataba ni wachache mno ni sawasawa na asilimia 0.5. Kwa hiyo, ni *negligible number* na Serikali inazingatia sana sana kwamba wale wanaoajiriwa kwa mikataba ni wale tu ambao wanahitajika kwa shughuli maalum. Na wala si Sera ya Serikali kuendelea kuwaajiri watu kwa mikataba.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Zungu mkakati uliopo Serikalini sasa hivi ni kuendelea kuwaajiri vijana wenye uwezo katika soko la ajira.

Na. 103

**Mpango wa Taifa wa Kutekeleza Miradi ya Maji**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Awamu ya Tatu imeshafanya maandalizi ya kutekeleza mpango wa Taifa ambao utekelezaji wake unahitaji michango kutoka Halmashauri za Wilaya na wananchi watakaonufaika:-

(a) Je, mpango huo utaanza kutekelezwa lini?

(b) Je, Halmashauri na wananchi wanatakiwa kuchangia kwa kiasi gani?

(c) Je, Miradi ya maji ya Jimbo la Bumbuli iliyofanyiwa michoro na usanifu, itaanza kunufaika na mpango huo lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Jimbo la Bumbuli lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini utaanza katika mwaka wa fedha 2006/2007 kwenye Wilaya zote za Tanzania Bara. Maandalizi ya utekelezaji kwenye ngazi zote za Taifa, Mikoa na Wilaya yanaendelea ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa fedha za utekelezaji katika muda uliopangwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Programu ya Kitaifa ya Maji na Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini Halmashauri zitachangia kiasi kile ambacho kitatoka kwenye Bajeti ya Serikali Kuu kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu.

Wananchi watatakiwa kuchangia fedha taslimu kati ya asilimia 2.5 hadi asilimia 5 ya gharama za ujenzi kufuatana na teknolojia itakayotumika. Aidha, wananchi watachangia pia nguvu kazi. Katika kuimarisha utekelezaji wa mpango huo, wadau mbalimbali wataunganisha nguvu zao ili kufanikisha lengo la pamoja ambalo ni utekelezaji wa programu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji Jimbo la Bumbuli iliyofanyiwa michoro na usanifu ni Mpalalu/Ngwelo, Kwakidole, Kweminyasa, Manga/Funta, Bumbuli na Mgwashi. Kati ya miradi hiyo baadhi itafanyiwa mapitio ya usanifu mwaka wa fedha 2006/2007 chini ya Programu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni Kwakidole, Kweminyasa, Bumbuli na Mgwashi. Miradi ya Mpalalu/Ngwelo na Manga/Funta itatekelezwa kulingana na upatikanaji wa fedha chini ya mipango ya Halmashauri ya Wilaya.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba ya Waziri pamoja na Serikali kwa mikakati hii mizuri aliyoweka. Je, Waziri atapokea shukrani za wananchi wa Jimbo la Bumbuli kwamba miradi hii kwa kweli itawasaidia sana na iende kwa kasi ambayo inategemewa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na tunapokea hizo shukrani na pia tutajitahidi kadri tuwezavyo kuzidi kuimarisha miradi ya maji Jimbo la Bumbuli. Ahsante. *(Makofi)*

Na. 104

**Maji ya Nyasa**

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Ziwa Nyasa halijachafuka na maji taka na kwa kuwa katika maeneo yote ya mwambao wa Ziwa Nyasa hakuna huduma ya maji kwa wananchi na hivyo kusababisha wananchi watembee kilometa nyingi kufuata maji katika Ziwa Nyasa. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza mradi wa kusambaza Maji ya Ziwa Nyasa kwa wananchi waishio vijiji vya Mwambao wa Ziwa hilo ili wapate maji kama ilivyo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutoa huduma sahihi ya maji kwa wananchi, jambo la awali ni kufanya utafiti ili kuona aina gani ya vyanzo vya maji na teknolojia gani itakayotumika ili kutoa huduma hizo. Kwa hali hiyo, Wizara yangu katika kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ya 2005 imefanya yafuatayo:-

Katika mwezi Mei 2006 Wizara yangu ilituma timu ya Wataalam kwenda kufanya utafiti kuhusu huduma na upatikanaji wa maji katika Wilaya ya Mbinga. Utafiti huo ulifanywa katika maeneo yafuatayo:-

Katika Kata ya *Mbambabay*, katika Kata ya Kingerikiti, katika Kata ya Ngumbo, katika Kata ya Mbaha, na katika Kata ya Lituhi. Utafiti huo ulionyesha yafuatayo:-

Ulionyesha katika Kata ya Kingerikiti, vijiji vyote huduma ya maji ni asilimia 0. Katika Kata ya Ngumbo pia ilionyesha huduma ya maji ni asilimia 0. Na katika Kata ya Lituhi ilionyesha vijiji vinne pia havina huduma ya maji ikiwemo kijiji cha Mbaha, Kijiji cha Ndumbi, Kijiji cha Mwera Mpya na Kijiji cha Litumbakuhamba. Baada ya hapo Wizara ilichukua hatua zifuatazo ambapo vijiji nitakavyovitaja vimeingizwa katika programu ya kusaidiwa katika awamu hii ambapo Mbinga Magharibi, Kijiji cha Kingerikiti, Kijiji cha Ukuli, Kijiji cha Ngambo, Kijiji cha Mkili, Kijiji cha *Mbambabay*,

Kijiji cha Lundu na Kijiji cha Litumbakuhamba vimeingizwa katika Programu ya Majisafi na Mazingira katika awamu hii.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahishwa na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini pamoja na furaha hiyo, nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mradi wa maji wa Ziwa Victoria unaopitia maeneo ya Kahama na Shinyanga karibu unakamilika na kuondoa kabisa kero ya wananchi wa maeneo hayo. Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya mradi kama huo huo kuanzishwa katika Ziwa Nyasa ili wananchi wa maeneo hayo wafaidike? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufuatanana utafiti tulioufanya imeonyesha dhahiri kwamba Wilaya ya Mbinga ina vyanzo vya maji vya kutosha kwa hivi sasa na kwa hali hiyo tutaendelea kutumia vyanzo hivi vya kutosha ila kwa mipango ya baadaye mipango ya muda mrefu Wizara yangu itatafuta fedha za pole pole kuanza kufanya utafiti kuhusu utumiaji wa Ziwa Nyasa.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja dogo la nyongeza. Ni kweli kwamba maji ya Ziwa Nyasa kwa kuonekana ni mengi sana na vile vile ni mazuri. Lakini kuna baadhi ya Kata zilizo kando kando ya Ziwa hilo zinashambuliwa sana na magonjwa kama ya vichocho na hivyo kupelekea wananchi wengi kuugua mara kwa mara ugonjwa huo. Je, wakati mipango inaendelea kufanyika kusambaza maji katika Kata zote za mwambao wa Ziwa Nyasa, Serikali inaweza ikafanya utaratibu wa kusaidia kusambaza madawa ya kutibu maji ya Ziwa Nyasa ili wananchi wale wanapokunywa maji yale waweze kupata usalama na wasiweze kuugua? Ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Kama tulivyosema katika swali la msingi, utafiti unaendelea juu ya matumizi ya maji ya Ziwa Nyasa. Utafiti huo unaambatana vile vile na uchunguzi juu ya ubora wa maji. Kwa hiyo, hapo utafiti utakapokamilika na kuelewa kwa kiwango gani maji yale ni mazuri kwa matumizi kwa binadamu, ndipo tutakapoweza kuamua kwamba tuna haja ya kutumia madawa kiasi gani yaweze kutumika ili maji yanayowafikia wananchi yawe bora na salama kwa maisha yao. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER-OLONYOKIE OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, labda niseme kwamba kwa kuwa Wilaya ya Simanjiro tatizo lake kubwa ni maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo na kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Simanjiro kwa kutambua uzito wa tatizo lenyewe wamechanga fedha zao na kuchimba visima vyenye kina kirefu vipatavyo vitano katika Vijiji vya Loborusweiti, Natwinyo, Emboreti, Sukuro, Rakago na Lwebosireti na kilichobaki sasa ni fedha kwa ajili ya pampu, mashine, birika na *cattle truph* kwa ajili ya matumizi ya mifugo.

Je, Waziri anawaambia nini wananchi hawa ambao wamekwisha changa fedha zao na kuwekeza na hasa ukizingatia kwamba maeneo haya mabwawa yaliyokuwepo mwaka huu yamekauka kwa kuwa mvua ilikuwa ni ndogo?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema ni kwamba nawapongeza sana wananchi wa maeneo hayo kwa kuchukua hatua ya kuwekeza katika huduma ya maji. Namwomba Mheshimiwa Sendeka tuonane tuzungumze ili tupeleke wataalam wetu kwenda kuelewa kiasi gani cha uwekezaji ili kuona mpango wa maji vijiji unahusianaje na maeneo hayo kama si kwa mwaka huu basi tufikirie kwa ajili ya mpango unaoendelea mwaka ujao. *(Makofi)*

Na. 105

**Barabara kutoka Natta – Mugumu**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara kutoka Natta – Mugumu, imeharibika sana na mabasi makubwa yaliyokuwa yakitumia barabara hiyo yamelazimika kuiacha na kusababisha kero kubwa ya usafiri kwa wananchi wa Serengeti:-

(a) Je, ni lini Serikali itaifanyia matengenezo barabara hiyo na itakamilika lini?

(b) Je, matengenezo yatagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnamka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Natta – Mugumu yenye urefu wa kilometa 37 ambayo ni ya kiwango cha changarawe na udongo inamilikiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaelewa umuhimu, kiwango cha uharibifu na kero wapatazo wananchi wa Serengeti wanaotumia barabara ya Natta – Mugumu. Kwa kuzingatia hali hiyo na kama hatua ya muda mfupi, Serikali kupitia Wakala wa Barabara imepanga kuifanyia matengenezo makubwa kwa kiwango cha changarawe barabara hiyo kwa kutumia fedha za Mpango wa kuendeleza Sekta ya Barabasra unaofadhilimiwa na *NORAD.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kuwapata makandarasi *procurement* zimekamilika na makandarasi wawili wameanza kazi. Mkandarasi wa kwanza anatengeneza kilometa 18 kuanzia Natta hadi Nyakitono na wa pili kilometa 18.6 kati ya Nyakitono hadi Mugumu.

Matengenezo haya yamepangwa kuchukua muda wa miezi sita, hivyo yatakamilika kati ya mwezi Novemba na Desemba, 2006. Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mpango wa muda mrefu, barabara hii, ambayo ni sehemu ya barabara ndefu ya Natta – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu itaanza kufanyiwa upembuzi yakinifu na wa mazingira yaani *environmental impact study* mwaka 2006/2007 ili hatimaye ijengwe kwa kiwango cha lami.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za kazi nilizotaja za kutengeneza barabara ya Natta – Mugumu kwa kiwango cha changarawe ni shilingi za Kitanzania milioni 256.817 kwa sehemu ya kwanza na milioni 297.267 kwa sehemu ya pili. Tunaamini kwamba kukamilika kwa matengenezo hayo kutaondoa kero ya usafiri kwa wananchi wa Serengeti hasa wa mabasi makubwa na pia wasafiri wengine wakiwemo watalii.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza. La kwanza kwa kuwa Wizara ya Miundombinu imeamua kulivalia njuga tatizo la hii barabara na kumfanya hata Mheshimiwa Waziri Mramba aje mwenyewe kuiangalia na vile vile kuitafutia pesa kutoka kwa Wafadhili ambazo amepata. Je, Mheshimiwa Waziri Mramba uko tayari kuja Serengeti ili wananchi waweze kumshukuru na kumwombea dua ili Mwenyezi Mungu ampe afya njema, hekima na busara? *(Makofi/Kicheko)*

(c) Kwa kuwa barabara za kutoka Silori Simba hadi Lung'abure na ile ya kutoka Mto Mara mpaka Mugumu ambazo zinatengezwa na *TANROADS* na zenyewe zina hali mbali. Wizara ina mpango gani wa kuzitengeneza hizo barabara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika Waziri wangu yuko tayari kwenda Serengeti kupata shukrani hizo. *(Makofi)*

La pili, kuhusu barabara alizozitaja za kutoka Silori Simba na zile za Mugumu ambazo zinatengenezwa na Wakala wa Barabara yaani *TANROADS* Mkoa wa Mara, kutokana na ufinyu wa fedha, barabara hizi zitaendelea kutengenezwa maeneo korofi ili ziendelee kupitika katika wakati wote wa mwaka mzima wakati ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha za kutengeneza barabara hizo kwa kiwango ambacho kitaridhisha zaidi.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa Serengeti inapakana na Wilaya ya Tarime na pia Wilaya ya Tarime iko pembeni mwa Hifadhi ya Serengeti na ina umuhimu vile vile katika masuala ya kitalii. Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara ya kutoka Tarime kwenda Mugumu ambayo itaiunganisha na mpango mkubwa wa Serikali wa kutengeneza barabara kutoka Arusha hadi Musoma kwa sababu iache kuwa Wilaya ya pembezoni. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hiyo ya kutoka Tarime kwenda mpaka Mugumu ikiungana na barabara hii ambayo kuna mpango wa

kuitengeneza ya kutoka Musoma-Mugumu-Loliondo-Mto wa Mbu itakuwa rahisi kwa wananchi na wengine watalii wanaotoka mipakani kutokea Sirari, Tarime kuja Mugumu kuunganisha barabara hiyo, itawezesha usafiri huo kuwa nzuri.

Lakini Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mpango wa kwanza tumenuia tujenge kwanza barabara hii ambayo nimeizungumzia na katika hatua inayofuata barabara hiyo ya kutoka Tarime kuunganisha kwenda Mugumu itawekwa kwenye mpango. Lakini kwa sasa barabara hiyo itaendelea kutengenezwa kwa kiwango cha kuridhisha ili wananchi waweze kupita bila matatizo yoyote. Lakini kwa mpango wa muda mrefu barabara hiyo na yenyewe itaunganishwa na Mugumu. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILIMBAH:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali dogo la nyongeza. Kule jimboni kwangu Iramba Magharibi nina barabara kama iliyozungumzwa kwenye swali la msingi inayotoka Kizaga-Mbago-hadi Singida. Barabara hii ilijengwa kwa kipindi cha mwaka 2004/2005 lakini barabara hii baada ya kukabidhiwa ni kipindi cha miezi sita tu ikawa imeharibika na ikawa haipitiki. Kwa hiyo, namwuliza Mheshimiwa Waziri, Wizara inasemaje kuhusiana na barabara hiyo ilivyojengwa na hasara iliyopatikana. Je, yupo tayari kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili iweze kupitika na kuondoa usumbufu uliopo sasa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu swali alilolileta ni swali jipya, awasiliane na sisi ili tuweze kuangalia hiyo barabara ni barabara gani na ina matatizo gani ili hatua za kurekebisha ziweze kufanyika. *(Makofi)*

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuniona. Kwa sababu nimesimama sana hatimaye lakini mwishoni umenipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa tatizo la barabara si Serengeti peke yake, hata hapa Dodoma pia lipo. Je, ni lini Serikali itatengeneza barabara ya kuelekea Chimwaga ambapo vikao muhimu vya Chama Tawala huwa vinafanyika pale na ukizingatia pia Chuo Kikuu kipya kinatarajiwa kujengwa Chimwaga. Barabara ile ina vumbi haipitiki. Naomba nisikilize majibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongezea majibu ya maswali ya nyongeza yaliyojitokeza kwa swali hili. Kwanza niseme kwamba kwa taarifa ya Mheshimiwa Dr. James Wanyancha wakati wa Pasaka nilikagua barabara yote hiyo aliyoitaja kwenye swali lake ili kuridhika kwamba kweli ilikuwa muhimu kuitengeneza. Kwa hiyo, kama anataka nije nitakuja tena kuangalia miradi mingine ya barabara. Na nawaomba waandaye ngoma mzuri ili kuonyesha shukrani zao kama alivyoonyesha yeye mwenyewe.

Ya pili, kwa hili la Dodoma ningependa kurejea sera iliyoko kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba kwa sasa hivi barabara za lami zitakuwa zile za kuunganisha Mkoa na Mkoa. Kwa mfano, nichukue mfano wa Mkoa wa Dodoma, kazi tunazofanya sasa hivi ni kuunganisha Dodoma na Morogoro ama kwa kukarabati barabara zilizokuwepo ziwe

nzuri zaidi au kwa kujenga mpya na ndiyo maana sasa tuna mradi wa Dodoma hadi Singida-Manyoni-Dodoma-Morogoro na tunaendelea kushughulikia mradi wa Dodoma kuunganisha na Mkoa wa Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunashughulikia Mkoa wa Dodoma kuunganisha na Mkoa wa Iringa. Hizi zote zitakuwa kwenye Bajeti hii ijayo ambayo naisoma Jumatatu. Nina hakika Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni watiifu kwa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), watanielewa na wataniunga mkono. Hizi barabara za mjini, Manispaa ya Dodoma, wiki mbili zilizopita kwa hisani na Waziri wa Fedha tulikutana hapa na Mwenyekiti wa Benki ya Kiarabu yaani *BADEA* na katika mambo tuliyozungumza naye na kukubaliana naye ni kwamba barabara za mji wa Dodoma zitachunguzwa upya ili zifanane na za Mji Mkuu. Hii ikiwa ni pamoja na maeneo ya kwenda hadi Chimwanga kama alivyouliza Mheshimiwa Chifupa na kwamba wataalam watafika hapa mwezi ujao kuangalia yenyewe inayotakiwa ifanywe ikiwa vilevile ni pamoja na kurefusha kidogo barabara ya kiwanja cha ndege cha hapa Dodoma na kuangalia uwezekano wa kujenga kiwanja kipya cha ndege mkoani Dodoma.

Kwa hiyo, kazi hizo tunazifanya kwa pamoja ningeomba tu kwamba avute subira mpaka hiyo benki ya *BADEA* itakapofikia mahali pa kutoa kauli ili tuweze kusema kwa uhakika zaidi, lakini juhudi zinazoendelea na ndizo hizo. *(Makofi)*

Na. 106

**Uzalishaji wa Mazao ya Mifugo Nchini**

**MHE. MARTHA MOSSES MLATA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kuwa na idadi ya mifugo mingi:-

(a) Je, uzalishaji wa mazao ya mifugo kama nyama na maziwa ukoje ikilinganishwa na nchi nyingine wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki?

(b) Je, uzalishaji huo unalinganishwaje na matumizi (ulaji) ya ndani ya nchi na viwango vya ulaji vinavyopendekezwa na Shirika la Afya Duniani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, Mbunge wa Viti Maalumu, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Tanzania, yenye ng’ombe milioni 18.5, ni nchi ya tatu barani Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ikizifuatia Sudan yenye ng’ombe milioni 38 na Ethiopia yenye ng’ombe milioni 35.

Uzalishaji wa maziwa hapa nchini unakadiriwa kuwa lita bilioni 1.4, mwaka 2004/2005 ikilinganishwa na lita 1.2 bilioni mwaka 2003/2004, ambalo ni ongezeko la asilimia 18.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji wa maziwa nchini Kenya unakadiriwa kuwa lita bilioni 2.8 kwa mwaka 2004/2005 na Uganda ni lita bilioni 1.1 kwa mwaka 2004/2005. Hii inaonyesha kuwa uzalishaji maziwa nchini Kenya ni mkubwa zaidi ikilinganishwa na nchi za Tanzania na Uganda. Kwa upande wa nyama, uzalishaji ulikuwa tani 378,509 mwaka 2004/2005 ikilinganishwa na tani 348,800 mwaka 2003/2004.

Hili ni ongezeko la asilimia 8.5. Kati ya kiasi hicho kilichozalishwa, tani 204,520 zilikuwa za nyama ya ng'ombe, tani 78,093 za mbuzi na kondoo, tani 27,000 za nguruwe na tani 68,896 za kuku.

Vile vile, uzalishaji wa nyama nchini Kenya ulikuwa tani 446,556 kwa mwaka 2004/2005 na Uganda ulikuwa tani 248,152 kwa mwaka 2004/2005. Hivyo uzalishaji wa nyama nchini Kenya ni mkubwa zaidi kuliko Tanzania au Uganda.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, unywaji wa maziwa hapa nchini unakadiriwa kuwa lita 39 kwa mtu kwa mwaka na ulaji wa nyama kilo 10.3 kwa mtu kwa mwaka. Ulaji unaopendekezwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)*, ambalo lina jukumu la kuweka viwango hivyo, ni lita 200 za maziwa na kilo 50 – 60 za nyama kwa mtu kwa mwaka.

Kutokana na takwimu hizo ni dhahiri kwamba viwango vya unywaji wa maziwa na ulaji wa nyama ni vidogo ikilinganishwa na mapendekezo ya Shirika la *FAO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii ya ulaji mdogo imesababishwa kwa kiwango kikubwa na Watanzania walio wengi kutokuwa na utamaduni wa kunywa maziwa na kula nyama kwa wingi. Matokeo ya dhana hiyo ni kuwa na soko la ndani finyu kwa mazao haya mawili ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulaji mdogo wa nyama na unywaji mdogo wa maziwa uchukuliwe kama changamoto k wetu sote. Napenda kutumia fursa hjii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge washiriki katika jitihada za kuhamasisha jamii unywaji wa maziwa na ulaji wa nyama na bidhaa nyingine za mifugo ili kuboresha afyaza wananchi na kupanua wigo wa soko la bidhaa hizo.

**MHE. MARTHA M. MLATA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nitakuwa na swali la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:

Kwa kuwa wananchi wa Mkoa wa Singida pamoja na Mikoa ya jirani kama Manyara, Tabora pamoja na Shinyanga wanajitahidi sana katika sekta hii ya ufugaji hasa ufugaji wa ng'ombe. Lakini wanakosa soko la uhakika wakati huo huo wananchi wa

Tanzania wanapata nyama pamoja na maziwa kutoka Argentina, Zimbabwe, Afrika ya Kusini na nchi nyingine duniani. *(Makofi).*

(a) Je, Serikali itawasaidiaje wafugaji hawa ili waweze kufaidi soko lao la hapa nchini?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu kwamba wakati sasaumefika wakati sasa kuweka kiwanda cha kusindika nyama katika mikoa hiyo ya wafugaji niliyoitaja?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Kwa sasa hivi uzalishaji wa maziwa na nyama unaendena na ile idadi ya wananchi, lakini suala la msingi tunalosisitiza hapa ni usindikaji wa mazao haya, kwa sababu kwa kiwango kikubwa mazao ya maziwa kwa mfano yananywewa bila kusindikwa.

Kwa hiyo, la msingi ni maziwa kusindikwa. Kwa hiyo, Serikali inahimiza uwekezaji katika usindikaji wa maziwa lakini vilevile Serikali inahimiza uwekezaji katika machinjio za kisasa na viwanda vya nyama na kwa kufanya hivyo soko kwa mazao ya maziwa na nyama yatapatikana kwa wafugaji wetu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa kiwanda cha usindikaji wa nyama kwenye mikoa yenye mifugo wengi napenda kusema kwamba tayari kuna machinjio ya kisasa iko hapa Dodoma na kuna machinjio nyingine inakamilika hivi karibuni huko Mvomero, Mkoani Morogoro, na nyingine iko Mkoa wa Rukwa. Machinjio zote hizi zitatoa soko la mazao ya mifugo na kuwezesha usindikaji wa nyama.

Lakini vilevile Serikali bado inaendelea kuhimiza uwekezaji wa viwanda vya nyama kwenye mikoa yenye mifugo wengi kama vile Shinyanga, Mwanza, Arusha, Manyara na kwingineko.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tutakubaliana kwamba maswali yamekwisha na muda wa maswali pia umemalizika. Nichukue fursa hii kuwatambulisha kwanza mgeni kutoka Marekani ambaye ni Mkurugenzi wa Kitengo cha wanawake, huyu anaitwa Shiney, kama yupo asimame, *Speakers Gallery. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yeye majukumu yake kule Marekani ni pamoja na kuboresha hali ya wanawake, hususan masuala ya kipato na mazingira. Huyu ni mgeni wa *TWPG* hapa chini na ambaye Mwenyekiti, ni Mheshimiwa Anne Makinda, Naibu Spika wa Bunge letu. *(Makofi)*

Vile vile atapata fursa na kuzungumza na *secretariat* ya *TAPAC* na kiserikali ni mgeni wa Wizara ya Mipango. Nimtambue Ndugu Cosmas Kasangani, Katibu wa CCM Bukoba Mjini, ambaye ni mgeni wa Mheshimiwa Batenga. Nimtambue pia Dickson Molongo kutoka Bunda, ni mgeni wa Mheshimiwa Steven Wassira.

Naomba niwatangazie Wajumbe wa Chama cha Utendaji ya Chama cha Idadi ya Watu na Maendeleo kuwa wakutane saa tano kwenye chumba cha *CPA*, tangazo hili limetolewa na Mwenyekiti, wao Mheshimiwa Paul Kimiti.

Pia kuna tangazo kwamba leo tarehe 28 Juni, 2006, Mheshimiwa Spika, saa nane mchana atazindua rasmi Baraza la Wafanyakazi la Bunge. Hivyo Wajumbe wote wa Huduma za Bunge wanaombwa kuhudhuria uzinduzi utafanyika chumba Na. 37 kilichopo katika Ukumbi wa Bunge wa zamani.

Taarifa ya kikao Mheshimiwa Anne Makinda anawatangazia Wajumbe wote wa *TWPG* kwamba kutakuwa na kikao saa saba mchana ukumbi wa zamani wa mikutano ya Bunge, agenda ya kikao hicho ni kukutana na mgeni wetu Ndugu Shiney kutoka Marekani Wizara ya Kazi, mnaombwa wote kuhudhuria.

Pia kuna tangazo la kikao cha Kamati kutoka kwa mheshimiwa Anne Abdallah, anasema naomba uwatangazie Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Wajumbe wa *The Inter-Parliamentary Committee for East Africa* kuwa kutakuwa na kikao leo tarehe 28 saa saba mchana chumba Na. 219 gorofa ya pili katika jengo la Utawala.

Tangazo la mwisho ni kutoka kwa Mheshimiwa Mwenyekiti, wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Missanga, kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu, wakutane leo saa saba mchana katika ukumbi Namba 432 gorofa ya nne katika jengo la Utawala , kwa ajili ya kukutana na watendaji wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA). Sasa baada ya matangazo hayo, Katibu endelea na *Order Paper*.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2006/2007
### Ofisi ya Waziri Mkuu

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza kwa kunipa nafasi ya kwanza asubuhi ya leo ya kuchangia Hotuba hii ya Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kabla ya yote nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa Hotuba yake nzuri aliyoitoa ndani ya Bunge hili Tukufu. Pia niwapongeze Mawaziri na Manaibu Mawaziri walioko katika Ofisi hiyo. Pia niwapongeze Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu na Wataalam wote walioshiriki kuandaa hotuba hii.

Kama walivyosema wachangiaji wa mwanzo kwamba hotuba hii nzuri, ila ninaomba uzuri wa hotuba hii isiishie kwenye kitabu bali ifikie wananchi ili waweze kufaidika na yale yaliyomo katika hotuba hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti, wa Chama chake pamoja na wale wote waliochaguliwa na watakia heri katika nyadhifa zao hizo mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kuchangia katika Hotuba hii ya Waziri Mkuu ya Bajeti kuna jambo moja ambalo ningependa kulisema ili kama kuna viongozi wengine wanaofanya hivyo waweze kuliacha na jambo hili lilitokea siku ya Jumapili, katika Kanisa nililokwenda kusali, huwa kuna au tuna utaratibu wa kutambulishwa, wageni na baada ya hapo huwa tunasalimu kwa wale Wakristo salamu inayojulikana ni Bwana Yesu Asifiwe.

Lakini kwa bahati mbaya kuna mjumbe mmoja aliyejitambulisha badala ya kutumia salamu hiyo alitumia salamu ya chama chake. Simlaumu mjumbe yule kwa sababu inawezekana hakujua. Tatizo lililonifanya mimi leo kusema hapa leo mbele ya Bunge lako Tukufu ni Mchungaji aliyekuwa anaongoza ibada ile kuidhinisha jambo lile kwamba ni halali kwa bahati mbaya sana Washarika waliguna. Lakini Mchungaji yule alisema ni sahihi kwa sababu chama kinachoongoza ni chama chake na kimetoa Rais wa nchi. (*Makofi*)

Sina tatizo na hilo ninajua Rais ni Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Hatuna ubishi na hilo, tatizo langu kwa nini tuingize siasa kwenye nyumba ya Mwenyezi Mungu, tunakwenda kusikiliza neno la Mungu, na tunawaomba viongozi wa dini tunawaheshimu sana, wao waendelee kuifanya ile kazi ambayo wametumwa na Mwenyezi Mungu kutufundisha na kazi ya siasa watuachie sisi Wanasiasa. Kama wameona upande wa pili unafaa zaidi basi waache kule waje huku tupambane kwenye majukwa ya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda sasa nije kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Waziri Mkuu kwa kazi nzuri waliyoifanya baada ya kupata tatizo la njaa. Kwa kweli viongozi wetu walijitahidi na kuhakikisha kwamba Watanzania hawafi kwa njaa.

Lakini ningependa kutumia nafasi hii sasa kwamba tujifunze kutokana na hili kwa sababu ni aibu kwa Watanzania kukumbwa na njaa, kwa sababu tuna ardhi kubwa sana tuliyojaliwa na Mwenyezi Mungu, ambayo mpaka sasa haijaguswa. Kwa hiyo, sasa ni kipindi muafaka cha kupanga mikakati yetu vizuri ili tusije tena tukapata tatizo hili la njaa katika nchi yetu.

Bajeti iliyopita ya chakula ya mwaka jana 2005/2006 kulikuwa na suala la umwagiliaji maji mashambani, sijui lilifanikiwa kwa kiasi gani lakini sasa tujifunze ili yale yote tuliyopanga katika Bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu yatekelezeke na tusipate tena tatizo hili la njaa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuzungumzia suala la ujambazi katika nchi yetu na hili pia napenda nilipongeze Jeshi la Polisi na Waziri wa Usalama wa Raia pamoja na *IGP* kwa kazi nzuri walioifanya mpaka sasa ambayo wameweza kupambana na majambazi, na kwa kiasi fulani wameweza kufanikiwa. Pia niwashukuru wananchi walioshirikiana na Serikali yetu, kwa misaada mbalimbali waliyoitoa katika Jeshi letu la Polisi ya vifaa pamoja na pesa na mali ambayo imewatia moyo askari wetu polisi na wameanza kuifanya kazi yao vizuri.

Pia ningependa kuwaomba wananchi waendelee kutoa ushirikiano mzuri katika jeshi letu hili la polisi ili waweze kuifanya kazi yao, na pia ningeiomba Serikali na ile Wizara inayohusika basi wawaangalie vijana hawa katika mishahara yao na posho zao mbalimbali ili waendelee kuifanya kazi yao kwa uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda sasa niingie katika suala la utawala bora. Kumekuwa na matatizo katika sehemu mbalimbali ya nchi yetu katika yale maeneo ambayo yanaongozwa na Wenyeviti kutoka Vyama vya Upinzani kuondolewa katika uongozi bila kufuata taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata tatizo hili katika kijiji cha Kichangani, katika Jimbo la Ulanga Magharibi, Mwenyekiti wetu wa Kijiji alitumiwa barua ya kuondolewa katika uongozi bila kufuata utaratibu na alipoulizwa aliyepeleka barua, mtendaji wa kijiji alidai kwamba alipata maelekezo kutoka kwa Diwani wa Chama cha Mapinduzi. Sasa ninapenda kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, hii nchi ni nchi yetu sote hakuna mtu mwenye hati miliki ya nchi hii, Mwenyekiti yule wa CHADEMA aliyechaguliwa na wananchi ana haki kama walivyo Wenyeviti wengi waliochaguliwa kupitia Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Tunawaomba ndugu zangu na wale viongozi wa Chama cha Mapinduzi hebu tufuate utaratibu wa sheria kama Mwenyekiti, yule alikuwa na madhambi basi ingetumika sheria. Walitumia kigezo cha kesi iliyokuwa katika kijiji kile iliyotolewa hukumu kumwondoa Mwenyekiti yule kwa kijiji kwenye uongozi pamoja na wajumbe wake, ambao wajumbe ambao wametoka katika Chama cha *TLP, CUF* wakaondolewa katika uongozi.

Sasa tunasema huu sio utawala bora, Mheshimiwa Rais wetu ameonyesha njia na anataka nchi yetu hii iwe moja, tusiwe na tofauti za vyama tunachotakiwa sisi ni kufanya kama Watanzania ni kuleta maendeleo kwa Watanzania wote bila kujali itikadi zao za Vyama.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nategemea hili Wizara inayohusika italifanyia kazi na tutapata majibu katika mwisho wa bajeti yao watakapotoa maelezo katika Bunge lako hili Tukufu. Kijiji cha Kisangani katika Jimbo la Ulanga Magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningenda kuzungumzia suala zima la Makao Makuu Dodoma. Hii ni Bajeti yangu ya sita katika Bunge lako hili Tukufu na kila

ninapopata nafasi ya kuzungumzia huwa nazungumzia suala hili la Makao Makuu Dodoma. Hili limekuwa jambo la muda mrefu sasa kwa sababu kila tunapokuja katika Bunge lako Tukufu kujadili swala hili tunaambiwa kuna mpango wa kuhamia Dodoma, lakini mpango huu huwa hautekelezeki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuweza kuleta Chuo Kikuu kitakochojengwa Dodoma na hii nampngeza kwa sababu ni sera ya CHADEMA toka mwaka 1992 ya kujenga vyuo katika Mkoa wa Dodoma, na sera bado ziko nyingi tunawakaribisha mweze kuzichukua kwa sababu mtakapozifanyia kazi ni kwa manufaa ya Watanzania wote bila kujali ametoka chama gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuhamia Dodoma ni la miaka mingi sasa tufike wakati sasa tuweke mipango yetu dhahiri kama kweli tunataka kuhamia Dodoma. Katika kitabu cha maendeleo zimetengwa bilioni moja za kujenga Ofisi ya Waziri Mkuu Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajiuliza tuna nia ya kuhamia Dodoma, wakati mnakarabati Ofisi zilizoko Dar es Salaam, niliwahi kuuliza hapa Bungeni kwamba kama kweli tuna nia ya kuhamia Dodoma kwanini nyumba za Mawaziri zinajengwa Dar es Salaam. Wakaniambia kwamba zinajengwa Dar es Salaam na Dodoma. Lakini nyumba zinazojengwa Dodoma hazina hadhi ya zile zilizojengwa Dar es Salaam. Siamini kabisa kwamba Mawaziri wale watakuja kukaa katika nyumba zile pale ambazo hazina fesi, hakuna miti, hawatakuwa tayari kuja kukaa pale.

Kwa hiyo, naiomba Serikali hii ya awamu ya nne. Kwa kasi hiyo hiyo waliyonayo basi, waielekeze kasi hiyo kuhamia Dodoam. Vingenevyo yatatimia yale maneno aliyosema Mheshimiwa Kabuye kwamba Dodoma itakuwa ni Makao Makuu ya Bunge na Makaburi ya viongozi. Hatutaki tufike hapo ningeiomba Serikali ihamie sasa Dodoma kwa sababu ni muda mrefu umepita tuweze kuleta hadhi ya mji wa Dodoma ionekane kweli ni Makao Makuu ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuipongeza Serikali hii iliyoanza na hasa Rais wa Awamu hii ya Nne kwa kitendo chake alichokifanya cha kuweza kukutana na Wabunge wa upande wa Upinzani na wale wa CCM. Tulikaa tulizungumza na Rais, na inaelekea Rais ana msimamo dhabiti wa kweli wa kutekeleza yale yote tuliyozungumza naye.*(Makofi)*

Ningependa kuchukua nafasi hii pia kuwaomba wale viongozi wengine walioko chini ya Rais, wafuate mfano wa Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ambao ameuonyesha kama kweli tunataka kuleta maendeleo katika nchi yetu, hatuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu kama tutaendelea kutengana katika vyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia yetu ni moja, mdau wetu ni mmoja basi wote tushirikiane kwa pamoja tuweze kuleta maendeleo katika nchi yetu hii na tuweze kutimiza zile ahadi zote tulizozitoa kwa wapiga kura wetu wakati wa kampeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache nakushuru kwa kunipa nafasi ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nianze kukushukur wewe kwa kunipa nafasi hii asubuhi hii ili na mimi niweze kuchangia kidogo katika hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri sana mimi sina matatizo na hotuba ya Waziri Wakuu. (*Makofi*)

Lakini kabla sijachangia hotuba yake, na mimi pia niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuongoza chama tawala cha Mapinduzi. Nampongeza sana kwa hilo.

Aidha niwapongeze na Wabunge wenzetu walioteuliwa ama kuchaguliwa na Chama cha Mapinduzi kushika nyadhifa mbalimbali, na nafikiri ni vizuri niwataje Mheshimiwa Yusufu Makamba, Mheshimiwa Agrey Mwanri, Mheshimiwa Rostam A. Azizi, Mheshimiwa Dr. Asha Rose Migiro, na Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana na mimi pamoja na wanachama wangu wa jimbo la Kondoa Kusini na Wilaya ya Kondoa kwa ujumla tutawapa ushirikiano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba na mimi nichangie maeneo machache ya Hotuba ya Waziri Mkuu. Nianze na shukrani kwa wapiga kura wangu wa Kondoa Kusini, wanaishukuru sana Serikali, kwa uamuzi wake wa kujenga Chuo Kikuu cha aina yake katika mji wa Dodoma. Nasema ahsante sana kwa zawadi na wapiga kura wangu wananiahidi ama wanaiahidi Serikali kwamba watachangia wanachuo pindi Chuo Kikuu hicho kitakapofunguliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe shukrani ya pili kama tunavyojua wote mwaka jana tulikuwa na tatizo kubwa sana la upungufu wa chakula katika nchi yetu wilaya ya Kondoa ni moja ya wilaya ambayo ilikubwa na tatizo kubwa la chakula ama njaa katika wilaya hiyo.

Pamoja na mwanzoni Serikali kubaini kwamba Wilaya ya Kondoa ilikuwa haina matatizo makubwa baada ya wawakilishi wake akiwemo Mbunge ama Wabunge wa Wilaya hiyo kueleza hali halisi, Serikali ilichukua hatua ya kufanya tathimini upya.

Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu yeye ndio alitoa maelezo kufanya tathimini upya na tathimini ilipofanyika ilionekana dhahiri kwamba Wilaya ya Kondoa nayo ilikuwa na upungufu mkubwa wa chakula. Kwa hiyo, Serikali ilitoa chakula hakikuweza kutosheleza mahitaji lakini kiliweza kusaidia sana kupunguza tatizo hilo, Kwa hiyo, wananchi wa Jimbo la Kondoa Kusini na Wilaya ya Kondoa kwa ujumla wanashukuru kwa msaada huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena nieleze kwamba bado tatizo la njaa katika Wilaya ya Kondoa liko pale pale kwa sababu hatukupata mvua za kutosha.

Lakini nasikitika kusema kwamba tathimini ya awali imeonyesha kwamba Wilaya ya Kondoa inajitosheleza kwa chakula. Si kweli, narudia kusema kwamba tathimini hiyo sio sahihi na naomba ofisi ya Waziri Mkuu itume wataalam tena, waende wakafanye tathimini upya na waweza kubaini ukubwa wa tatizo la chakula katika Wilaya ya Kondoa ili pindi muda utakapowaidia basi msaada uweze kufikishwa kwa walengwa, na napenda labda niwaelekeze kwamba hasa maeneo yaliyoathirika sana ni Tarafa mbili. Tarafa ya Farkwa na kwa-Mtoro katika Jimbo la Kondoa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa hizo zimeathirika mno na hasa hasa kata zifuatazo: Mpendo na Sazawa katika tarafa ya kwa Mtoro, na Gwadi, Farkwa na Makorongo katika tarafa ya Farkwa. Naomba wataalam watumwe katika kata hizo ili waweze kuona hali halisi ili pindi muda utakapowadia basi wananchi wa kata hizo waweze kupata msaada wa Serikali. Kwa kweli msaada unahitajika sasa katika kata hizo kwa hiyo ni vizuri wataalam wakatumwa mapema ili waweze kubaini tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la njaa katika Mkoa wa Dodoma linasababishwa zaidi na ukame bila ukame Mkoa wa Dodoma una eneo kubwa la kilimo na rutuba na sisi hatuhitaji mbolea hizo za chumvi chumvi kwa hiyo ni eneo lenye rutuba lakini tatizo ni upungufu wa mvua ama kwa kifupi ni ukame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimshukuru sana Waziri Mkuu katika hotuba yake amebaini vizuri sana tatizo hili na napenda ninukuu sehemu ya hotuba yake katika ukurasa wa 45 aya ya 56 kuhusu suala la ukame Waziri Mkuu anasema hivi: "Uzoefu tulioupata wakati wa kipindi cha ukame umeonyesha kuwa hatuna budi kukipa kipaumbele kilimo cha umwagiliaji maji kama mkakati wa kukabiliana na ukame kwa siku zijazo," mwisho wa kunukuu.

Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kutambua hilo na sisi katika Mkoa wa Dodoma tatizo linalotukabili ni hilo hilo kwa hiyo, tunaomba tusaidiwe wananchi wa Jimbo langu na Wilaya ya Kondoa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla tunaomba tusaidiwe ifuatavyo:-

Serikali ya Mkoa kwa kutambua kwamba hili tatizo ni la kudumu kwa nyakati tofauti ilifanya tathmini ama tafiti katika mabonde mbalimbali kwa lengo la kuanzisha miradi ya umwagiliaji maji katika mabonde hayo na bonde kubwa ambalo limebainika kwamba ni zuri kwa ajili ya umwagiliaji ama kilimo cha umwagiliaji ni Bonde la Mto Bubu na imefanyiwa tafiti mbalimbali na kutokana na tafiti hizo imebainika kwamba kama Serikali ama kama bwawa litajengwa katika Kijiji cha Farkwa katika Bonde hilo la Mto Bubu kuna uwezekano wa hekta 10,000 kumwagiliwa maji na kuna uwezekano wa kuzalisha tani 24,678 kila mwaka mazao mbalimbali yakiwemo mahindi, mpunga na karanga. *(Makofi)*

Sasa ombi la wananchi wa Mkoa wa Dodoma ni kwamba tusaidiwe tuweze kuanza mradi wa umwagiliaji katika bonde hilo, tunaomba tusaidiwe nataka niseme kwamba hatuna mpango wa kuhama mkoa huu lakini tatizo litakuwepo kama hatutasaidiwa kwa hiyo, tunaomba tusaidiwe ili tuweze kujitosheleza kwa chakula na kuweza kuzalisha na mazao ya biashara ili tuweze kuondokana na njaa ya mara kwa mara na pia kuweza kupunguza umaskini uliokithiri kwa wananchi wetu. Tunaomba sana hili lizingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo wananchi wamenituma niweze kuwasemea ama niweze kulifikisha kwa Serikali ni suala la barabara na barabara hapa nitazungumzia barabara moja tu ambayo Serikali imekuwa ikitoa ahadi kwa muda mrefu nayo ni barabara ya kutoka Babati – Kondoa – Dodoma – Iringa. Sipendi kueleza umuhimu wa barabara hii nimerudia sana kueleza umuhimu wa barabara na kila mmoja sasa hivi ameelewa tunachoomba sasa ni utekelezaji, tunaomba basi upembuzi yakinifu ambao ulikuwa unafanyika sasa tuanze kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Napenda niikumbushe Serikali kwamba Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, wakati alipokuwa anaomba kura aliahidi mara nyingi kwamba katika miaka mitano ya utawala wake atahakikisha ama awamu ya kwanza ya utawala wake atahakikisha kwamba barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Sasa tunaomba ahadi hiyo itekelezwe na hii ya lami amerudia rudia sana wakati akizungumza katika nyakati tofauti alipokuwa anahutubia wananchi wa Dodoma pale *Jamhuri Stadium*, alipokuwa Manyara alirudia ahadi hiyo, sasa bila shaka Serikali iko makini kutekeleza ahadi ya Rais.

Lakini nashangaa sana nimeangalia bajeti ya mwaka huu ya barabara hii imetengewa shilingi milioni 910 tu sijui utajenga barabara ya aina gani ya lami, lakini nimefarijika kuona kwamba kuna mpango mwaka 2007/2008 Serikali ina mpango wa kutenga shilingi bilioni 33 na mwaka 2008/2009 shilingi bilioni 38, jumla katika miaka hiyo ni shilingi bilioni 71. Tunaomba basi mpango huu utekelezwe kama ulivyopangwa kwa faida ya nchi yetu na kwa faida ya maendeleo ambapo barabara hii itapita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na ombi la mwisho la wapiga kura wangu na wananchi wa Wilaya ya Kondoa ambalo ni ombi la muda mrefu pia.

Napenda niiambie Serikali kwamba Wilaya ya Kondoa ni moja ya Wilaya kongwe sana katika nchi hii, ina umri wa zaidi ya miaka 100, imeanzishwa tangu wakati wa enzi za Ujerumani na mipaka yake haijabadilishwa mpaka leo lakini tunashangaa kuona kwamba Wilaya hii pamoja na kukua kwa maana ya idadi ya watu na pamoja na eneo lake ni kubwa na pamoja na wananchi kuomba Wilaya hii igawanywe katika Wilaya mbili ili iweze kutawalika vizuri Serikali kila ombi tunaambiwa tusubiri, hivi tunasubiri kwa miaka 100 tuendelee kusubiri kwa mingapi? Napenda na naomba Serikali ichukue hatua za dhati kugawa Wilaya hii katika Wilaya mbili kwa sababu haitawaliki na Mkuu wa Wilaya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Rais alipokuwa anahutubia ama alipokuwa anakutana na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hoja hii niliitoa na yeye akasema nimesikia sasa bila shaka ndiyo jibu lenyewe, naomba lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kugawa Wilaya pia Majimbo ya Wilaya ya Kondoa kwa kweli ni makubwa mno. Napenda niwarejeshe kwamba haya Majimbo yapo tangu tumepata Uhuru mwaka 1961, Kondoa ilikuwa na Majimbo mawili kitu kinachobadilishwa hapa ni majina tu leo inaitwa Ntomoko, keshokutwa jina lingine na kadhalika lakini Majimbo hayajagawanywa miaka 45. Majimbo makubwa jamani siyo tunashindwa lakini tunapata taabu sana kuyahudumia lakini majirani zetu naweza kusema majirani zetu kama Babati, Majimbo yamegawanywa mpaka yamekuwa ni madogo wanaweza kuyahudumia vizuri, hivi sisi wa Kondoa tuna kosa gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unafahamu mtatufikisha mahali tuseme kwamba labda haya Majimbo yanagawanywa kwa upendeleo, tunaomba tusifike hapo tunaomba Majimbo yetu yaongezwe na Rais ashauriwe jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi na naomba niunge mkono hotuba ya Waziri Mkuu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ANIA SAID CHAUREMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mimi kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa afya na kusimama leo mbele kwa mara ya kwanza katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwanza napenda kutoa shukrani zangu za dhati kabisa na za pongezi kwa Rais wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania na wajumbe wanzake ambao wamechaguliwa katika Chama chao katika nyadhifa za uongozi. Vile vile napenda kutoa pongezi kwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake yote kwa kutengeneza hotuba hii ambayo ndani yake ina malengo mazuri katika kutekeleza malengo ya kumwezesha mwananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila napenda kutoa shukrani za dhati kabisa na za pekee kwa baraza la uongozi la chama changu Chama cha Wananchi *(CUF)* pamoja na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa kuniwezesha kufika hapa leo na kusimama kuchangia katika kuendeleza Taifa letu hili kwa kuwakilisha wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais,Mazingira Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, katika swali langu la mara ya kwanza kulitoa katika Bunge lako hili alilipatia majibu na aliahidi kufika sehemu husika na alifika eneo la *Breweries* na wanachi wa Kata ya Jangwani na Kata ya Mchikichini wanatoa pongezi za dhati kabisa na Mheshimiwa amenipa taarifa kwamba ameiona hali halisi nategemea ataifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kabisa naanza katika hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 30 mpaka 36 Waziri Mkuu ameelezea kwa undani kabisa malengo na azma ya majukumu ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo makubwa katika Halmashauri, Halmashauri zetu ndiyo zinaongoza katika Wilaya hizi na katika Wilaya Halmashauri kuna viongozi ambao wamechaguliwa na wananchi mfano Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa lakini jambo la kusikitisha Mheshimiwa Waziri Mkuu hili nataka lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Jambo la kusikitisha ni kwamba kuna baadhi ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Madiwani hawashirikishwi katika shughuli zozote katika Kata zao na katika Mitaa yao. Haya nayasema nina uthibitisho kabisa kwamba mpaka leo toka uchaguzi ufanyike mwaka 2004 Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji bado baadhi yao hawajapewa miongozo ya kufanyia kazi na vilevile hawajashirikishwa katika vikao vyovyote, hali hii inawakosesha kufanya uwakilishi ambao wamekabidhiwa na wananchi naomba hili Mheshimiwa Waziri Mkuu ulifanyie kazi na ninatoa mifano ya sehemu, kuna Mtaa wa Kombo, Mtaa wa Miembeni, Mtaa wa Mtakuja, Mtaa wa Mtambani na Mitaa mingine ambayo ipo katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es salaam ni Mkoa ambao Serikali Kuu ndiyo inafanya kazi, bado Wenyeviti wanaohusika na Serikali za Mitaa hawashirikishwi katika kutekeleza majukumu yao, je, Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vitongoji wa Nyarubusu, je wa Mtwara, Tandahimba na kadhalika hawa nafikiri baadhi yao ndiyo watakuwa hawajui hata wafanye nini? Kwa hiyo, hii hotuba yako ukurasa wa 30 mpaka 36 kama hamkuwashirikisha kikamilifu Wajumbe hawa ambao nimewataja hapa kwa hiyo itakuwa ni kazi bure na azma yetu ya kulisukuma gurudumu la Taifa hili kimaendeleo halitakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kuna jambo ambalo linasikitisha zaidi. Daftari la wakazi linatakiwa kukaa kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Vitongoji na Vijiji lakini jambo la kusikitisha na la aibu kabisa Daftari la Wakazi wa Mtaa wa Mtogole, Tandale linachukuliwa na mtendaji na kesi yake inakwenda mpaka katika Halmashauri na mpaka Waziri Mkuu anaingilia kutoa amri kwamba Daftari lirudishwe katika Mtaa wa Mtogole lakini hadi hii leo nimesimama hapa Daftari halijarudishwa, hii ni dhahiri kuwakosesha Watendaji wa Serikali za Mitaa kufanya kazi zao sawasawa, naomba Waziri Mkuu ufuatilie kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya nasema kuhusu Mfuko wa Wanawake na Vijana. Mfuko huu wa Wanawake na Vijana Serikali iliazimia kuwaendeleza Wanawake na Vijana ili kujikwamua na umaskini lakini kitu cha kusikitisha mfuko huu unagawiwa kwa upendeleo, Mfuko huu unagawiwa kwa upendeleo, narudia kwa sababu Vijana wengi kuna baadhi ya kundi la vijana limenijia na kusema kwamba wamekwenda katika eneo lao na kuambiwa hakuna kitu kama hicho, hali hii inarudisha nyuma maendeleo ya Vijana na Wanawake, naomba elimu itolewe ya kutosha ili Wanawake na Vijana wapate kufaidika na mfuko huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vile vile kuna asilimia ambayo inarudi vijijini kutoka Halmashauri, katika Halmashauri nyingi inafanya vizuri lakini kuna baadhi ya Halmashauri asilimia ile inakuwa hadithi kurudi vijijini ili kuleta maendeleo kwa wananchi. Naomba mambo haya yaangaliwe kwa undani kabisa na kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nazungumzia suala la afya, suala la afya ni uhai wa binadamu. Kwa kweli Jiji la Dar es Salaam ni Jiji kubwa sana linahitaji hospitali za ziada kila sehemu, wakati umepita sasa wa kujenga hospitali mabanda tu sasa hivi hospitali kwa sababu Dar es Salaam nafasi ni ndogo zijengwe ghorofa angalau basi ghorofa mbili kuwawezesha wagonjwa wanoumwa afadhali wapande juu na wale wanaozidiwa wapande juu. Hali hii imejidhihirishia katika hospitali ya Ilala, Mwananyamala na Temeke, lakini kabla sijasema kwanza napongeza Halmashauri ya Ilala kwa kusimamia kuongeza hospitali ya akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku niliingia hospitali saa 6 usiku kwa kutaka kutafiti na kuangalia hali niliyoikuta kwa kweli inatisha, nilikuta hospitalini Ilala Wodi ya Wazazi karibu wazazi 60 ma-*nurse* wawili mzazi mmoja ana kifafa cha uzazi, mzazi wa pili anataka kuhudumiwa yaani anataka kujifungua, mzazi mwingine ana *bleed* sana na ma-*nurse* wawili wamechoka hawawezi kuwahudumia wagonjwa wote kwa usiku mmoja. Kwa hiyo, hii inafanya kabisa suala zima la wazazi liwe ni unyanyasaji na naomba sisi wazazi ndiyo tunaojenga Taifa hili tuangaliwe sana na ma-*nurse* waongezwe katika hospitali wasiachiwe ma-*nurse* wawili usiku mmoja. *(Makofi)*

Vile vile hali hiyo katika Wodi ya Watoto, watoto kitanda kimoja wanalala watoto mpaka watatu au wanne, mtoto mmoja anaharisha, mmoja anatapika na mmoja ana malaria, hali hii mzazi anasimama kutwa kuhakikisha mtoto wake anamwangalia ili asitapikiwe na mtoto mwingine au asiharishiwe na mtoto mwingine. Ikifika usiku wazazi wamechoka wanachukua watoto wanalala kwenye ma-*corridor* hali hii Mheshimiwa Waziri Mkuu kutokana na hotuba yako hii naomba ziangaliwe sana sehemu hizi ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha sana zaidi ni kuona mgonjwa wa UKIMWI na mgonjwa wa kifua kikuu wanalala kitanda kimoja, hii vile vile ni hatari sana kwa sababu unapomchukua mgonjwa wa UKIMWI ukalaza kitanda kimoja na mgonjwa wa kifua kikuu na ule wa kifua kikuu mtu akikohoa mwingine anaweza kupata maradhi kwa kuvuta hewa kwa hiyo, unamfanya yule wa UKIMWI afe haraka na siyo kumsaidia katika matibabu. Tunaomba liangaliwe magonjwa ya kuambukiza yatafutiwe eneo muhimu na kubwa na lijengwe na watu wa magonjwa ya kipindupindu, UKIMWI na kifua kikuu tuwaweke eneo lao na tuwaangalie kwa hali na mali, hawa vile vile ni wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naendelea ugonjwa wa kipindupindu katika Jiji la Dar es Salaam umekuwa sugu sana na hii inatokana na bwawa la Spenko ambalo liko Vingunguti. Bwawa hili linaangaliwa na *DAWASCO* wanakuja kumwaga maji machafu katika eneo ambalo wanakaa wananchi na mvua nyingi zinanyesha na hivyo bwawa hilo

linatema na hatimaye husababisha kuingia katika mfereji wa Msimbazi na wauza michicha, bamia na karoti wanachukua maji yale kumwagilia katika mimea hii na hatimaye tunakuta Jiji la Dar es Salaam kipindupindu hakiishi. Tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu Bwawa la Spenko lihamishwe Vingunguti na liende moja kwa moja kwenye Mikoko kwa sababu maji yale yanaingia baharini hakuna sababu ya kuwa katika mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nimetumwa nilisemee ni kuhusu wazee, Rais aliyepita alitoa kabisa kipaumbele kwa wazee kwamba watibiwe bure lakini hadi hii leo wazee wanahangaika mzee akiumwa kwanza aende kwenye kata au kwenye mtaa kama hajamkuta mzee wa mtaa hawezi kupata barua. Kwa hiyo, wazee waangaliwe kwa jicho la huruma na wazee vile vile na walemavu wapewe vitambulisho maalum ambavyo moja kwa moja mtu akiumwa anakwenda hospitali badala ya kwenda kutafuta barua katika Serikali zetu za Mitaa na Vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia vile vile suala la sisi Wabunge wa Viti Maalum. Sisi Wabunge wa Viti Maalum hatushiriki katika Vikao vya Halmashauri zetu kwa hiyo, katika hali hii kuna sheria ambayo tumeambiwa kwamba inataka kurekebishwa. Tunaomba Wizara husika ilete sheria hii katika Bunge ili tupate nafasi ya kuingia katika Halmashauri na Manispaa kuwawakilisha wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ni kwamba wananchi wa Kipawa wameniagiza Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere wa Kipawa ulikuwa unataka kupanuliwa kuanzia miaka 10 iliyopita wananchi waliambiwa kwamba lilishafidiwa eneo lile na hawana ruhusa ya kukarabati wala kujenga maeneo yao, kwa hali hiyo wananchi wale wamekuwa wakinyanyasika, nyumba mbovu lakini hawana mamlaka ya kujenga, sasa wanaiomba Serikali kama imeazimia kupanua kweli Uwanja wa Mwalimu Nyerere basi iwalipe mafao yao na iwalipe viwanja ambavyo wakati huu wakisubiri kuvunjwa kwa eneo lile watengeneze nyumba zao na hatimaye mtakapokuwa tayari kupanua Uwanja wa *Mwalimu Nyerere International Airport* wananchi wale tayari walishakuwa na nyumba zao na hii itakuwa mmewasaidia vile vile bila ya matatizo yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho nazungumzia kwamba sasa hivi naiomba Serikali iangalie suala zima la viwanja vya watoto, watoto wanadhalilika sana siku za sikukuu, watoto wanakwenda baharini, wanagongwa na magari, watoto siku za *Christmas* na *Eid* wanahangaika sana na wanatia huruma hawa ni watoto wetu lakini tutenge maeneo ambayo tutatengeneza mabembea na tutatengeneza vitu ambavyo watoto nao wanakwenda kuburudika kama tunavyoburudika sisi wazazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:-** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Awali ya yote napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri ambayo imelenga katika sehemu zetu za maisha ya kila siku.

Kabla ya kuchangia napenda kumpongeza Rais, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa CCM pamoja wale Wabunge waliochaguliwa kwa nyadhifa zao tofauti. Vile vile napenda kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri, Wabunge waliochaguliwa na walioteuliwa katika Bunge hili Tukufu.

Pamoja na hayo napenda kuwashukuru Watanzania wote waliokipigia chama changu cha CHADEMA kura na kukiwezesha chama changu kuweza kuniteua mimi kuwa Mbunge katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Kabla sijaanza kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu  kwa kukaa na sisi Wapinzani pamoja na Chama Tawala na kuonyesha demokrasia ya kweli. Mheshimiwa Rais ameonyesha kwamba hana ubaguzi, lakini jumapili cha kusikitisha unaangalia kwenye televisheni unasikia mtu anaimba wapinzani tuwachanechane, tuwatupe tuwapeleke mbali sidhani kama hili ni jambo zuri.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia  napenda kumpongeza Waziri Mkuu kwa kuangalia suala zima la Afya. Waziri Mkuu katika ukurasa wa 58 amezungumzia suala la afya. Kwa kusisitiza napenda kuungana na Mheshimiwa  Ania Said Chaurembo kuhusu sekta hii Waziri Mkuu amesema atakarabati Hospitali za Wilaya, Zahanati na Vituo vya Afya, namwomba Waziri Mkuu auangalie Mji wa Dar es Salaam kwa mtazamo tofauti. Mji wa Dar es Salaam ina wakazi zaidi ya milioni 3 na hapo hapo Hospitali za Wilaya zilizoko Dar es Salam ni tatu tu Mwananyamala, Temeke na Mnazi Mmoja. Wakati Hospitali za Wilaya zinaweza zikatibu watu 100,000 na Vituo vya Afya watu 50,000 kwa hakika hospitali hizi haziwezi kukidhi mahitaji ya watu na hii itapelekea kutokuwa na huduma nzuri kwa wagonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ninachoomba kwa sababu watu wamekuwa wakienda kwenye hizo hospitali na wanakuwa ni wengi sana kwa wakati mmoja hii inapelekea ile Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kutumika kama *Dispensary*. Mtu anajikata hata na wembe anakimbilia Muhimbili inapelekea Madaktari Bingwa wanashindwa kuhudumia zile *emergency cases,* wanabaki kutibu au kuhudumia magonjwa madogo madogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Dar es Salaam haina Hospitali ya Mkoa, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliangalie hili *at least* mjaribu kufanya Wizara ya Afya. Igawe  hospitali kama jinsi Jeshi la Polisi lilivyofanya kugawa kazi zake kikanda, mkifanya hivyo itafanya Hospitali ya Muhimbili ipungukiwe na kazi katika kutibu wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine naomba Zahanati na Vituo vya Afya Vijijini mviboreshe muweke Maabara, mtu anakwenda kwenye hospitali kijijini hakuna vipimo vya kupimia damu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Tanzania hatuna tabia ya kupima afya zetu, lakini sasa hivi watu wanazingatia kupima afya zao wanafikiria ni UKIMWI tu. Vijijini watu wanaugua malaria kadhalika na *TB.* Hakuna elimu kule vijijini, mtu kama bibi mzee anaumwa na kichwa anakimbilia dukani anakwenda kununua *panadol* pengine anaumwa shinikizo la damu, tuwahimize watu wawe na tabia ya kwenda kupima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Afya ijaribu kutupa elimu, kuelimisha watu kwamba wanatakiwa kwenda kupima afya zao. Watu wakipima afya zao ina maana magonjwa ya malaria hayawezi kutokea na pia wawajulishe kule vijijini ni jinsi gani wanaweza kusaidia wajenge nyumba bora na kwa bei rahisi, unakuta kuna nyumba kijijini lakini dirisha ni dogo bibi au mama yupo pale anamhudumia mgonjwa wake mwenye *TB* na ya kuambukizwa kutokana na kutopata hewa nzuri kwa hiyo wakiweza kuwasaidia watu hawa tunaweza kupunguza magonjwa ya kuambukiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo naomba niende kwenye Ulinzi na Usalama wa Raia. Hivi karibuni tumeona kuna ajali nyingi sana zimetokea na Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumza kwamba ajali nyingi zimetokea kwa sababu kumekuwa na aidha, magari yanakimbizwa sana yaani yanakwenda kwa mwendo wa kasi. Sasa tujiulize katika hili Bunge Tukufu ilipitishwa sheria ya vidhibiti mwendo je, haya mabasi yanayotoka Moshi kwenda Dar es Salaam yana vidhibiti mwendo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukawa unapita barabarani linateremka basi la *Dar Express* au mabasi haya ya abiria linakimbia utafikiri ni *Air Tanzania* inataka kupaa, hapo hapo polisi wa usalama barabarani anatoka kwenye kichaka na kamera yake ananyoosha kama ana-*check speed limit,* hii ni hatari kwa yule polisi na kwa abiria vile vile. *(Makofi)*

Mimi ningeshauri mabasi yote aidha, ni abiria na dereva wote wawe na mikanda, zile *seatbelt* hii itasaidia kuzuia ajali nyingi ambazo zitatokea barabarani.

Vile vile Wizara husika ijaribu kuweka alama barabarani kumtahadharisha yule dereva kwamba kuna Polisi mbele ya safari au kuna *Police Camera* mbele ya safari. Hivi juzi tumesikiwa kwamba kuna Polisi wameuawa pale Tanga, pengine kungekuwa na alama kwamba kuna Polisi mbele ya safari, yule dereva angepunguza mwendo na hiyo isingeweza kutokea.

Kwa hiyo, naomba alama za barabarani ziwekwe na *speed limit* ziwekwe, siyo kuweka tu kwenye daraja au unapofikia karibu na kijiji. Pia watu wengi hatujui *speed limit* ya kuendesha barabarani kwa mfano barabara ya Shekilango watu wanaendesha mbio, hatujui tuendeshe kwa *speed limit* ya kiasi gani. Kwa hiyo, naomba Polisi waongezewe vitendea kazi, wakiwa barabarani wapewe *helmelt, vest* za *bullet proof* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hayo napenda niwapongeze jeshi la polisi kwa kuweza kudhibiti wizi lakini zaidi ya hayo wizi unaweza ukapungua zaidi kama ikiweza kuwekewa taa za barabarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Moshi na Dar es Salaam taa za barabarani hazifanyi kazi unaweza kukuta taa ya barabarani imeungua *bulb* ni ya kubadilisha tu *bulb* lakini hakuna mtu anayeshughulika kubadilisha zile *bulb*. Miji yetu ikiwekewa taa ina maana hata biashara itakuwa na watu watakuwa na uhakika wa usalama wao na ina maana wanaweza wakafungua maduka yao kwa muda zaidi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ina maana wakiweza kufungua maduka yao mpaka saa mbili usiku wakiwa na uhakika wa usalama wa biashara zao, hii itapelekea kuwa na mzunguko wa biashara na uchumi. Mara nyingi sasa hivi watu wanatoroka ofisini wanaenda kufanya *shopping* zao kwa sababu saa za kufungua maduka ni saa za ofisi. Wakifunga maduka kwenda *lunch* na wao wana mapumziko ya kwenda *lunch*. Mfano kama Mtaa wa Samora siku za Jumamosi saa 6.00 mchana maduka yote yameshafungwa, wale wafanyabiashara wanafunga maduka kwa sababu hawana uhakika na usalama wao. Kwa hiyo, tunaomba Jeshi la Polisi liangalie ni jinsi gani wanaweza kushirikiana na Wizara husika wakaweka ulinzi zaidi na wafanyabiashara wakaweza kufungua maduka yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezungumzia suala la dawa za kulevya, hili ni kero. Tunazungumzia suala la dawa za kulevya lakini kuna bangi inalimwa ndani ya nchi hii na katika sehemu nyingi kuna bangi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna tatizo la gongo, nafikiri wengi wanafahamu gongo ni nini? Ukimkuta mnywa gongo amelewa utafikiri ana ugonjwa wa UKIMWI. Vijana wanavuta bangi wanakosa maadili, wanatukana, utakutana na kijana anakwambia oya mama, lugha chafu tu ambazo hazina maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nafikiri Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ikishirikiana na Polisi wanaweza kuangalia ni jinsi gani wanaweza wakatumia dawa ambazo zinaweza zikaua yale magugu ya bangi. Tuanze na hii bangi iliyopo hapa Tanzania kwanza. Ushauri wangu wakiweza kufanya hivyo kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa zinaweza zikatekeleza suala hili.

Vile vile ningependa kuzungumzia suala la walemavu. Katika suala la walemavu kwa kuwa kila mwanadamu ana haki ya kupata habari. Sijui ni kwa jinsi gani Wizara husika inaweza ikawasaidia wale wasiosikia na wasioona katika vyombo vyetu vya habari, magazeti, televisheni na kadhalika. *At least* kwa kuanzia na televisheni au yule mtu anayetoa *signs* kuweza kuwajulisha wale wasiosikia waweze kupata habari za Tanzania *at least* waelewe ni nini kinachoendelea katika nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza napenda kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi kwa kuteua jina langu ili nigombee katika uchaguzi uliopita nafasi ya Ubunge Viti Maalum Mkoa wa Kusini Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, napenda sana kuwashukuru wanawake wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa Kusini Pemba, kwa kunichagua kwa kura zote za ndiyo kuwa Mbunge wao hapa Bungeni na ninawaahidi kwamba nitawafanyia mema kama kawaida yangu na sitowaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutoa pongezi kwa Serikali yetu hii ya Awamu ya Nne inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi zake nzuri na ninampongeza sana kwa kupata ushindi wa kishindo na vile juzi tulivyomchagua pale Chimwaga kwa kumpa kura zote za ndiyo kuwa Mwenyekiti wetu mpya wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, napenda kumshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Awamu ya Tatu, kwa sababu huwezi kushukuru Awamu iliyopo peke yake, wote kwa ushirikiano. Napenda kumshukuru Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa uongozi wake wote alivyotuongoza sisi Watanzania kufikia hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wake Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa uongozi wake mzuri ambapo anatuongoza sisi Zanzibar bila ya ubaguzi. Napenda kumpongeza kwa kazi zake nzuri na napenda kumpongeza kwa kupata kura za kishindo za ndiyo na ni Rais ambaye anaongoza Zanzibar hata kama wengine wanasema hawamtambui, lakini wanamtambua kwa sababu maendeleo yake wanayatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi yake nzuri anayoifanya Tanzania. Halali mchana na halali usiku Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi. Tunampenda sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi zake na tunakupongeza kwa kweli kwa dhati na Mawaziri wako wote hasa wale Mawaziri wanawake. Zamani tulikuwa nao kila wakati lakini sasa hivi mchana hata usiku hatuwi nao hawa Mawaziri wanawake kila siku ofisini, asubuhi ofisini na usiku ofisini tunawapongeza sana. Kwa hiyo, kufikia hapo naunga mkono hoja mia kwa mia na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kuchangia sasa. Mchango wangu wa kwanza unakwenda kwenye Muungano wetu wa Tanzania. Muungano wetu wa Tanzania ni Muungano imara ambao ulianzishwa. Kwa sababu mimi siwezi kuusema Muungano bila kuwataja waasisi wa Muungano, Marehemu Julius Nyerere na Marehemu Sheikh Abeid

Amani Karume, hawa ndiyo waasisi wetu wa Muungano. Kwa hiyo, nausemea Muungano kwa maendeleo makubwa ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wanaubeza Muungano, ole wao! Nasema ole wao! Sisi Watanzania tusiubeze Muungano kwa sababu ndiyo uliotufikisha hapa leo na maendeleo yote tuliyoyapata ni kwa sababu ya Muungano. Zanzibar kule kusingekalika kama isingekuwa Muungano na tusingenufaika zaidi kama isingekuwa Muungano. Kwa hiyo, nawaambia wale watu wa kule Zanzibar wanaobeza Muungano ole wao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano una faida nyingi. Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete katika hotuba yake ya kufungua Bunge mwaka jana katika ahadi zake alizozitoa katika ukurasa wa 30 alisema kwamba ataimarisha Muungano, kuongeza kasi ya kuzishughulikia kero za Muungano, kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano katika kusukuma maendeleo ya Zanzibar. Lakini mpaka leo kero, kero, kero lazima ziwepo ndogo ndogo na zinashughulikiwa isiwe ndiyo sababu ya kuukataa Muungano. Muungano ndiyo uliotufikisha hapa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema kwa sababu watu wa kule kwetu wengi ndiyo wanaosema Muungano haufai wakati wana majumba makubwa huku Tanzania Bara, wana biashara kubwa huku, sasa Muungano ukivunjika watakwenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa Vyama vya Upinzani hivi ndivyo vinavyokataa sana Muungano. Wakifika hapa wanajidai kusema wanataka Muungano, wanataka Muungano si kweli. Kwa hiyo, tunawambia wautake Muungano kwa sababu ndiyo unaowapa faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya Muungano nyingine ni mgao wa fedha tunazopata, miradi mbalimbali ya *TASAF*, ujenzi wa ofisi mbalimbali ya Bunge, ingawa ofisi yetu ya Bunge Zanzibar haina vifaa na haina wafanyakazi wa kutosha, naomba hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu ulishughulikie, lakini jengo lipo zuri tu. Ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji, ujenzi wa nyumba za majeshi kule katika Jimbo la Wawi na ujenzi wa nyumba za Askari Polisi Wawi na kadhalika.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni ya 50.

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema kwamba Vyama vya Upinzani havitaki Muungano. Kwa mujibu wa Sheria namba 5 ya Kuandikisha Vyama. "Chama chochote ambacho kinaleta ubaguzi au kinakataa Muungano hakiwezi kupata *Registration."* Tunaomba atoe uthibitisho kama Vyama vya Upinzani kweli havitaki Muungano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, imetolewa hoja hapa kwamba Vyama vya Upinzani kama vinakataa Muungano au sivyo. Unaweza kuyaweka sawa sawa maneno yako uliyoyazungumza.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza. Nimesema hivyo kwa sababu Vyama vya Upinzani hasa *CUF* tulivyokuwa tunapitisha hoja ile ya kujadili mambo ya Muungano wao wengi au wote ndiyo walisema kwamba wanataka Serikali tatu. Wanataka Serikali ya Muungano, halafu wanataka Serikali ya Zanzibar pekee yake na ya Tanganyika peke yake. Kwa hiyo, hawautaki Muungano moja kwa moja. Wanataka Serikali tatu, wao ndiyo walisema. Asinipotezee muda. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningeomba tuzungumze lugha ya Kibunge. Umenipa ruhusa ya kuzungumza hapa ndani kwa mujibu wa kifungu cha 50 cha Kanuni. Naomba ulinde, utaratibu atupatie majibu sahihi. Kwa sababu hata ukisema Muungano wa Serikali tatu bado ni Muungano. Nasema atupe majibu sahihi ya ushahidi kwamba sisi hatutaki Muungano. Kwa sababu vyama hivi vinaandikishwa kwa mujibu wa sheria na moja katika sheria namba 5 ya Vyama vya Siasa inasema: "Chama chocote ambacho kinaleta ubaguzi wa aina yoyote au kina mfumo tofauti na ambao umekubaliwa na Serikali Chama hicho hakiwezi kupata uandikishaji." Vyama hivi vimeandikishwa rasmi kwa mujibu wa sheria ya nchi na vinatambuliwa na ndiyo maana hapa tuna viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa sababu vinatambuliwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge atupe ushahidi. Vinginevyo naomba Bunge lako lichukue hatua za kinidhamu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 50 kinasema Mbunge yeyote haruhusiwi kutumia maneno yanayoudhi na Mheshimiwa Mbunge katika kutoa hoja yake amesema tusiseme maneno ya kihuni. Sasa ni nani aliyesema maneno ya kihuni. Atuthibitishie maana ni lugha ya kuudhi. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana Mheshimiwa Juma Akukweti, hakunisikia. Nimesema tutumie lugha ya Kibunge, sikusema neno la kihuni. Mimi najua ninachokisema. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Baada ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kuweka sawa sawa hilo na kulirekebisha lile, nimwombe sasa Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, kwa vile vyama vya upinzani wanasema wao hawapingi Muungano na kwa vile Mheshimiwa Mbunge sio Msemaji wa vyama vya upinzani urekebishe hilo tu ili umalizie hoja yako.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru sana kakiri hapo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed. Kwa sababu kasema kwamba wao hawakatai Muungano, lakini yeye mwenyewe kasema Muungano ni Muungano hata kama ni wa Serikali tatu. Kwa hiyo, mimi nakiri kwamba kumbe wao walikuwa hawataki Muungano wa Serikali mbili. Kwa hiyo, naendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenda moja kwa moja kwenye maendeleo ya wanawake. Kwenye maendeleo ya wanawake hatuwezi kutaja maendeleo ya wanawake kama hatujaitaja Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakiuliza maswali hapa Bungeni kuhusiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Mawaziri wamekuwa wakisema bajeti yao ni finyu. Bajeti yao ni finyu kweli wakati Wizara hii ni Wizara mama, tuiongezee fedha. Kama Wizara hii haina fedha za kutosha kwenye mwaka huu wa fedha basi katika mwaka wa fedha unaokuja iongezewe fedha kwa sababu inaendeleza jamii nzima hasa wanawake, watoto na wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Tanzania ni wanawake imara, wanawake wa Tanzania wanafanya kazi kwa bidii kwa kuleta maendeleo ya jamii, lakini wanawake wa Tanzania wako nyuma kimaendeleo, tujiulize kwa nini? Tukijiuliza kwa nini tutapata jibu kwamba wanawake wa Tanzania yaani wengi wao elimu yao ni ya chini na vile vile mikopo hawapatiwi na wakipatiwa mikopo hawapewi elimu ya kuendeleza mikopo hiyo. Kwa hiyo, naomba Serikali inapowapa mikopo wanawake wa Tanzania wakiwemo wa Mkoa wa Kusini Pemba wapatiwe elimu jinsi ya kufanya biashara zao.

Vile vile, wapewe elimu ya kutafuta masoko hapo ndipo wanawake wa Tanzania wataimarika siyo kuwapa mikopo tu, tukawaachia. Naiomba Serikali iangalie riba za mabenki na Taasisi zipunguzwe. Wanawake hawawezi kumudu riba hizo ni kubwa. Kwani Serikali yetu ni Serikali yetu wenyewe na hayo mabenki yaliyopo ni mabenki yetu wenyewe na hizo Taasisi na hata kama ni ya nje. Kama mtu anataka kuleta Taasisi yake ya nje hapa Tanzania ajue kama wananchi wa Tanzania hawana uwezo wa kulipa riba kubwa na natetea sana riba za mabenki zipunguzwe katika mikopo ili wananchi wetu waweze kuendelea. Jana Msemaji mmoja wa Kambi ya Upinzani alisema bila ya wanawake CCM isingeshinda, lakini eti hatuwatetei wanawake. Mimi si mnaniona hapa nawatetea wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, si kweli kwamba Chama cha Mapinduzi hakiwajali wanawake, Chama cha Mapinduzi kinawajali wanawake na Serikali hii. Kwa hiyo, naiomba Serikali hii iendelee kuwajali wanawake kama kawaida yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Ulinzi na Usalama wa Raia. Napenda sana kumpongeza kwanza Waziri, Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, mtoto wa Mjini na vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Mohamed Aboud Mohamed na watendaji wao wote wa Wizara hii. Wizara hii ni Wizara ngumu sana, lakini wameiweza au siyo wenzangu? Wameiweza kwa sababu ujambazi uliokuwepo katika miaka iliyopita jamani umepungua, si kweli kwamba ujambazi unaendelea sana.

Kwanza yale makundi yote ya ujambazi yameshapatikana. Kwa sababu sasa *IGP* Said Mwema ametoa mpango wa kutoa namba za simu zao, jamani ile imesaidia sana. Zamani Wizara hii *IGP* na Maofisa wake walikuwa wanaongopwa na wananchi. Lakini sasa hivi mtu yeyote hata kama raia, hata kama mtoto akiona jambo fulani baya basi anampigia simu *IGP,* anampigia simu *RCO,* anapiga simu kwa *RPC,* ni kitu muhimu sana na huu ni mpango mzuri sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faida Bakar ni kengele ya pili. Tunakushukuru sana .

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Muda wangu umepotea pale tulivyokuwa tunazungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, muda wako umeishafidiwa tayari. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ambayo iliwasilishwa mbele yetu na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambazo amezifanya hadi sasa hivi, kadhalika Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, naye ametoa mchango mkubwa sana katika kipindi hiki kifupi cha uongozi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda niseme kwa dhati kabisa na ukweli kwamba nawapongeza kwa kauli zao hasa wanaposisitiza kwamba nchi hii ni yetu sote. Hakika maneno ya viongozi wetu hawa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu yana umuhimu wa kipekee. Ni vyema basi takayaenzi, tukaangalia kwamba hilo ni angalizo ambalo limetolewa na viongozi wetu nasi tunapaswa kufuata haya ambayo viongozi wamesema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, nitapenda nizungumze suala la Bunge. Najua Bunge ni chombo ambacho kina hadhi, Bunge linaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu na ninajilazimisha sana nisije nikafika mahali nikawekewa *point of order*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi wote ambao tuko humu ndani tumeletwa hapa na wananchi. Lakini inapofikia mahali tukatengeneza kanuni, taratibu ambazo zinamzuia mwananchi asilihoji Bunge hatuwatendei haki wananchi wetu. Nadhani yapo maeneo kama hayo ambayo tunapaswa tukae kama Waheshimiwa Wabunge tuyatazame na tuweze kufanya marekebisho. Nilikuwa nashauri kwamba tungeweza kufanya mjadala pengine ukawa umefungwa kwa Waheshimiwa Wabunge tu wakalizungumzia Bunge lao,

wakatazama kanuni na taratibu mbalimbali ambazo kama zinaweza kurekebishwa basi zirekebishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wiki iliyopita Mheshimiwa Spika, alimtoa nje Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kwa mujibu wa kanuni na wala hakukosea na wala sisemi kwamba Spika alikosea katika kufanya maamuzi yale. Tatizo pale lilikuwa ni *gloves*. Sasa mimi nikajiuliza hivi *gloves* ni vazi la kiafrika, hivi *gloves* ni vazi la mwanamke wa Kitanzania. Sasa tuziangalie hizi kanuni. Kanuni nyingine tumerithi kutoka kwa wakoloni, zimepitwa na wakati. *Gloves* siyo vazi la mwanamke wa Kitanzania, ndiyo nilikuwa nashauri kwamba tungetazama ni kwa namna gani tunaweza kutazama haya masuala ambayo yanaligusa Bunge na pia tuwasikilize wananchi, wananchi wanaposema kwamba Bunge limekuwa ni mhuri wa Serikali basi tujiulize sisi Waheshimiwa Wabunge ni kweli tumekuwa mhuri wa Serikali na vitu kama hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa busara yenu mtaangalia ni kwa namna gani tunaweza tukalizungumza hili suala ambalo linahusu Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nitapenda sasa nijielekeze katika suala la mipango, mipango ni kuchagua, mimi binafsi sina matatizo yoyote kuhusiana na vipaumbele ambavyo vimechaguliwa na Serikali ya Awamu ya Nne katika kukabiliana na matatizo tuliyonayo kwa wakati huu, sina matatizo kabisa. Nakubali, nawapongeza sana suala ni usimamizi na utekelezaji wa hayo ambayo tumeyaamua kwamba ndiyo vipaumbele vyetu tutayatekeleza namna gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo linanisumbua sana mimi ni wataalam. Wataalam wetu wana uzalendo wa kiasi gani, wataalam wetu watatusaidia kwa kiasi gani kutuondoa hapa tulipo. Tuna mipango mizuri, lakini kwa sababu haikuandaliwa ipasavyo kila wakati tunakwenda tuna gota. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema kuhusu wataalam kwa mfano, juzi hapa Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi alipokuwa anawasilisha kauli ya Mawaziri hapa Bungeni alizungumzia suala la ongezeko la watoto katika shule za sekondari, akasema kwamba idadi ya watoto ambao wamejiunga na shule za sekondari mwaka huu wa 2006 yalikuwa ni malengo ya mwaka 2009. Kama wataalam hawawezi kutupa takwimu sahihi ndipo pale nchi itakapoanza kuingia katika *operations* za zimamoto. Haiwezekani nchi yenye wataalam wazuri na wazalendo wakashindwa kujua ongezeko la wanafunzi na kuishauri Serikali kufanya maandalizi mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ongezeko la wanafunzi ni dhahiri lilikuwa linajitokeza mwaka hadi mwaka hasa tangu pale tulipoanzisha mpango wa *Universal Primary Education (UPE)* kwenye miaka ya katikati ya 1970 na leo ni kipindi cha miaka 30. Mpango ule wa elimu kwa wote watoto walijiandikisha kwenda shuleni, lakini kasi ya kuongeza madarasa haikuwepo, wataalam wetu hawakutushauri. Matokeo yake tumeanzisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari bila maandalizi,wataalam wanatuacha tunakwenda tunavyotaka.

Watusaidie watalaam kwa kuweza kutupa malengo sahihi ili Serikali iweze kujipanga na kufanya vitu katika mpangilio unaoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu katika nukta hiyo hiyo tumejikuta kwamba tuna matatizo ya madarasa pamoja na jitihada kubwa na juhudi iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Tatu katika kuongeza madarasa nawapongeza. Lakini bado tuna tatizo la walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni kweli kwamba pamoja na matatizo yetu tuliyonayo katika eneo la Afya hatuna Madaktari wa kutosha, hatuna wauguzi, hatuna watalaam wa fani mbalimbali katika eneo la Afya. Leo Serikali iamue kwamba watoto wote waliofaulu kwa *division one* katika masomo ya *Biology* basi tunawapeleka hospitali, haiwezekani na wala Serikali haitafanya hivyo. Serikali inajua ikifanya hivyo matokeo yake ni kwamba watu watakufa. Lakini kwa makusudi kabisa tunawaua watoto wetu kwa sababu madhara ya elimu hayaonekani wazi kama ya mtu mgonjwa. Tunaamua kufanya *crash programme* ya mwezi mmoja na baadaye kumpeleka mwalimu kwenda kusomesha watoto ni matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wanaotufikisha hapo ni wataalam. Wataalam wetu wabadilike, watusaidie ili tuweze kupanga mipango yetu iwe ni mipango ambayo ina tija na inayoweza kuiondoa Tanzania hapa ilipo. Hilo lilikuwa ni eneo moja kuhusu wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wataalam wanasema nini sasa hivi? Nchi yetu imeingia katika tatizo la njaa. Tumepata ukame, mvua hazitabiriki, mito yetu inaendelea kukauka pamoja na kwamba kilimo cha umwagiliaji maji ndiyo tunachofikiria kwamba kinaweza kikatukomboa, lakini hatuna uhakika wa hizo mvua, mito inaendelea kukauka tutafanya nini na tufanye nini. Wataalam wetu wanasema nini?

Mheshimwia Mwenyekiti, inashangaza kabisa Tanzania kuagiza ngano Saudia. Saudia ni jangwa lakini wanazalisha ngano. Tunasoma taarifa mbalimbali zinaeleza maji katika sura ya dunia yanapungua. Tuna mpango gani wa kufanya utafiti wa kujua rasilimali ya maji iliyopo chini ya ardhi na yatatusaidiaje kwa kuweze kuzalisha chakula. Wataalam wajielekeze katika eneo hilo la kutumia maji yaliyopo chini ya ardhi. Tuanze kufanya mipango sasa ili tuweze kutafuta njia za kuweza kujitosheleza kuzalisha chakula ili tuondakane na aibu ya kwenda kuomba chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pengine tunaweza kusema kwamba haya wameweza kufanya kwa sababu wanazo rasilimali, wanazo fedha na wanayo mitaji. Ni kweli huwezi kulinganisha Tanzania maskini na Saudia au Kuwait huwezi. Lakini kwa nini wao wamefika hapo ni kwa sababu ya matumizi mazuri ya rasilimali zao. Nchi hizo hazina rasilimali nyingine zaidi ya mafuta. Lakini hawajayaacha mafuta yao yakachimbwa na yakamilikiwa na wazungu mia kwa mia. Serikali ina ubia katika rasilimali ya mafuta. Nchi yetu imeziachia rasilimali zetu zote zinamilikiwa na wageni jamani tujisahihishe. Ipo haja ya kubadilika sasa tuangalie na kwamba Serikali iwe mbia katika kusimamia rasilimali zetu tulizonazo ili ziweze kutusaidia kukuza uchumi wa

Taifa letu ili tuweze kujitegemea zaidi. Mrahaba wa asilimia 3 hautoshi kutuondoa hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa kwa sababu kengele ya kwanza imeishagonga, nijielekeze katika maamuzi. Je, tunapotoa maamuzi tunayasimamia maamuzi hayo? Je, tuna majibu sahihi juu ya maamuzi tunayoyatoa? Nataka hapa nizungumzie suala la mazingira. Kwa kweli suala la kuhifadhi mazingira ni suala la kufa na kupona na ni suala letu sote. Kila mmoja kwa nafasi yake ahakikishe kwamba tunafanya jitihada za kuhifadhi mazingira yetu kwa ajili ya urithi wa vizazi vinavyokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapofanya maamuzi kwa mfano ya kuzuia matumizi ya kuni na mkaa, tuna majibu gani ya kuwaambia wananchi kwamba nishati mbadala ni hii. Ni lazima tuwaeleza wananchi kwamba kama hamtatumia mkaa basi tumieni gesi na gesi wataipata namna gani na itamfikia kila mtu. Ni lazima tuwe na majibu katika maamuzi yetu tusiwababaishe wananchi wanapotujia kutuuliza tunashindwa kuwapa majibu ya kutosheleza.

Aidha, katika hilo hilo ni lazima yatatolewa maelekezo sahihi ya utekelezaji wa hayo maamuzi. Vinginevyo ni vurugu huko katika ngazi za chini. Watu wamenyang'wanywa mbao zao wana leseni wamelipa kodi toka mwezi wa pili zile mbao haziwezi kurudi leo kuwa miti, zimeshakatwa, zimezuiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijatoa tamko lolote kuhusu tabia hiyo, wananchi wanatupigia kelele. Serikali iseme, itoe maamuzi kama inachukua zile mbao wananchi kwamba mbao zao zimechukuliwa na Serikali kwa sababu ya makosa moja, mbili au tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walikuwa wamefanya sawa sawa basi wapewe mbao zao wauze waendelee na biashara yao na tuangalie taratibu ya namna ya kuweza kufanya uvunaji sahihi wa raslimali zetu hasa za misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba tunapofanya maamuzi basi ni lazima pia tutoe maelekezo kwa Watendaji wetu huko chini. Sasa hivi watu kuingia kwenda kukata matawi ya miti kukokotoa. Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kuungana na wenzangu kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi za asilimia 99.9 kuwa Mwenyekiti wetu wa chama.

Pili, napenda nimpongeze Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri, imeeleweka vizuri na ina mambo ambayo hata mimi katika udodosi wangu nilishayaweka naona tumeoana vizuri sana. Tatu, kabla sijatoa mchango wangu napenda niwatoe hofu wananchi wa Wilaya ya Kilombero kwa kauli ya Mbunge wa Mufindi Kusini jana kwamba kutokana na uchafuzi wa Kiwanda cha *SPM* kwamba maji ya kwetu kule

kwenye mito yetu inapewa sumu. Niliongea na Waziri wa Mazingira kumbe ameshalishughulikia suala hili kwa hiyo, wasiwe na hofu, wanywe maji bila ya wasi wasi.

Mimi mchango wangu utahusu hasa kwenye masuala ambayo yanahimiza kilimo kwa vile kilimo inachangia asilimia 45.6 katika Pato la Taifa. Naomba niliongelee hilo kwa kirefu kidogo. Mheshimiwa Rais wakati anatoa shukrani kwa watu wa Mkoa Morogoro alitamka kwamba angependa Mkoa wetu uwe katika mikoa inayotoa ziada ya chakula katika nchi hii. Mkoa wa Morogoro una sifa zote, sina haja ya kujipendekeza au kufanya nini, ni hali ambayo iko dhahiri. Tunataka kama alivyoongea Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi kwamba ziko *Agro Ecological Zones,* sasa mojawapo ni hiyo ya kwetu kwamba inafaa kwa kilimo cha kila kitu. Sasa sisi tuwazalishieni chakula, mle tuondokane na adha hii ya kuwa na njaa kila mahali ni aibu. Ndugu yangu Mheshimiwa Jacob Shibiliti wa Misungwi, Mwanza yeye afuge sisi tuzalishe chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kilimo naomba niongelee kitu kimoja katika kusaidia wazo alilotoa Waziri Mkuu. Labda turudi kwenye historia. Baada ya *October Revolution* kule Urusi akina Karl Max walikaa wakaangalia wakulima wao *(peasants)* sitaki kusema maneno aliyoyasema Karl Max kuhusu *peasants* yalikuwa sio mazuri. Lakini aliwatafsiri kwa lugha ambayo mimi sitaki kuirudia hapa, lakini nasema kwamba alibaini wakulima wadogo wadogo ambao ni *peasants,* hao ni watu wanaopenda kukaa peke yao *which is true,* ni watu hawapendi mabadiliko*, which is true* ni watu wanaiogopa Serikali, *which is true*, lakini wakati huo huo wanafikiria kwamba siku moja watakuwa matajiri.

Baada ya kukaa hapo wakasema sasa tufanyeje katika jumuiya ya watu kama hao. Wakasema tuwaweke katika vijiji na sisi tumefanya hivyo, wamewakusanya wakawaweka katika vijiji. Wenzetu walifanya *rural electrification,* wakaweka umeme kila kijiji kama mwanzo wao wa Mapinduzi ya kiuchumi.

Sisi tumefanya hatua zote hizo ni kweli kabla ya vijiji vya ujamaa wananchi walikuwa wanaogopa Serikali. Siku hizi watu hawaogopi Serikali. Lakini sisi tumefanya kama walivyofanya Warusi, lakini sasa tumeachana pale wenzetu wakasema tuweke umeme kila kijiji sasa sisi tukaenda mkondo mwingine. Wale wakafikia kusema kwamba *communism is electricity.* Lakini sisi tukasema hatuna uwezo wa ku-*electrify* kila kijiji tukaja kwenye hatua nyingine ya kufanya siasa ni kilimo. Sasa kilimo vipi? Sasa nataka kuongelea hapa tumekosea wapi? Sisi tumekosea mahali. Waziri Mkuu ameeleza vizuri na ameongea kwenye hotuba yake tumeipata lakini sasa tufanyeje kwenye kilimo lazima tufanye mageuzi ya kilimo. Nitatoa mfano mzuri sana.

Mimi natoka kwenye Wilaya ambayo kilimo ndiyo uti wa mgongo Kilombero. Miaka 45 tangu tupate uhuru sisi tuna *broadcast* mpunga. Je hamna Afisa ugani anayejua hiyo? *We are broadcasting* mpunga. Hamna mtu aliyefanya *PhD* ya mpunga kweli aka-*compare broadcasting* na ukulima wa kisasa kwa msitari na kupanda mbegu au miche akamwambia Professa wake kwamba *yield* ya kupanda kwa miche unatoa hekta moja unapata gunia 40 kama alivyosema Kilasi, Mradi wa Mbarali *which is true*. Mnapata

gunia 40 au 50 hekta moja na *broadcasting* unapata gunia 10. Wamekaa miaka 45 tangu mwaka 1961 hawasemi chochote utamlaumu mkulima?

Kwa hiyo, kilimo ni ugani hamna kitu kingine. Maafisa ugani tusiwaambie waende kijijini tu, hapana. Tuwaambie waende kijijini na hadidu za rejea. *You are going to Kilombero, you are going to Ulanga* hakikisha kwamba wale watu hawa ku-*broadcast* mpunga ndiyo kazi yako wewe kwa miaka hii tuliyokupa ya kufanya kazi *then* tunaweza kufanya mageuzi. Bila ugani, bila kilimo, ni ugani tu.

Mimi kama Mbunge nimehangaika sana baada ya kufikiria hivi kweli sisi tumekaa hapa miaka watu hawa wana *broadcast.* Hawa wakulima wetu. Karl Max alifanyaje, alisema kwa sababu wale watu wanaogopa Serikali wakasema *at the end of the day* tufanyeje. Wakaamua kwa ujumla kwamba hao watu wanahitaji kuelekezwa. Kila jambo waelekezwe. Kila jambo waelekezwe kwa sababu wakulima *they don't know*. Tuwaambie sasa tayarisha mashamba, sasa tayarisha kitalu cha mpunga, sasa pandeni, sasa weka dawa, sasa palilia, *something like that.* Afisa ugani ndiyo kazi yake bila ugani hakuna kilimo. *(Makofi)*

Mimi kwa kuhangaika kwangu nimekutana na maafisa ugani, *the roving extension officers*, unajua wanatoka wapi? Ndugu zangu wa Same nawashukuru sana, wanatoka Ndungu sikujui wala sijafika. Nimekutana nao wale akinamama *Ruvu NAFCO* wakaniambia mbona wewe tunakufahamu, wewe si Ligallama, Mbunge wa Kilombero tulikuwa kule tunapanda mpunga kwenye shamba la *KOTACO* wakati wa Kampeni. Hao ni akinamama wa Ndungu wamejua utaalamu wa kilimo wanakwenda kwetu wakimaliza wanakwenda *NAFCO Ruvu* kueleza watu jinsi ya kulima mpunga.

Sasa mimi naomba msaada wako Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara inayohusika, akinamama wale nimewaalika angalau niwapate 38 tu nina Kata 19 nipate wawili kila Kata ili msimu huu tufanye mageuzi haya ya kilimo, *yield* ya kulima kisasa ni nzuri. Ndiyo tutabadili kilimo *otherwise* itakuwa ni ripoti tu kilimo kinaendelea na kadhalika, haisaidii. Ugani ndiyo jibu la mageuzi ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima wa miwa. Sisi tunalima miwa. Wiki iliyopita walikuja wakulima wetu hapa viongozi wa vyama vya wakulima wa miwa wao wanalalamikia kodi. Tunatoza wakulima wadogo wale wako 14,000 nchi hii ndio wanaotuzalishia sukari tani 250,000. Wale wanatozwa *income tax*, wanatozwa *withholding tax at the same time* tunasema zao la miwa ni *VAT* e*xempted*. Sasa tunaambiwa *at what stage in time* katika kilimo cha miwa *VAT* inakuwa *exempted* kwa sababu anapolima anatumia trekta, mafuta yamelipiwa *VAT*. Dawa akinunua *VAT*, mbolea *VAT,* sasa tena imeanza miaka miwili iliyopita mtu wa *TRA* akaja pale akaanza kuwatoza akikata muwa wake tu *VAT*, akipakia kwenye gari *VAT*. Sasa msimu huu wanasema akisomba kwenda kiwandani *VAT*. Jamani *do we want to encourage them or to discourage them?* Wanachoomba hawa kodi hii iondolewe, kama ni *VAT exempted* wewe unaposema *VAT exempted* ni wapi. Kwenye kulima huko wamelipa kodi za petroli, kodi za madawa, kodi za mbolea anapokata muwa wake kodi, anapopakia kodi, anaposomba kodi sasa wewe *VAT* umem-*exempt* wapi. Hilo lingine la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, mimi natoka kwenye tarafa ya Mngeta katika Wilaya ya Kilombero pale tuna shamba la *Korea Tanzania Corporation (KOTACO).* Baadaye mwaka 1999 kwa sababu ya muda nitaeleza haraka haraka lile shamba likapewa mwekezaji anaitwa Eric Williams baadaye akaingia ubia na *Bulima Investments Corporation*. Lile shamba, nilishaongea hapa kwamba lile shamba tunaomba lirudishwe kwetu kwa sababu watu wameongezeka. Lakini shamba hilo liko chini ya *RUBADA.* Mheshimiwa Estherina Kilasi alichoongea linafanana na la kwangu bahati mbaya Mheshimiwa Estherina Kilasi yeye la kwake limeshauzwa kule Mbarali, wanangojea watu kupewa.

Mimi shamba halijauzwa, lakini linataka kuuzwa katika mtindo wa *out right purchase* kwa mzungu jamani. Muingereza anunue ardhi yetu sisi tumekosa nini bwana. *Why* katika *stage* hii tunauza ardhi, kwa nini tusimkodishe kama tunataka maendeleo? Yeye aje na teknolojia ya kiwanda, yeye anataka kufanya *bio-diesel*. *Bio-diesel* tupande michikichi tutengeneze dizeli. Lakini sasa wewe ununue ardhi halafu mambo haya yanafanyika kichinichini Mbunge sijui, Wilaya haijui wananchi wa Kata ya Mchombe hawajui. Hapana! Nasema hii hatukubali. Iangaliwe *RUBADA* kama anataka a-*review* mikataba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalofuata ni kuhusu barabara. Hivi kweli barabara zote zinazojengwa nchini kwa lami, zinafuata bidhaa? Isiwe kwamba tunajenga barabara kwa ajili ya kusomba watu, tutakuwa tunafanya makosa sana. Barabara hufuata bidhaa, wote tumejifunza kwenye uchumi. Kwa hiyo, unajenga barabara kwa ajili ya kubeba watu. Sisi kule tunazalisha chakula kwa wingi tunalisha Morogoro na Dar es Salaam. Barabara kutoka Kidatu mpaka Ifakara imepewa fedha kidogo tu. Nimeangalia ni kwa ajili ya *maintenance* tu. Mimi nina barabara ya kilometa 300 tu katika Wilaya lakini katika hizo kilometa 25 tu ndiyo zenye lami kutoka Kihansi pale kwenye umeme mpaka Mlimba mjini na kilometa 10 za *Otter seal* kutoka Kiberege mpaka kati kati pale. Tujenge barabara kufuatana na mazao jamani, tubebe uchumi sio watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niongee kwa kifupi sana ni umeme. Nilisema wakati nachangia hotuba ya Rais kwamba sisi na walinzi wa umeme. Zile *pylons* kutoka Kihansi zimepita kwenye vijiji ambavyo watu wake chini hawana umeme. *Pylons* zimepita kwao, kwa huruma tu sasa hawa watu kwa vile umeme umepita kwao, tuwape umeme. Ni tarafa moja tu haina umeme ambayo na mimi Mheshimiwa Mbunge ndiyo tarafa yangu. Ukitoka Mlimba, Kihansi kuja Ifakara katikati pale katika tarafa ya Mngeta ndiko ninapotoka mimi, hamna umeme. Ninachosema Waziri alinijibu kwamba kupoza umeme kutoka *pylons* zile ni gharama kubwa, mimi sitaki kukubali hilo. Nasema kwamba kuna njia iliyojengwa kwenda Mlimba kutoka Kihansi ya umeme ndiyo hiyo hiyo ijengwe kutoka Kihansi kuja Udagaji, Chita, Chita JKT, Mngeta, Mkangawalo, Njage mpaka Mbingu. Ndiyo hiyo hiyo ijengwe, wataalamu wananiambia inawezekana sio lazima kupoza umeme kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri, alivyonijibu katika jibu la barua.

Pili, sisi tuna *infrastructure* imejengwa pale Mngeta, *dam* imejengwa jamani, *dam* kubwa imejengwa mwaka 1993, *dam* ya kuweza kuzalisha umeme *megawatt* moja ambayo inatosha vijiji vyetu vyote kupata umeme lakini inakaa pale *idle*. Ina *drive only turbines* mbili tukiongeza *turbines* 3 kwa gharama ya bilioni 1.5 tayari umeme utaenda vijiji vyote. Uki-*electrify,* Warusi wale wanasema *communism is electricity* wana maana kwamba ukishapata umeme utakuwa umechochea viwanda vidogo vidogo na hawa vijana hawatakwenda mjini. Watajiajiri pale pale kwenye viwanda vidogo *(Cottage industries)* zitaanza na hapatakuwa na haja ya kwenda mjini. Watachomelea, watafanya shughuli nyingine zenye kuhitaji umeme..

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Kwanza kabisa nampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na jinsi alivyoiandaa, nafikiri ndani ya hotuba hii ya Waziri Mkuu kama haki na uadilifu utatumika, naamini kabisa neema itapatikana na kila Mtanzania atakuwa na maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu ameongoza sana katika hotuba yake hii. *(Makofi)*

Pili, napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, pia kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa katika Bunge hili.

Pia napenda kuwapongeza viongozi wote wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa kuniteua kuwa Mbunge wa Viti Maalum na leo hii niko mbele yako hapa Mheshimiwa Mwenyekiti nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu. Napenda kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napenda kuanzia sehemu ambayo Waziri Mkuu katika hotuba yake amehusiana na mikopo ya wanawake na vijana. Nia ya Waziri Mkuu ni nzuri na nia ya Serikali ni nzuri. Lakini basi huko tunakopeleka mikopo hii je, itawafikia walengwa? Naiomba Serikali iongeze mkakati zaidi kujua kwamba walengwa hawa watapata mikopo hii kama inavyotakiwa. Kwanza kabisa naiomba Serikali kabla ya kupeleka mikopo hii kwa vijana na wanawake wawatengee maeneo ya kufanyia shughuli hizo, isije ikawa vijana wanapewa mikopo hiyo na bado wanakaa wanakimbizwa na wanakuwa wakimbizi ndani ya nchi yao kwa biashara na mikopo waliyopewa na Serikali na baadaye hatimaye washindwe kurejesha mikopo hiyo. Nina mfano hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikopo hii nikiwalenga vijana wa Jiji la Mwanza na wanawake wa Jiji la Mwanza. Jiji la Mwanza wanasema kwamba wametenga maeneo ya kufanyia biashara vijana. Ni kweli yapo, umetengwa mlango mmoja ambao sasa umejaa na uimara na una ulinzi mzuri na biashara zinakwenda vizuri katika eneo hilo la mlango mmoja. Pia wametenga *Buzuruga Stand. Buzuruga Stand* vijana wanafanya biashara zao na wanawake wanafanya biashara zao, wameandaliwa

eneo zuri na kuna ulinzi, lakini katika majibu ya swali langu nililojibiwa na Naibu Waziri wa Usalama wa Raia akasema kwamba wale watu wanazagaa na kwamba wametengewa maeneo ya Sabasaba.

Napenda kumweleza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba eneo la Sabasaba lililotengwa kwa biashara ya vijana na akinamama eneo hilo kwanza halina choo, eneo hilo halina sehemu ya kuhifadhia mali za wale vijana wanapomaliza jioni kufanya shughuli zao. Kwenda kwenye eneo hilo na kurudi kama wewe na mzigo kwenda ni shilingi 2,000 na kurudi ni shilingi 2,000 ni shilingi 4,000 umekwenda na hukuuza kitu je, utarudije na utakula nini? Unaishi nyumba ya kupanga. Kwa hiyo, mikopo hii pamoja na kwamba imeandaliwa lakini waboreshe maeneo ya vijana na akinamama kufanyia shughuli hizi ili waweze kurejesha mikopo na watu wengine wakopeshwe pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye eneo hilo nakuja kwenye eneo la utawala wa kisheria. Inatokea wakati chaguzi zinapita za Serikali za Mitaa, chaguzi zinapita zingine lakini inapofika sehemu kwamba eneo fulani labda Chama cha Upinzani limepata lile eneo kama Serikali ya Mtaa inafikia sehemu Mtendaji wa Kijiji anakwenda kutengua matokeo hayo. Je, Mtendaji wa Kijiji hana haki kisheria? Tunaiomba Serikali sasa imulike hili kwa sababu wananchi ndio wenye maamuzi ya mwisho. Kama wananchi wameamua kumchagua Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa awe Mbunge wao nani anamtengua?

Tunaiomba Serikali nina mfano hai wa kijiji cha Kabangaja. Kabangaja amepita mgombea Uenyekiti wa Mtaa wa Chama cha Upinzani, lakini akatangazwa na Mtendaji huyo kwamba ni fulani ndiyo Mwenyekiti wa Mtaa huu. Lakini baada ya wiki moja Mtendaji huyo huyo amekwenda kutengua matokeo hayo. Kama kuna malalamiko yanatakiwa yafuate sheria, uchaguzi ukatenguliwa Mahakamani. Lakini Mtendaji huyo baada ya Serikali kumchukulia hatua wakamhamisha Kata hiyo na kumpeleka Kata nyingine, hapa tunajenga au tunabomoa? Wananchi wanaotoka katika kijiji hicho watakuwa na imani ipi. Tusiishie hapo eneo la Kabangaja hapo hapo mradi mwananchi ametoka Kigoma yupo pale ndani ya miaka sita anaambiwa yeye ni Mkimbizi mradi ni Muha tu hatakiwi kukanyaga Mwanza anaitwa yeye ni Mkimbizi. Lakini nashangaa Wachaga wameenea nchi nzima hakuna, Mchaga sehemu anaambiwa Mkimbizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, huyu mtu yuko na miaka 6 kama ni Mkimbizi Wizara ya Mambo ya Ndani inafanya kazi gani? Hii yote ni ushabiki wa kisiasa maadam wananchi wakishaamua kwamba tunamtaka fulani eneo lile lisitengwe na yule yule Mwenyekiti hata kama ni Chama cha Upinzani akubaliwe kwa sababu ndio chaguo la wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitarudi sehemu moja ya uvuvi. Nafikiri Mkoa wa Mwanza ni maarufu sana kwa uvuvi, lakini wavuvi hawa wanatumia uvuvi walioachiwa na marehemu babu zao. Hawana uvuvi wa kisasa pamoja na kusema mikopo mingi inapelekwa kwa wavuvi, hawana elimu ya kutosha na wala wengine hawajui kabisa kwamba kuna mikopo ya uvuvi. Pia tunaiomba Serikali kupitia katika Wizara ya Maliasili na Utalii ijaribu basi kuwaambia wavuvi waje wakae nao pamoja,

wawaeleweshe ili wawape semina ya uvuvi wa kisasa na wao wavuvi wana yao wajadiliane na Serikali wakae pamoja, nafikiri hapo tutakavyofanya hivyo maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nasema kwa masikitiko sana eti katika Wilaya tatu maskini sana na Geita imo, ni ajabu. Geita Mungu ameijalia kwa kila kitu. Geita ina madini, ina pamba ya kutosha, ina uvuvi pia ina wafugaji. Mimi naomba MKUKUTA, MKURABITA na MKUMBITA usiishie kwa mkulima tu na mwananchi anayeishi mjini. Huu MKUKUTA, MKURATIBA na MKUMBITA ufike pia kwa mfugaji. Nafikiri Wilaya ya Geita kama hata wafugaji wa Wilaya ya Geita au wa Mkoa wa Mwanza watajaliwa kwa sababu hapa tunasema kwamba wafugaji wapunguze mifugo tunakunywa maziwa ya kutoka Indonesia, Afrika ya Kusini lakini tunasema wafugaji wa Tanzania wapunguze mifugo kwa nini tusiseme wafugaji wa Tanzania sasa tunawawekea viwanda ili maziwa yetu wayasindike na yaweze kunywewa Tanzania nzima na tuwape kipaumbele. Huyo ni mfugaji. Kwa hiyo, Tanzania mfugaji hana maana. Ukimuelimisha mfugaji akaweza kuuza maziwa yake hata ng’ombe hutomwambia awapunguze, atatafuta mashine atasindika na nyama mwenyewe na tayari atakuwa amewapatia vijana wetu ajira kwa kusindika maziwa yale na nyama. Tayari maisha bora kwa kila Mtanzania yatapatikana. Tusitegemee maisha bora kwa kila Mtanzania au ajira ziko Serikalini tu *TRA*, *TANESCO* hapana. Ajira tuanzie nazo huko vijijini tunakotoka, tuanzie nazo huko Mikoani tunakotoka kwa kuwaenzi hawa watu wenye mali na wanaweza wakawasaidia vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita ambayo ni maskini inashika katika Wilaya tatu ina matunda ya kutosha. Geita ina mananasi mpaka yanaozea shambani maana yake hata ukiyavuna ukayapeleka sokoni pia yataoza. Serikali ina mpango gani katika matunda haya tunakunywa *juice* kutoka nchi za nje. Mkoa wa Mwanza tuna maembe, tunakunywa *juice* ya embe kutoka Afrika ya Kusini. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu auangalie Mkoa wa Mwanza. Mkoa wa Mwanza unaweza kumbadilisha Mtanzania na hasa maskini kama watu wa Geita.

Napenda kuchangia eneo la afya. Tunaelewa wazi katika eneo la afya watoto na wazee tayari wamepata upendeleo wa kupata matibabu bure. Lakini baadhi ya hospitali au zahanati watoto hao wakishafikishwa wanaumwa, unaambiwa kuchangia na bado utakapobishana na mhudumu kwamba huyu mtoto anatakiwa kutibiwa bure mhudumu hakuelewi yaani wale Manesi hawakuelewi wanakwambia uchangie. Sasa je, wanakwambia au ukitaka upitie kwa Bwana Msamaha au upitie kliniki kwanza. Sasa mtoto huyu ameugua saa 7 usiku nafikiri kliniki wanafunga saa 9 mchana. Kwa hiyo, huyu mtoto tumwaache mpaka kesho asubuhi aende kliniki ndiyo apewe msamaha aje hospitali. Ni kwa nini basi Serikali isiweke sababu za makusudi kwamba anajulikana tayari huyu ni mtoto na anaumwa atibiwe na akishatibiwa huo msamaha mtautafuta kesho au kesho kutwa lakini maadamu hata akitibiwa usipoweka rekodi ya msamaha ni mtoto umri wake umeonekana. Mfano kama hospitali ya Sekou Toure, Mwanza sisemi kwa kubahatisha hili nafikiri Naibu Waziri wa Afya alikuja Mwanza na niliongozana naye mpaka Sekou Toure, alioyaona ni siri yake yeye mwenyewe. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya pia na wao wajaribu kuwa na huruma hata kwa watoto

hawa kwa sababu mtoto wa mwenzio ni mtoto wako. Madaktari wote wanaofanya hospitali ya Sekou Toure wana mama zao na baba zao waliowazaa lakini wanatutibu hata sisi. Kwa hiyo, si watoto wetu lakini ni watoto wa wanawake wenzetu. Kwa hiyo, naiomba Serikali iliangalie hili pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waziri Mkuu pia kuongelea mikopo ya akinamama, ningeomba basi akinamama hii mikopo isiwe nenda rudi, nenda rudi. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anaongea kila siku linalowezekana leo lisingoje kesho na kesho, kesho hataki. Utakuta ni wasumbufu hawa watu wanaotoka kwenye Kata wanakwambia mikopo inatolewa yaani vyama vinasajiliwa mara mbili kwa wiki. Mtu anatoka eneo la maili 3 au 4 wanakuja kusajili chama chao lakini anaambiwa chama kinasajiliwa mara 2 kwa wiki ni Jumatatu na Ijumaa na ukichelewa ukinikuta nimekwenda Jiji basi. Sasa ningeomba utaratibu ubadilike na huyu Msajili anayesajili vikundi awepo kila siku kwenye Kata ili aweze kujua ni vikundi vingapi vinakuja na vikundi vingapi vinasajiliwa. *(Makofi)*

Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Katiba na Sheria, pongezi yangu kwa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu ni kwa kuwa juzi tu amemaliza kutuambia kwamba ataleta Muswada wa Sheria Bungeni wa kutaka watoto walelewe na wazazi wote wawili ili akina baba nao waweze kubanwa na kufanya kazi ya kulea hawa watoto. Kwa sababu sasa hivi akinamama ndio wamekuwa na mzigo mkubwa wa kulea watoto. Kwa mama mwenye uwezo anaweza akamlea mtoto na kumsomesha lakini kwa mama asiye na uwezo mtoto yule anabakia kuwa chokoraa na wanakuwa watoto wa mitaani wameongezeka. Kwa hiyo, labda ningemwomba hii sheria Mheshimiwa Waziri ailete mapema zaidi ili ianze kufanya kazi mapema na ongezeko hili lipungue na lisiishie kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa, watoto wengi wa mitaani pia wanatoka ndani ya ndoa. Ni pale baba anapompenda yule binti anamchukua miaka mitatu amemzalisha watoto wawili, halafu anamwambia ondoka. Yule binti anayeambiwa ondoka ni binti wa miaka 17 au 18 akiwa ni mkubwa sana miaka 20 hana kazi haelewi vipi atajikimu mbaya zaidi anaambiwa aondoke na wale watoto. Yule binti anakwenda kwao, kwao hawajiwezi kwa lolote matokeo yake ni nini. Huyu baba anabakia mjini kula starehe yeye anatafuta binti mwingine tena amuharibie maisha kama alivyomwaribia yule.

Kwa hiyo, kwa hili ningemwomba Mheshimiwa Waziri, huo Muswada aulete mapema tuujadili na uweze kufanya kazi jinsi inavyotakiwa. Kwa sababu, sasa hivi akina mama ndiyo tumekuwa tunabeba mzigo mkubwa. Akina mama wanaamka asubuhi kabla watu wote hawajaamka, mama huyohuyo analala usiku watu wote wamekwishalala, baba hajulikani aliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuongelea jambo moja. Jambo hili ni pale ambapo mtu anapoamua kutoa mawazo yake binafsi ambapo hata Katiba ya Jamhuri ya Muungano inamruhusu kutoa mawazo ilimradi asivunje Sheria. Lakini mtu mwingine anaweza akambeza, anaweza akamtukana na anaweza akamfanyia kitu chochote anachotaka. Wazo ni wazo, sio lazima likubaliwe. Mtu unaweza ukatoa wazo na lisichukuliwe na nafikiri hata hapa sote tunatoa mawazo na sio kwamba yote

yatachukuliwa. Kwa hiyo, litakalofanyiwa kazi ni lile ambalo limeonekana linastahili kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda kukushukuru kwa kupata nafasi hii. Asante. (*Makofi*)

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana kukushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Kabla sijasema lolote, napenda nichukue nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura za kishindo na kuwa Mwenyekiti wa Chama Tawala. Vilevile, nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa muda mfupi. Kila Mtanzania anakiri kwamba Mheshimiwa Rais ametufanyia mambo makubwa na kwa kweli tunastahili kumpongeza.

Napenda nimpongeze Mheshimiwa Yusuf Makamba kwa kuteuliwa kuwa Mbunge na Mheshimiwa Rais na vilevile kuteuliwa kuwa Katibu wa Chama chetu Tawala. Napenda niwapongeze Wabunge wenzetu ambao wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali katika Sekretarieti ya Chama Tawala. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Napenda kuwapongeza Wakuu wetu wote wa Mikoa, akiwemo Mkuu wangu wa Mkoa Mheshimiwa Isidori Shirima kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais. Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa mna kazi ngumu na naamini kwamba mtatufanyia kazi nzuri. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nilipochaguliwa hapa kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika nilikuwa sijaongea. Kwa heshima na taadhima napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Waziri Mkuu kwa kunipa kura za kishindo. Kwa kweli mimi katika maisha yangu sikutegemea kuwa Mbunge wa Afrika. Lakini mlinishauri, nikachukua fomu na kwa kweli mkanipa heshima. Nasema asanteni sana ndugu zangu na kazi mliyonituma huko nitaifanya kwa ukamilifu na kwa kuzingatia maslahi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Serengeti, napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imeamua kuendeleza Jimbo la Serengeti kwa Kasi mpya, Ari mpya na Nguvu mpya. Nimeamua kufanya hivyo na vigezo vipo. Leo Serengeti umeme unawaka, kazi ya Serikali yetu! Barabara ya lami ambayo hatukutegemea, leo inashughulikiwa na Mheshimiwa Mramba amesema hapa kwamba anatarajia kuja tuchinje ng'ombe. Namwambia aje tutakula *kichule*, karibu sana. *(Kicheko/Makofi)*

Kuhusu bwawa la Manchila ambalo lilinzishwa mwaka 1982, leo hii tumeshaambiwa Shilingi bilioni mbili na nusu zipo, Mheshimiwa Wasira alishakuja akatupa ahadi na kazi itakamilika. Tunashukuru. Lakini vilevile Mheshimiwa Rais alipokuja Musoma, alituahidi kwamba ile Hospitali ya Wilaya aliyosema itajengwa katika Wilaya yetu ya Serengeti, itajengwa na ahadi ipo, kwa hiyo napenda sana kumpongeza kwa ahadi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa sikumtetendea wema Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mama Meghji kama sitampongeza kwa hotuba nzuri aliyotoa. Bahati mbaya sikuweza kuchangia kwenye hotuba yake, lakini kwa heshima na taadhima nampongeza sana na nawapongeza sana Manaibu Waziri wake na Makatibu Wakuu. Bajeti hii ni nzuri, kila mtu amesema ni Bajeti ya kutuletea maendeleo. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuchangia hotuba hii. Kwanza kabisa naomba nichuke nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa hapa. Kwa kweli kila mtu anaamini ni hotuba ambayo itatuletea maendeleo. Kwa hiyo, namshukuru sana yeye na Mawaziri wa Nchi wote, Manaibu Mawaziri na Makatibu Wakuu ambao hutayarisha hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Lowassa sisi tunakufahamu, wewe katika *history* unajulikana kama mchapa kazi na mtu wa kuweza kutoa maamuzi hapo hapo na ukakuta ni mazuri.

Kwa hiyo, tunakuombea Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mwenyezi Mungu akupe afya njema, busara na hekima utuongozee hili Taifa, msaada wako tunauhitaji katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kusema kwamba naunga mkono hotuba hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na kuunga mkono mia kwa mia, nitakuwa sijalitendea haki Taifa hili kama sitaweza kuchangia machache kuhusu hii hotuba. La kwanza kabisa ni kuhusu Serikali yetu iliyoondoa kodi ambazo zilikuwa ni kero. Kwanza, Kodi ya Maendeleo ilikuwa inafanya vijana wanashinda vichakani kuogopa kukamatwa, wazee, akina mama wakifika na maandazi kwenye sehemu zao za biashara wanatozwa kodi ambayo ilikuwa ni ya kero sana. Sasa katika kuondoa ile kero, Serikali ilisema itatoa ruzuku. Lakini kuna Wilaya ambayo ukiangalia ile ruzuku inayokuja hasa zile za wafugaji, maana ilikuwa inategemea kodi ya mifugo, lakini ukiangalia sasa ruzuku inayokuja kutoka Serikalini ni ndogo mno ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti na zile za wafugaji huenda na Wilaya nyingine nazo hazipati ruzuku ya kutosha.

Tunaomba zile ruzuku zitazamwe, zilingane na hali ile ya wakati ule watu wanalipa kodi. Hatutaki kodi zirudi, lakini ile hela ya ruzuku inayotolewa ilingane na hali halisi. Wilaya ya Serengeti inapata kama Shilingi milioni 60 kwa mwaka kama ruzuku, lakini sisi tulikuwa tunakusanya karibuni Shilingi milioni 300. Sasa kodi zile zimefutwa, Halmashauri imedumaa. Naomba hili jambo liangaliwe, tusije tukawa na Halmashauri ambazo zimedhoofika kabisa. Baada ya kuondolewa zile kodi, Halmashauri zimedhoofika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee jambo lingine ambalo ni Halmashauri kupewa hati chafu. Zikishapewa hati chafu, zinaambiwa sasa hela zinapunguzwa kwenda kule ama haziji kabisa. Hivi unafikiri kweli Wizara zikifanyiwa hivyo Serikali itakwenda? *(Makofi)*

Haya matatizo husababishwa na Watendaji. Sasa, mtendaji wa kazi anapozembea, wewe unamuadhibu mwananchi! Hili jambo tulichukulie *serious.* Hili jambo la hati chafu, ikipatikana, Watendaji wanasambaratishwa na wawajibishwe, sio wananchi! Hili naomba sana Serikali ilitazame na liachwe, ama sivyo tutaua Wilaya nyingine. Kuna Watendaji ambao ni wabovu, wanapelekwa kila mahali wanapatikana na hati chafu na kila mwaka hakuna fedha zinazokwenda huko na wananchi wanaadhibiwa. Kwa kweli tukifanya hivyo hatufiki popote. Kila mwaka tunasema kuna ubadhirifu kwenye Halmashauri zetu, hili jambo litafutwe chanzo chake.

Nchi haiwezi kuendeleza wakati Mkaguzi Mkuu akienda tunasikia pesa zimepotea na wafanyakazi wako palepale wanafanya kazi. Sasa hivi kuna kompyuta, kuna *internet banking,* kuna kila kitu. Mahesabu haya yakaguliwe kwa muda wa miezi sita kusudi waliofanya hayo makosa wachukuliwe hatua, tusiendelee na mambo ya karne ya 19. Kulikuwa hakuna kompyuta, watu wanatumia makaratasi tu na *calculator*, sasa hivi kompyuta zipo, hivi mahesabu yanashindwa kukaguliwa kwa muda wa miezi sita na waliohusika wakawajibishwa? *(Makofi)*

Tuache uzembe na kulifanya hilo watu wengi, utakuta kila mtu anagoma, Watendaji watatia kigingi kwa sababu wanajua watakamatika. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba hilo. Watu waambiwe mahesabu miezi sita yakaguliwe na wanaojulikana wameharibu wachukuliwe hatua.

Lingine ni la Madiwani. Madiwani wanafanyakazi kubwa! Wanatumia muda wao mwingi ili kusaidia wananchi kuleta maendeleo. Lakini mwishoni hawapati posho yoyote, hakuna mshahara, hivi karne ya 21 unapofanya kazi na hulipwi, wewe unategemea kula nini? Baadaye wanaanza kuambiwa wanakula hongo. Jamani tuangalie, hivi huyu *His Highness* Kiimbisa, Meya wa Dar es Salaam, kila wakati utakuta anafanya kazi za Jiji, usipomlipa unataka ale wapi? Tuaomba sana Madiwani wafikiriwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni pensheni. Hivi kweli karne ya 21 tunamlipa mtu Sh.20,000/= eti ni pensheni! Alikuwa Katibu Mkuu unamlipa Sh.20,000/=! Huoni kwamba unapoteza muda! Hawa watu wameadhirika na walikuwa watu waliojenga Taifa. Pensheni iangaliwe upya, Sh.20,000/= haiwezekani huyu mtu ukamlipa hizo hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni viwanja vya Mbezi na Tegeta. Serikali inataka kuvichukua, sasa hivi ndiyo tunaandaa watu wapatiwe fedha za mikopo wajenge, wewe unakwenda kuwanyang’anya. Hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tunaomba sana liangaliwe kwa karibu. Kwa sababu watu watanyang’anywa viwanja, wengine watavichukua kwa wingi halafu wataviuza na hivyo italeta matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni la mazingira. Katika suala la mazingira, ukingalia wanaolaumiwa ni Wizara ya Maliasili na Utalii, misitu imekatwa, misitu inakatwa! Lakini Waziri wa Mazingira hahusiki na upandaji wa miti. Tunataka mtu anayehusika na mambo ya mazingira ahusike na upandaji wa miti. Tunataka mtu

anayehusika na mazingira akabidhiwe misitu, tusilaumu. Sasa wewe kama hukabidhiwi misitu, utakuwaje Waziri wa Mazingira wakati kigezo kikubwa pale ni misitu kutoweka na yeye hana la kusema! Ukame wa mwaka huu umetuonyesha tulivyoathirika.

Sasa bwana, siri moja, ukienda *South Africa*, mimi nilipelekwa na Bunge kutembelea *South Africa,* nilishangaa. Pale kilimo ni umwagiliaji wa maji. Tuweke nguvu kweli kweli maana yake bila chakula, hili Taifa litakuja kuadhirika sana. Angalia Shilingi yetu ilivyoshuka, angalia mfumuko wa bei, kwa kweli Mheshimiwa Rais ameanza kwa hali ngumu sana, tunaamini Mungu atamsaidia. Lakini mambo ya maji yawe kufa na kupona.

Vilevile, wafugaji wamepoteza ng'ombe wengi sana. Tunaomba mambo ya maji, pale wanapofuga tuweke nguvu. Mfugaji akipoteza ng'ombe amekwisha. Tunaomba hilo sana.

Lingine ni Walimu wa Sekondari. Sasa hivi watoto wale wa *division one* na *two*, ndiyo wanakwenda Chuo Kikuu, tunaachiwa *division three,* wakafundishe *Secondary School*. Sasa siri ilipo ni kwamba mtoto akifundishwa vibaya *Form One* mpaka *Four* usitegemee kwamba atafanya vizuri *Form Six* na Chuo Kikuu, hawezi. Kwa sababu zile *principles* za *Physics* na *Chemistry* usipozichukua vizuri ndiyo unazokwenda kutumia kule. Sasa ukienda kuzikuta kule na hukufundishwa huku! Wale Walimu wapewe muda maalum tu wa kufundisha mwaka mmoja waende kusoma. Vilevile, tutumie Walimu waliostaafu. Wapo wengi, vilevile hata Wabunge wapo wasomi, nikipangiwa nitafundisha kila mtu achangie elimu, ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu madarasa, ameongea sana pale Mheshimiwa Mbunge. Wale watoto wa MMEM tulioingiza baada ya mwaka mmoja wanaingia Sekondari, sidhani kama tumefanya matayarisho na Walimu wa kutosha. Ni lazima Bajeti inayokuja, hilo liangaliwe kwa undani. Bila hivyo, wale watoto itafika wakati wa kuingia Sekondari tutaadhirika. *Percent* ya kuingiza *Secondary School* itapungua. Tunatakiwa tufanye *marshal plan* watoto wale wakifika Darasa la Saba waende *Secondary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo nasema kwamba naunga mkono bajeti hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu kwanza kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM na pia niipongeze timu yake yote aliyoichagua kumsaidia katika kazi ya kukiongoza Chama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi iliyoko mbele yake Mheshimiwa Rais ni kubwa na ndiyo maana nafikiri Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wakaona ni wakati muafaka kumkabidhi kofia ya pili ili awe na *mandate* kamili ya kuweza kuyashughulikia matatizo ya nchi yetu. Tunawapongeza sana kwa uamuzi huo wa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ningeomba kuisaidia Serikali kwamba Serikali inafikiria haina *resources* za kutosha na ndiyo maana miradi mingi ya nchi yetu imekwama katika kipindi kirefu kutokutekelezwa. Lakini mimi nafikiri tatizo la msingi ni *management of our resources,* ndiyo tatizo kubwa tulilonalo. Haiwezekani Kampuni kufanya uchunguzi tu, unawapa Dola za Kimarekani milioni 65 waondoke nazo hapa na pengine hata kodi hawalipi. Maana Kampuni iko nje halafu utegemee kwamba Watanzania hawa wataondokana na umasikini? Tatizo la *management of our resources ni serious problem* na nafikiri Serikali inatakiwa ikae chini ilitizame upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *performance* ya Serikali Kuu ni wastani wa asilimia 50 mpaka 56. Kama Serikali Kuu ni asilimia 50 mpaka 56, Serikali za Halmashauri zitakuwa katika hali gani? Hali itakuwa mbaya zaidi. Kwa hiyo, nasema tatizo moja ni hili, hatujapata utaratibu mzuri wa kupima hata ile *performance* yetu ili itusaidie tuone kiwango gani huyu mtu anaweza kufanya. Nitatoa mfano mmoja. Wakati mmoja, niliwaomba Wakuu wa Jeshi la Polisi kumpandisha kijana fulani daraja. Mkuu wa Jeshi akanimbia Afende, yule hawezi tena, pale alipofikia panatosha, mimi nikasema hapana anachapa kazi vizuri apandishwe cheo, basi akapewa cheo. Ilikuwa Morogoro hapo. Baada ya muda nikapita pale Morogoro nilimkuta yule jamaa amelewa chakari. Nikamwambia wewe umepandishwa cheo juzi, halafu umepiga mtindi namna hii! Nikarudi kwa *IGP*, *IGP* akaniambia nilikwambia kwamba yule kijana ndiyo kikomo chake. Yule kijana akaniambia Afande bora nirudishwe pale nilipokuwepo maana kiwango changu ni kile. Sasa nasema inawezekana wakati mwingine tunafanya mambo ambayo hatuna uwezo nayo.

Unapeleka Shilingi 500 kwenye Mkoa: Je, umeupima Mkoa huo uwezo wake wa utekelezaji au *resources* hizo unazipeleka tu kwa sababu unataka kuzipeleka! Kwa hiyo, hiyo ni kasoro moja ya kwanza ambayo tunayo katika maamuzi yetu ambayo hatuyafanyii utafiti vya kutosha tukapima viwango vyetu vya utekelezaji na hatimaye tukapeleka *resources* zetu panapotakiwa. Hii ndiyo kasoro kubwa tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye *procurement*, angalia hali ya *procurement* ilivyo. Unaweza ukaikuta Halmashauri imepewa hati safi, lakini ukifanya *performance auditing*, maana hati safi maana yake ni kwamba mtu ameweka risiti vizuri, *auditor* akija anakuta nyaraka zote zipo. Lakini je ukienda kwenye *value for money* hicho kitu kimefanyika? Hakuna. Lakini hati safi imetoka.

Kwa hiyo, nasema moja ambalo tunatakiwa kulifanya hivi sasa ni kuwawezesha Wabunge, mbali na Serikali peke yake kupeleka vipimo, lakini kuwawezesha Wabunge kufanya *performance auditing* kikamilifu. Tutaangalia mahesabu kwenye makaratasi, lakini Wabunge wakaangalie utekelezaji halisi wa kila mradi ambao umekua *approved* na Serikali. Hiyo itaisaidia sana Serikali kuweza kupima uwezo wa utekelezaji wake. Sasa hili ni eneo moja ambalo nilitaka niliseme kwa ufupi ili niisaidie Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna tatizo moja la uvanjaji wa sheria katika nchi yetu. Sasa pande zote mbili zina matatizo, raia wamefika mahali wanachukua hatua

mikononi mwao, Vyombo vya Ulinzi na Usalama navyo vinachukua sheria mikononi mwao. Mimi nafikiri hii ni *"serious issue"* inatakiwa iwe *addressed* sasa hivi. Nimesema pande zote mbili, raia wanachukua sheria mkononi mwao pale wanapoona Vyombo vya Dola havifanyi kazi sawasawa au hawakuridhika. Lakini Vyomba vya Dola navyo anaweza akakosea mtu mmoja lakini ikatolewa *capital punishment* bila ya mhusika kupelekwa Mahakamani. Sasa nasema, hili nalo ni tatizo, linahitaji kuwa *addressed* katika nchi yetu hivi sasa.

Kwamba hili tatizo linakuwa kila siku, matokeo yake itakuwa ni *chaos*. Kwa hiyo, nafikiri hili nalo tungekaa kitako tukali-*address,* ni namna gani tunaweza tukalipunguza. Tulilizungumza hili sana katika Kikao kile cha muafaka baina ya CCM na *CUF*. Lakini mpaka leo halijapatiwa ufumbuzi wa kina. Mimi nafikiri *it is time* tukae kwa sababu hizi *trends* zinaendelea. Ukienda kwa Sungusungu wanafanya wanavyotaka, ukienda katika Vyombo vingine vinafanya vinavyotaka. Sasa hatuwezi kwenda na jamii ambayo haiheshimu utawala wa Sheria. Mimi nafikiri hili tunahitaji kukaa kitako na kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema hili la Shilingi milioni 500, ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu ame-*propose* katika Bajeti yake. Wabunge walikuwa wanazungumzia sana suala la mifuko ya maendeleo ya Majimbo na tukasema pengine labda tungoje mpaka sheria itakapopitisha na kadhalika.

Lakini pengeni tungeangalia sheria yetu ya Tawala za Mikoa tukafanya marekebisho hizi fedha zinazoanza kupatikana hivi sasa zikaanza kupelekwa kwenye Majimbo ili Wabunge wakaweza kuzisimamia. Tukingoja hizi pesa tukazipeleka nje ya ule utaratibu maalum wa hivi sasa, ambapo mpaka sasa tumeshapeleka hela nyingi, lakini hela zimetumika vibaya, mimi nasema utaratibu wa kutumia pesa vibaya utaendelea. Tuanze kuwashirikisha Wabunge katika hiki kidogo kilichopatikana hivi sasa kwa kuzigawa fedha hizo katika Majimbo ili Wabunge wakaweza kusimamia kuanzia hivi sasa kwa kubadilisha sheria ndogo ya Sheria ya Tawala za Mikoa, tutakuwa tumeanzia mahali pa zuri. *(Makofi)*

Kuna fedha za *TACAIDS* ambazo zinakwenda kwa mawakala, kwanini ziende kwa mawakala? Matatizo ya *AIDS* yako kwenye Majimbo yetu, iendeleze katika mfuko huu wa Majimbo tuliyonayo ili Wabunge wapate nafasi kwa Kamati zitakazoteuliwa kuweza kusimamia. Mimi nafikiri hapo tutakuwa tumefanya kazi nzuri zaidi badala ya kushughulika na Mikoa ambapo kwenye Mikoa kuna *administration* ambayo inaweza isisimamie vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi. Gharama zinazotumika katika uendeshaji wa Mfuko huu ni kubwa sana. Wanazo Ofisi mbili, wana Ofisi ya Dar es Salaam, wana Ofisi na hapa Dodoma. Nilimshauri Mheshimiwa Waziri Mizengo Pinda kwamba ni vizuri sasa wahamie Ofisini kwao Dar es Salaam ili kupunguza gharama. Hiki ni chombo cha kibiashara, maana kinawahudumia wafanyakazi wao. Mimi nafikiri wahamie Dar es Salaam wafanye shughuli zao. Lakini kuwe na Ofisi mbili, Dar es Salaam ni *very expensive*. Unamkuta *Managing Director* anatoka Dar es Salaam asubuhi anakuja Dodoma kufanya Mkutano, gharama ni kubwa sana. Mimi

nafikiri gharama nyingine hazina sababu. Hasa kwenye michango hii ya wanachama ambao wenyewe wanataka baadaye iwasaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nilitaka kuzungumzia suala la Muungano. Rais katika hotuba yake amezungumzia kwamba yapo matatizo na amesema kwamba atachukua hatua ya kuyakabili. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuitisha Kikao cha pamoja na Waziri Kiongozi wakayazungumzie baadhi ya matatizo ya Muungano. *(Makofi)*

Kama nilimwelewa vizuri Mheshimiwa Rais ambaye hotuba yake ninayo hapa, ni kwamba aliona hili jambo linahitaji upana wa kushirikishwa kila jamii ili manung'uniko yaweze kupungua. Mimi nafikiri ni wakati muafaka sasa, mbali na Kikao mlichokaa, Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi muwashirikishe na wadau wengine kwa sababu msipofanya hivyo, bado mtapata tatizo lile la watu kunung'unika kwamba wengine hawakusikilizwa mawazo yao na wengine pengine wana mchango mzuri wa kutoa.

Kwa hiyo, mimi nilifikiri pande zote zinazohusika na jambo hili washirikishwe kikamilifu, tuyazungumze kiupana kama alivyosema Rais bila haya, bila ya uwoga ili tupate ufumbuzi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikukumbushe mwaka 1993, Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likiitwa *G55*. Walikuja na *motion* wakitaka Serikali tatu na Bunge likapitisha azimio hilo. Mheshimiwa Jaji Nyalali na Jaji Kisanga naye wakaleta hoja vilevile kwamba ni vizuri tukawa na Serikali tatu. Mwalimu Nyerere akaenda kwenye Chama cha Mapinduzi akawaambia Wabunge kwamba hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi ya kuwa na Serikali mbili. Akawaambia kama mnataka kubadilisha sera rudini kwanza kwenye Chama, Chama kikishakubali kubadilisha sera ndiyo *then* Bunge linaweza kuchukua hatua. Hayo ndiyo yaliyotokea. Ndiyo maana mimi nasema bado kuna kasoro katika mfumo wetu wa Muungano.

Ni dhambi kwa Chama chochote, nasema ni dhambi kwa mawazo yangu, Chama chochote kuwa na mfumo wa Serikali katika nchi yetu, iwe yule anayesema Serikali moja, yule anayesema Serikali mbili, yule anayesema Serikali tatu. Lazima tupate *mandate* ya wananchi wanataka mfumo gani wa Serikali ili hatimaye kisiweko Chama chochote ambacho katika sera zake kitakuwa kinazungumzia mfumo wa sera kwa sababu tayari utakuwa umeshaamuliwa na wananchi. Lakini leo CCM wakisimama wanasema sera yetu ni Serikali mbili, *CUF* wakisimama wasema sera yetu ni Serikali tatu, Chama kingine ni Serikali moja.

Mimi nasema *this is wrong.* Ni kwa sababu wananchi hawajatoa *mandate* kamili ya kusema kwamba tunataka mfumo wa namna gani. Sasa hili mimi nasema ni muhimu likawa *addressed* na tukalifanyia kazi ili haya maneno ya kitoto yaweze kupungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumzia ni kwamba, tunazo Taasisi nyingi sana zinazotoa mikopo na misaada mbalimbali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 50, katika maelezo yake mazuri sana ambayo ameyatoa, lakini nadhani Mheshimiwa Mbunge amepatwa na jazba kidogo aliposema kuna watu wanasema maneno ya kitoto. Sasa suala hili linajadiliwa sana na wanasiasa, sasa anaposema maneno ya kitoto kitoto inaleta maneno ya kuudhi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba kwa heshima ya wanasisa ambao wanalishughulikia jambo hili ni vizuri ama aondoe maneno haya ama aseme hali ya kitoto, kitoto inasemwa katika mazingira gani na watu gani.

**MWENYEKITI:** Anachosema Mheshimiwa Waziri ni Kanuni ya 50 fungu dogo la (viii) (a). Endelea Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema maneno ya kitoto kitoto, maana yake hata kule kwangu Barazani Wawi wanazungumza zungumza, ndiyo maana nilisema ni yakitoto-toto. Sikuzungumzia hapa Bungeni. Hata huko barabarani huko na kadhalika sikuzungumzia ndani ya Bunge, sikukusudia hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI WA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Kwa hiyo, kama kule Wawi wanasema mitaani kitoto kitoto, basi pengine ni huko Wawi. Sasa mimi nikubaliane naye kwamba kule Wawi wanasema kitoto kitoto, maana kule kwao wanasema kitoto. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED**: Hata Dar es Salaam wanasema kitoto kitoto, ni Mitaani sio *official*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, unaweza ukaendelea na dakika zako zitakuwa zimekwisha.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema hili jambo tulizungumze *seriously* ili sasa tuwe na msimamo wa kitaifa ili wananchi wapate nafasi ya kulizungumza jambo ambalo wana hakika nalo.

Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu nakipongeza kikao chenu mlichokaa lakini kinahijika kupanuliwa ili tutoe maamuzi ya pamoja ili hizi kasoro zinazotokea zisitokee. Nitatoa mfano, baada ya mazungumzo yenu tulimsikia kiongozi wa juu kabisa akisema, yale mazungumzo ni tofauti na yale mliyokubaliana. Sasa unajua vitu hivi tunachukulia *seriously*. Rais ameamua mambo ambayo ni mazito kwamba ninyi mkiwa watu *serious* muamue mambo ya msingi. Sasa yanapokuja yakatafsiriwa vingine, sio heshima katika Taifa letu. Sasa mimi nilifikiri tupate nafasi sote tukae pamoja tuyachambue na tukubaliane na hatimaye tutoe mwelekeo wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningeomba kusema kwamba sisi Kambi ya Upinzani tunarudia ahadi yetu kwa Rais kwamba tutamsaidia, tutashirikiana naye kwa yale yote yanayoleta maslahi kwa Taifa letu. Tunamwomba vilevile Mheshimiwa Rais, ipo *perception towards us* ambayo sio nzuri. Wenzetu kila wakati wanatuangalia kama maadui, sisi ni raia wa nchi hii, tuna haki kama raia mwingine. Tumewaomba ndugu zetu wa CCM mtusaidie kwa hili. Tunaunga mkono hoja hapa sio kwa sababu yetu, ni kwa sababu ya maslahi ya Taifa letu na tunapopinga jambo, tunapinga kwa maslahi ya Taifa letu, hatupingi kwa ushabiki wa kisiasa. Hili naomba kuli-*register* kwenu. Tumeli–*regist* kwa Rais na tunaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu tusaidiane sana katika *level* ya Mkoa, Wilaya na hata Vijiji vyetu. Asante sana. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Lakini pia na wewe nikupongeze kutokana na wadhifa wako ulionao hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Waziri Mkuu kutokana na hotuba yake pamoja na Watendaji wake wote. Kwa kweli hotuba hii imetupa matumaini makubwa sana katika kuendeleza na kufanikisha Taifa letu.

Lakini kabla ya kuanza kuchangia hotuba hii, napenda kusema kwamba katika nchi yetu kuna Vyama Vingi na katika kila Chama wakati kimefanikiwa, basi kina mwelekeo wake wa kuendeleza na kufanikisha namna ya kuendesha nchi. Hivi sasa Chama kilicho madarakani ni Chama Cha Mapinduzi.

Kwa hiyo, Serikali itakuwa inaongozwa na Chama Cha Mapinduzi. Hili ningependa tulielewe kabisa. Hata kama hao wengine wangeweza kufanikiwa, basi wangekuja na taratibu zao za uongozi. Lakini nina imani kabisa taratibu hizi zilizotawala sasa zimekubalika na ndiyo hotuba hii ikaungwa mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekee katika hotuba yetu, lakini kwa leo niliona hakuna hata mmoja aliyesimama akasisitiza kuhusu maradhi yaliyotuingilia ya Ukimwi. Toka asubuhi, nipo. Haya yote tunayoyachangia, kama hatukufanikisha suala hili, itakuwa kazi bure. Mtu anasema, nataka maji, utayanywa vipi wakati mgonjwa? Mtu anataka kilimo, utalima vipi wakati uko kitandani? Hili suala zito sana! Nalichukulia kwa uzito huo.

Nasikitika kwamba wote, kila mmoja anadai nataka maji, nataka kilimo. Hebu hili janga tulione hali halisi lilivyo kwamba hapa tunaambiwa milioni 2.5, inaonyesha hawa ni wale waliojulikana tu. Lakini, mimi nasema hata milioni tano watatimia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, Serikali ina wajibu wa kuzingatia sana. Taaluma tunasema kwamba tunapewa, Serikali inatumia fedha, lakini sijui baada ya kutumia na wale wanaopata matibabu kwamba labda warefushe maisha, Serikali inafuatilia kiasi gani? Hiyo haieleweki. Sasa hili suala ni zito sana na kubwa. Kitabu hiki toka tuseme kilipoletwa hapa, basi naamini wengine mlisharithishwa haya maradhi. Kwa hiyo, ina maana siyo milioni mbili tena. Eti, hatulijui, ndiyo! Hii sio milioni 2.5 tena! Ishaondoka idadi hiyo! Sasa, suala hili vipi Serikali itachukua hatua na hasa kwa vijana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kwamba tunawaelimisha, eeh tunawapa mijadala. Bado haijasaidia kwa sababu kwanza kosa lililopo kuhusu namna ya malezi ya watoto wetu, mimi nilivyolelewa sivyo anavyolelewa mtoto mdogo leo. Mimi nilikuwa nalelewa Kijijini na wazee wote. Ilikuwa kila mzee namwogopa na kila mzee nakuwa mwangalifu wakati ananieleza jambo ambalo halistahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tujiulize, leo ndivyo tulivyo na ndivyo tunavyolea watoto wetu! Leo unafika hadi kumlea mtoto, lakini mtoto yule akienda kushitaki, unaambiwa unapelekwa Mahakamani. Siyo maadili yetu tunakotoka huko nyuma! Kama tutafuata labda mila za kizungu, hatufiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi sio Wazungu. Lakini hatari zaidi, tunasema kwamba labda *condom* itamsaidia. Hivi mimi kama nawaambia ukikanyaga hapa, huingii shimoni. Nifanye nini? Nitakanyaga pale nisiingie shimoni. Lakini malezi mazuri ni kwamba kitu hiki moja kwa moja hakifai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari iliyoko, basi tulishampa mtu dawa, tunasema aongeze maisha. Mimi nasema tunamtia nguvu ya kufanya matendo maovu zaidi. Kabisa! Ndiyo! Kweli atamudu yule! Atamudu kwa muda wote kwamba kitendo kile asifanye! Tujiulize, kweli! Kama atafanya, si amekwisha mwambukiza mwingine! Lazima Serikali tutafute taratibu kamili ambazo zitatufanikisha katika suala hili.

Tuko hatarini Watanzania! Kule tunasema, Mwenyezi Mungu anasema: *"Laa takrabu zinaa."* Mwenyezi Mungu anasema, usiikurubie zinaa. Licha ya kitendo chenyewe, hata kuikurubia, usiisogelee hata kuikurubia! Leo sisi tunafanya nini? Ni suala la kujifikiria. Haya maji tunayopanga hatutayanywa! Kwamba mie nivutie Mto fulani uje, Rufiji nivutie, tia bomba, hutakunywa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninalotaka, Serikali itafute taratibu. Serikali ndiyo chombo kikubwa na watu wote wanakitazama. Lakini itazame muundo mbadala utakaotusaidia. Pasi na hivyo, ni hatari kwa sababu hili janga bado linaendelea, leo tuna milioni 2.5, mbali hao watoto yatima na tunasema leo, hatutawaweza!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wosia huu napenda kuutoa, Serikali ichukulie uzito suala hili. Pasi na hivyo, tutafika mahali pabaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni mtu mzoefu hapa, nisije nikagongewa kengele. La pili, Katika suala hili la Muungano, kwa kweli Serikali yetu inajitahidi sana kufanikisha mambo ya Muungano. Lakini, vile vile mambo haya ya kimsingi yaangaliwe sana. Kama tumekubali kushirikiana, basi pawe na mashirikiano. Tuseme kama hata Sekta ya Elimu ya Juu, unajua katika Tume nyingi kule, ina Watendaji kama Ma-S*ecretary General* wale, Ofisi yote hii, haina Mzanzibari hata mmoja. Sasa, kuna vitu kama hivi hata kwa upande wa Makao Makuu tuseme *UNESCO* iliyoko Paris, tuseme utaona kwamba kuna *Commission* kule, kama mawasiliano, elimu na kadhalika lakini, hakuna Mzanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa vitu kama hivi tunawajibika na upande wa Zanzibar nao pia wawemo. Lakini, hata hivyo, utaona katika harakati zetu hizi shughuli za uchumi, yameletwa maelezo hapa ukurasa wa 23. "Tunakusudia kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya Zanzibar bila ya kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mambo ambayo siyo ya Muungano. Lakini naamini uchumi ni mkubwa zaidi, una wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar, ambao ni mdogo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama una ndugu yako siku zote unampelekea kitoweo nyumbani, hukumpenda. Ndugu yako mfundishe uvuvi, utafanikiwa sana. Hata kama anapenda mambo ya kilimo kwamba unamsaidia, basi mfundishe shughuli za kilimo. Sasa Zanzibar ni Kisiwa kidogo sana, ina maana uchumi wake uko chini. Lakini kwa nini wanakuja wawekezaji hatuwezi kuwaambia kwamba hivi sasa hebu kawekezeni Zanzibar? Kwa nini hatuwachangii hivyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vinne tu vizuri, Pemba viwili, Unguja viwili. Basi tunaweza kufika mahali pazuri na hata hizo ajira wafanyakazi wengine watatoka huku huku Bara watakuja kule. Sasa, hili ni suala muhimu sana na ni suala ambalo linaweza kutusaidia sisi. Lakini sasa kwa kusema kwamba leo tunawapa 4.5 iwe kama mtoto, "chukua mwanangu katumie" chukua na hii katumie." Mzazi akishakufa mtoto atakuwa vipi? Ni hatari!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, lazima wakati wanakuja wawekezaji tutumie fursa hiyo. Tunajua *Government* ina *influence* na tunajua kwamba kuna mambo ambayo yana uzito ambayo lazima yaweko. Tuseme, *Marketing* lazima iwekwe, *Raw Material*, *Labour Supply*, *Land Climate*, kila kitu, vitu hivi lazima viweko. Lakini utaona kwamba kutoka Zanzibar kuja Tanzania Bara siyo mbali na utaona kwamba kuna baadhi ya viwanda hata hizo *raw material* zake zinaagiziwa nje.

Kwa hiyo, ningependa suala hili mlipokee na mlichukulie uzito ili kuweza kusaidia, udugu uwe udugu wa kweli. Tukifanya hivyo, nahisi tutafika mahali pazuri na tunaweza kufanikiwa na Zanzibar yenyewe ikaweza kufanikiwa shughuli zake kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii leo tunaona hali ya Tanzania Bara hata Bajeti hii kama alivyosema Mheshimiwa Hamad Rashid, ameona kwamba mambo yote yamekaa vizuri na kwa kweli Tanzania Bara kipindi kijacho hakuna upinzani. Huo ndio ukweli ulivyo! Hawa wote mimi naamini CCM na Viti vyote vitakaliwa na CCM. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa nina uzoefu mrefu na mtu wa zamani, naunga mkono hoja mia juu ya mia, nisije kugongewa kengele. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niwashukuru sana wananchi wa Temeke kwa kunichagua kwa kura nyingi sana za kishindo. Pili, nimpongeze sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM. Tatu, nichukue nafasi hii kumpongeza mpendwa wetu Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Juma J. Akukweti, Mheshimiwa Mizengo Pinda, Naibu Waziri Dr. Luka Siyame, Mheshimiwa Celine Kombani na Katibu Mkuu, Ndugu yetu Mrisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba kwa kuchaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi pamoja na Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Rostam Aziz na mama yetu mpendwa Mheshimiwa Asha-Rose Migiro na dada yangu Kidawa Hamid Salehe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa hiyo, michango yangu mingi, kwa kweli itakuwa kupongeza, kwa sababu najua nini makusudio ya Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 11 kifungu Na.15 - Kujitosheleza kwa Chakula. Hapa mchango wangu, wenzangu nyuma walisema, lakini na mimi naomba niongeze kusema kuhusu chakula cha njaa cha Shilingi 50/=. Sisi Dar es salaam hatukubahatika kupata chakula hiki na sababu kubwa tunaambiwa tunajitosheleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, matarajio ya Dar es salaam ni kupata chakula kutoka katika Mikoa. Sasa kama Mikoa hiyo ina njaa, Dar es Salaam tutapata chakula wapi? Ombi langu siku za mbele na sisi Dar es Salaam mtuhesabu kwamba na sisi tunahitaji chakula cha njaa. Kwa sababu kama Mikoani kuna njaa, Dar es Salaam hatuna njia ya kupata chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dar es salaam tunaponzeka sana na umaridadi wetu. Watu wa Dar es Salaam hupenda sana kuvaa maridadi, mtu huvaa suruali yake nzuri, shati zuri, akafunga mkanda wake hapa juu ya tumbo, lakini mfukoni hana hata senti

tano. Sasa ukiwaona vile, unajua watu wa Dar es salaam wana uwezo na wana chakula. Ombi langu katika hilo, siku za mbele tusiangalie mavazi na siye tuna njaa pia, mtufikirie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini, nizungumze kidogo katika hili. Mimi naomba kabisa, naiomba Serikali kwa kupitia Wakuu wetu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, tuhimize wananchi wetu walime chakula. Kama kuna mvua chache, basi kiko chakula cha kulimwa, mihogo, mtama, watu walime. Tukiendelea hivi, hatari yake inaweza miaka mitano yote tukapata malalamiko ya njaa. Tuseme ukweli tu, tusiogope kunyimwa kura. Wananchi wetu wengine wanayo desturi, wanalima, wakishavuna chakula chote wanauza wakijua Serikali ipo, tutalalamika, wataleta chakula cha njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wengine ni wafugaji, unao ng'ombe 200, unalalamikaje njaa, si uuze 10 ununue chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie pia katika ukurasa wa 15 kifungu Na. 19. Kaka yangu Mheshimiwa Mwenyekiti Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa alichangia. Mchango wangu ni mdogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa MMES turudishe kwenye utaratibu wa MMEM, wasimamie Wakuu wa Wilaya pamoja na Wakurugenzi wao. Tulifanya hivyo, mimi nimebahatika kuwa Mkuu wa Wilaya, Shule zilijengeka vizuri sana. Lakini mpango wa MMES kuuacha kwa Walimu Wakuu wa Sekondari, kwa kweli ni matatizo makubwa sana. Mimi naamini wale Wabunge wenzangu waliosema mpango huu unakwenda taratibu, nina uhakika utakwenda mbio tu, tusiwe na haraka kwa sababu mpango wenyewe nao ndiyo kwanza unaanza. Nina uhakika utakwenda mbio kama ule Mpango wa Shule za Msingi. Tuwe na subira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchangia ukurasa wa 16 kifungu namba 20, Kuhifadhi mazingira. Hapa nataka kutoa pongezi za dhati kwa Waziri Prof. Mark Mwandosya. Wananchi wangu wa Mtoni Dampo pale, walilalamika siku nyingi kuhusu athari za lile Dampo. Lakini pia nisimsahau na Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Mheshimiwa Mizengo Pinda, maana yake alifika kimya kimya bila mtu yoyote kujua, lakini watu wachache walimwona. Ila Waziri Mwandosya yeye tulikwenda kwa mbwembwe na viongozi wote. Lakini nimshukuru alifika pale akaiona ile hali na akakubaliana na wananchi kuhamisha lile Dampo mwezi Desemba.

Kwa hiyo, wananchi wa Mtoni najua wananisikia na Waziri Mwandosya yupo. Pia, kulikuwa na ahadi tokea mwanzo linaanzishwa lile Dampo kuhakikisha pale barabara zinatengenezwa nzuri na mifereji yake. Nalo tumeahidiwa, litatekelezwa. Kwa hiyo, namshukuru sana Waziri Mwandosya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuchangia ukurasa wa 19 - Usajili wa Vyama vya Siasa. Kwanza, nimpongeze Msajili, lakini nitoe ushauri tu kwamba umefika wakati, tuwe na idadi inayoweza kushindana. Kuna Vyama vimeingia kwenye Uchaguzi, unashindana na Mbunge unamwonea huruma, anapata kura moja, kura

mbili, yake na ya Mkewe. Wengine pale Temeke walipoona maji mapana, kama Vyama viwili, walijitoa, wakaamua kurejea CCM. Basi ifike wakati, sasa tumeshakomaa, tuvitazame Vyama viwe Vyama ambavyo vinaweza kushindana. Mara nyingine hata tukiingia kwenye mashindano, unashindana na watu wewe mwenyewe unasikia raha. Lakini, unashindana na watu, wengine unawaonea huruma kabisa! Inakuwa haipendezi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niipongeze sana Tume ya Uchaguzi. Kwa kweli naipongeza sana Tume ya Uchaguzi. Daftari la Kudumu la Wapiga kura, kwa kweli limeleta ufumbuzi wa kutosha. Pale Dar es Salaam chaguzi zile mbili zilizopita, lazima tuseme ukweli. Mtu ulikuwa na uwezo wa kupiga kura mara tatu, lakini kwenye Daftari la Kudumu haikutokea hiyo. Kura yako hii, moja! Ndiyo maana hata kesi za uchaguzi Mahakamani ni chache, maana unaona kabisa umeshindwa kihalali, utakwenda wapi? Pale nimeshinda kura 105,000 dhidi ya anayenifuatia 47,000, unatarajia utakwenda wapi? Utakwenda kushtaki nini? Kwa hiyo, naipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kazi yake nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpongeze *IGP* Mstaafu, Mzee Omar Mahita, aliweka ulinzi mzuri sana. Pale Dar es Salaam tunapata heka heka watu wakirudi kwenye chaguzi, mara maandamano, mara nyang'anya vitu barabarani, lakini *IGP* alitusaidia, aliweka ulinzi mzuri na tukafanya uchaguzi mzuri wa salama. Tukapata washindi waliostahili wenye haki yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ulinzi na usalama wa raia, pia nimpongeze *IGP*, nimpongeze Mzee wangu Waziri Harith Mwapachu kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ila tu, tunaomba, mimi pia ni Mwenyekiti wa Wabunge wa Dar es Salaam. Pale Dar es Salaam mmetupa ma-*RPC* watatu. Dar es Salaam, Ilala na Kinondoni lakini katikati mkawawekea *barrier*. Wote wanaripoti kwa *IGP*, lakini hawa mmewawekea Mkuu wa Kanda. Basi, tunaomba na hawa wawe na nguvu, wawe wasemaji nao waripoti kwa *IGP*. Hilo ndio ombi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru dada yangu Mheshimiwa Diana Chilolo, kazungumza sana. Lakini naomba nguvu zije Temeke, hali ni mbaya sana kwa vijana wetu walioathirika na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuwapongeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Mimi ninaposikia mtu akiwabeza, nasikitika sana. Wabunge muda mrefu sana tunakaa Bungeni, lakini kazi za Majimboni ni Wakuu wa Wilaya na Wakuu wao wa Mikoa. Mimi nawapongeza sana na kwa kweli wanatakiwa wapate vifaa vya kutosha waweze kufanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Mkoa kwa kweli hali ya Ulinzi na Usalama kwenye Wilaya na kwenye Mkoa ni tatizo. Kwa hiyo, naomba sana tusiwabeze, tuwape nguvu. Ukiona Mbunge anagombana na Mkuu wake wa Wilaya, basi ujue ana tatizo lake binafsi, lakini siyo la kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kuzungumzia vile viwanja vya Dar es Salaam ambavyo vimeandikwa kwenye magazeti kwamba *notice* yake ni ya magazeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uko utaratibu, unapotaka kumnyang'anya mtu kiwanja, huwezi ukaandika kwenye gazeti ukasema ukisoma tu gazeti, kiwanja hicho sio chako. Kuna utaratibu wa Kutoa *notice*, kuna utaratibu wa Kamati ya Waziri, kuna utaratibu wa kupeleka kwa Rais kufuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuzungumzia fidia kuhusu watu wa barabara ya Kilwa. Alizungumza Mbunge mwenzagu Mwinchoum Msomi, lakini bahati mbaya hatukupata jibu. Natarajia sasa tutapata jibu kwa sababu watu wa *Kilwa Road* wametutuma, wanahitaji fidia kama wenzao wengine wanaovunjiwa majumba yao, wanavyopewa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi wa Dar es Salaam wanauliza, Daraja la Kigamboni, tulisikia siku nyingi *NSSF* iko tayari kujenga. Kulikoni? Kuna tatizo gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuzungumzia kila Mkoa kutengewa Shilingi milioni 500 kwa ajili ya vijana na akina mama. Kwa kweli tunasubiriwa na bahati mie niliwaambia tunakwenda Bungeni, tukirudi, tutarudi na jibu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipotamka siku ile, mwili mzima nilikuwa nafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ombi kwamba Dar es Salaam tukipewa Shilingi milioni 500 kwa kulinganishwa na Mikoa mingine, mtakuwa mnatuonea, pamoja na kwamba tunaambiwa Dar es Salaam tuna miradi mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana muda uliobaki ni kidogo sana, hautoshi kwa mchangiaji mwingine na uchangiaji unaendelea jioni ya leo. Atakayekuwa wa kwanza ni Mheshimiwa Zuleikha Haji, atafuata Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Aziza Ali. Hawa ndiyo watakaokuwa wachangiaji wetu wa kwanza jioni ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hivyo, basi sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 leo jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja ya Mheshimiwa Waziri

Mkuu, ambayo ameiwasilisha vizuri. Kwanza nataka nihakikishie nyumba hii ya kwamba naunga hoja mkono kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Kabla ya yote nitoe pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais, ambaye pia ndiye Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi, kwa kazi nzuri iliyofanyika Chimwaga na yeye kupata ushindi mkubwa sana katika uchaguzi wa Uenyekiti. Sisi tumefurahishwa kwa sababu pia baada ya hapo alifanya kazi nzuri ya kuteua timu yake ya kumsaidia kazi ikiongozwa na Katibu Mkuu - Mheshimiwa Yusuf Makamba. *(Makofi)*

Tuna imani kabisa wote walioteuliwa tutawasaidia na tutawapa kila aina ya msaada ili wafanye kazi yao vizuri na sisi ambao tumekuwa katika *system* ya Chama kwa muda mrefu, tuna imani kabisa hiyo ni timu nzuri na hasa tulipompata Katibu Mwenezi mwenyewe Bwana machachari, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, atatusaidia sana kukifufua Chama ili sasa kiende katika misingi tuliyokubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nataka pia nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa, yeye pamoja na wasaidizi wake wote ambao wamemsaidia katika kazi hii. Wamefanya kazi nzuri, sisi tuna imani kabisa huu mwanzo mzuri umetokana na uwezo wa Mheshimiwa Edward Lowassa, kufanya kazi kwa uaminifu kama alivyoahidi yeye mwenyewe kufanya kazi katika hali ya viwango vya juu. Sisi tunamfahamu, hatuna wasiwasi na matamshi anayoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakachoomba Mheshimiwa Edward Lowassa, ni kuangalia sasa safu zinazokusaidia kazi. Tungependa upate safu nzuri. Umeshamaliza Wakuu wa Mikoa, nadhani imebaki Wakuu wa Wilaya. Tungependekeza kabisa kwa *speed* hiyo hiyo ambayo umeanza nayo, tuendelee kutafuta wale ambao tunadhani watatusaidia kwenda katika kasi hii uliyoanza nayo. Nina imani kabisa utawapata, wako wazuri, lakini usitie wasiwasi kama ulivyosema, wale ambao hawawezi kwenda na kasi unayoitaka, basi afadhali wakae pembeni wakuachie ufanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Pia, nataka nitumie nafasi hii labda nikumbushe. Kwa kipindi ambacho nimekuwa nacho, napenda kusema kwa dhati kabisa nimeridhika na kazi ya utendaji ya Mawaziri wetu, wamejitahidi sana. Wamejitahidi pamoja na hali ngumu ya maisha, lakini wamejitahidi kutekeleza kazi zao. Ila ningependa kushauri kwamba ni vizuri Mawaziri sasa wakawa na Waandishi wa Habari, wawe wanasaidia kutoa maelezo ya mambo wanayofanya katika maeneo yao kwa sababu itasaidia angalau wananchi wajue kila wakati Waziri anafanya nini katika eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi hizo, sasa nitumie nafasi hii kupongeza vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama kwa kutuhakikishia ulinzi umekuwepo katika maeneo yetu. Yuko *IGP* - Mwema amefanyakazi nzuri kwa kipindi kifupi tu. Ni vizuri tukatambua kazi nzuri anayoifanya na mimi nina imani kabisa ataendelea kushika uzi huo huo ambao ameanza nao na sisi Wabunge, tutampa kila aina ya msaada ili aweze kufanikisha kazi zake, kwa sababu kuna usemi wa zamani unasema: *"Help the Police to*

*help you."* Lazima sasa utumike sasa. Tusaidie Polisi ili ikusaidie tuitumie kwa nia nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, nataka nitumie nafasi hii nizungumze kama nilivyozungumza katika Kikao cha Mwezi Aprili kwamba niliwashukuru wapigakura wangu wa Sumbawanga Mjini kwa jinsi walivyokuwa wamepiga kura zao. Katika Miji 21 ya Mikoa yote, Mji wa Sumbawanga ndio ulioongoza kwa kura nyingi kwa Mheshimiwa Rais. Hivyo, Mji wa Sumbawanga ndiyo kipenzi kikuu na ndiyo chimbuko la CCM pale. *Politics* za Mijini ni tofauti na Vijijini. Mijini vipo Vyama Vingi vya Siasa, lakini tulivuka asilimia 90 kwa kura za Mheshimiwa Rais. Hii ni dalili tosha ya kwamba yapo mambo ambayo tutamwomba Mheshimiwa Rais atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nije katika mambo ambayo nadhani ni vizuri nikayachangia. Hapa katikati, mwaka 2005 Mheshimiwa Waziri Mkuu atakumbuka niliomba katika hoja ya Bajeti ya kwamba Wizara ya Mifugo na Maji ningeomba zitenganishwe. Mwanzoni wengine hawakunielewa, lakini nashukuru Mheshimiwa Rais, alisikia kilio chetu na akazitenganisha. Mimi nina imani kabisa mwanzo huo utasaidia Wizara ifanye kazi yake vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uwingi Wizara siyo hoja kwangu. Hoja ni nini Wizara itafanya ili kusaidia kupunguza umaskini kwa wananchi? Hata ukiwa na Mawaziri wanne, watano kama hawawezi kusaidia wananchi, ni bure. Lakini nina imani kabisa alipofanya kazi hiyo alikuwa na maana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, karne ya 18 Wafaransa ilibidi waongeze Wizara nyingi sana. Wizara mojawapo waliyoiunda wakati huo ilikuwa ni Wizara ya *Solidarity*. Wizara ya *Solidarity* waliiongeza baada ya kuona mazingira ya wakati huo yalikuwa ni magumu kuoanisha Shughuli za Bunge, Shughuli za Serikali na Serikali za Mitaa ya kwamba lazima waunde Wizara, kufuatana na mazingira yaliyopo wakati huo na ndiyo maana Rais, anapounda Wizara anazingatia mazingira ya wakati huo. Siyo lazima ziendelee zinaweza kuongezeka au zikapungua. Sasa suala la wingi wa Wizara lisiwe ni noma. Tuna imani kabisa atalifanya hilo kwa sababu nzuri tu. *(Makofi)*

Sasa baada ya kusema hayo, mimi mwenyewe napenda kuomba mambo yafuatayo: Nilipokuwa napitia Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Bora, katika ukurasa wa 13 kuna kitu kimoja kimenifurahisha sana. Wajumbe waliozungumza ambao bahati nzuri Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa George Lubeleje, alisema hivi: "Kuwe na programu maalum ya kuendeleza Mikoa yenye maendeleo duni na kwamba katika mwaka wa fedha ujao, fedha za kutosha zitengwe kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara na kuimarisha miundombinu ya Mkoa wa Rukwa." Mwisho wa kunukuu. Aliyazungumza haya kwa makusudi mazima! Kilichonifurahisha, Wajumbe wote katika mtandao wao hakuna hata Mjumbe mmoja anayetoka Mkoa wa Rukwa. Lakini wameona umuhimu wa kuangalia miundombinu katika Mkoa wa Rukwa, ili Rukwa iruke kweli.

Napenda kuwashukuru kwa niaba ya wananchi wote wa Mkoa wa Rukwa kwamba wameona tatizo hili na tuna imani kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mtaliangalia suala hili kwa sababu limeletwa kwa uzito maalum. Hakuna Mkoa mwingine uliozungumzwa humu, ni Mkoa wa Rukwa na Manyara. Sasa hiyo imenifurahisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu waliotembelea Mkoa wa Rukwa, wameona tatizo kubwa la Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa ukiwapa mambo makubwa matatu utashangaa maendeleo yatakayokuja. Kwanza, wape barabara tena ya lami, tena itoke Tunduma – Sumbawanga – Mpanda mpaka Uvinza, ikiingia Uvinza iungane na Kigoma. Wape barabara kutoka Sumbawanga mpaka Kasanga ili iungane na Ziwa Tanganyika kwa ajili ya barabara ya kwenda Burundi - Rwanda na Kongo. Wape barabara ya kutoka Matai mpaka Kasesya mpakani mwa Zambia, mtaona Rukwa itakavyofumuka. Rukwa itafanya maajabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa tuna bahati, Mungu ametujalia katika Mkoa huo hali ya hewa ni nzuri na mvua ni za uhakika. Mwaka 2005 peke yake licha ya kuuza mazao kupeleka Zambia na kila mahali, akiba ya chakula peke yake ilikuwa na tani 32,000 za mahindi ambazo zilikwenda kwa wenzetu Mikoa ya Tabora na Shinyanga. Ni kazi hivyo inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Mkoa wa Rukwa wapeni elimu, wapeni kila upendeleo, wapate elimu ya kutosha. Elimu ndio msingi. Ukimpa mtu elimu, hata haya mambo ya afya yatamalizika yenyewe. Elimu ndiyo msingi wa mambo. Magonjwa mengine kwa kweli yanatokana na ukosefu wa elimu. Tunaweza kupoteza fedha nyingi sana kwa ajili ya suala zima ambalo linahusiana na mambo ya afya, lakini elimu inaweza kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Mkoa wa Rukwa, uwape pembejeo za kilimo. Pembejeo za kilimo ni pamoja na mbolea na zana za kilimo za kisasa. Sisi hata tukipata plau, tukipata pembejeo kwa ruzuku maalum, tukipata maksai, vikundi vya vijana vikasaidiwa, Rukwa hamtapata mtu yeyote anayekuja Mjini hata siku moja.

Vijana wa Mkoa wa Rukwa walio wengi utakuta wanashinda mashambani, hutawakuta hata Dar es Salaam kwa sababu tulichofanya ni mambo mawili. Binadamu ukimpunguzia ile adha ya kusukuma jembe ukamtafutia kautalaam kidogo, ana tabia ya kupenda kazi hiyo. Unapotumia plau ambayo hata vijana wakitoka shuleni wanatumia kwa ajili ya kulima mashamba yao, wanaona ni faraja kubwa sana kuliko wanaotumia jembe la mkono. *(Makofi)*

Ndio maana wazee na vijana wa kule wanapewa maeneo yao ya kulima ili wajione nao wanamiliki uchumi. Usipompa eneo, ataona anamfanyia kazi baba na mama na fedha anazozipata zinakwenda kwa baba labda atanywea pombe na yeye hapati kitu chochote. Unahakikisha na wenyewe unawashirikisha! Ndiyo maana mimi ningependelea na ninapendekeza kwa Serikali, hizi fedha ambazo zinakuja kusaidia vikundi, licha ya

kusaidia vikundi ambavyo vipo, maana yake watu wakishasikia kwamba kuna vikundi vitapewa fedha, vitafumuka vikundi ambavyo hatuwezi kuvi-*manage*.

Sasa lazima tuona namna ya kuweza kuangalia vikundi ambavyo vipo na vikundi ambavyo ni waaminifu, wanafanya kazi yao vizuri kwa kuanzia mwaka wa kwanza. Lakini pia tuangalie vijana ambao wana miradi midogo midogo wakopeshwe maksai, wakopeshwe pembejeo, watafanya maajabu vijana hawa kuliko tukizisambaza tu. *(Makofi)*

Mimi ningependekeza pia hizi fedha wakati wa kugawiwa Waheshimiwa Wabunge, tuhusishwe kwa sababu tusipoangalia fedha hizi zinaweza kuja zikawa ni kitanzi kwetu Wabunge ya kwamba fedha zimekuja watu wamependelewa. Mbunge akifanya lolote, mambo yameharibika. Mwaka 2010 watatunyonga! Watatusubiri tu ya kwamba ulifanya nini? Fedha mlizipitisha ndani ya Bunge, lakini zimetumika vibaya na Mbunge unaona! Sasa ni vizuri tukashirikiana na uongozi tuone namna zitakavyotumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, yako makosa mengine ambayo nadhani ni vizuri tukayaangalia. Katika suala la Utawala Bora pamekuwa na kipindi ambacho kwa kweli mimi siridhiki. Wakurugenzi wetu wamekuwa kila wakati wako safarini, kila wakati wanasafiri kwenda kwenye Semina na kongamano. Kwa nini kusiwe na utaratibu wa kuratibu hizi Semina? Kama Semina ni mambo ya elimu na afya angalau mkaweka hata wiki moja wakamaliza Semina zao wakarudi kufanya kazi za watu. *(Makofi)*

Lakini utakuta kila siku fedha zinatumika kwa ajili ya kusafiri na kila wakati watu wanakaimu. Wanaokaimu ni watu wa aina mbalimbali ndio maana utakuta maendeleo wakati mwingine hayaonekani. Sisi ambao tunakaa katika Mikoa ambayo ni mbali na Makao Makuu, fedha zinazotumika kwa ajili ya kusafiri ni nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutoka Sumbawanga mpaka hapa sio chini ya lita 200, lita 300 na bei ya mafuta Sumbawanga utakuta kwenda na kurudi anamaliza nusu milioni au milioni nzima kwa mafuta tu peke yake. Hivi Halmashauri zetu zitaweza? Akisafiri mara tatu/nne amemaliza kabajeti. Tulidhani ni vizuri tukaliangalie kwa sababu suala hili linaanza kutuletea matatizo. Mara nyingi hata Vijini hawafiki huko. (*Makofi*)

Lingine linahusu posho za Madiwani. Mwaka 2005 pia nilizungumza kwamba Madiwani jamani ni wasaidizi wetu. Hapa tulipo Madiwani wako Vijijini na ndiyo wanaoratibu shughuli zetu kwa niaba yetu. Mara nyingi, mkikaa vizuri na Diwani anaweza kukufanyia kazi vizuri zaidi. Lakini Madiwani kutegemea posho ya Sh.30,000/= kwa mwezi kwa kweli ni utani. Zamani tulikuwa na msemo unaosema hivi: "Uongozi sio kazi ingawa kuna kazi za Uongozi." Mheshimiwa Aggrey Mwanri, uongozi sio kazi, lakini kuna kazi za Uongozi. Nini tafsiri yake? *(Makofi)*

Kuna wale Viongozi ambao wanalipwa mshahara, kuna Viongozi wanaojitolea, lakini kuna kiwango cha kujitolea ambacho unaweza kusema mtu atajitolea. Lakini

itafika mahali fulani atashindwa kujitolea. Tulidhani kwa kweli waanze kufikiriwa ili Madiwani nao waweze kufikiriwa wapate chochote, kaposho kazuri, mliangalie katika Bajeti yao inayokuja ili angalau sasa waanze kufanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Pia, tujitahidi ili waendelee kupata elimu nzuri na wenyewe wafanye kazi zao vizuri hasa katika mazingira tuliyonayo haya ya kujua mahesabu ya kila Halmashauri, wasije wakadanganywa na Wakurugenzi. Madiwani wakijua watamchachafya Mkurugenzi, lakini wasipojua watafumbwa, hawatajua lolote la kufanya. Ni vizuri tukaliona hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungeomba mawasiliano ya kiutalaam ya kila Wizara na Halmashauri kwa kweli yazingatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya pili jioni hii ili na mimi niweze kutoa mchango katika hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, naomba na mimi niungane na wenzangu wote kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura zote. Nimesema zote, kwa sababu ni asilimia 99.99 kuwa Mwenyekiti wa Chama chetu cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Pia, nawapongeza wale wote ambao wamechaguliwa kuiongoza Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi. Uwezo wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete katika nafasi hiyo ambayo tumemchagua juzi juzi kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, unaeleweka, tuna hakika nao. Kwa hiyo, mimi nina hakika na wenzangu wote Wana-CCM wenzangu na Watanzania kwa ujumla tuna hakika kabisa kwamba Chama chetu sasa kitakwenda kwa kasi mpya, nguvu mpya na ari mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu uwezo wa Wabunge wenzetu, uwezo wa Mheshimiwa Yusuf Makamba na wenzake waliochaguliwa katika nafasi hizi mbalimbali kuiongoza Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi na tuna hakika kabisa kwamba Chama chetu, kimepata sura mpya, lakini sura ambazo zitakiwezesha kwenda kwa kasi ambayo tunaitegemea. Wote hawa nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Bahi na Mkoa mzima wa Dodoma, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete na Serikali nzima kwa uamuzi wa kujenga Chuo Kikuu hapa kwetu Dodoma. Nikiwa katika hili vile vile nawashukuru na kuwapongeza wenzetu wa Kanisa la *Anglican* kwa kuamua kuchukua iliyokuwa Shule ya Sekondari ya Mazengo na kuigeuza kuwa Chuo Kikuu ambacho watakiendesha wao wenyewe.

Kwa maamuzi haya yote, sisi tumeyafurahia sana, tumeyapokea kwa furaha sana na tunashukuru sana na nina hakika kabisa kwamba yatachochea kwa namna moja au nyingine maendeleo ya elimu hapa kwetu Dodoma, kwa sababu Waswahili wanasema, ukikaa karibu na waridi, nawe huachi kunukia. Kwa hiyo, naamini kabisa maamuzi haya

yote ni ya manufaa sana kwetu, ndiyo maana sisi tumepokea maamuzi haya kwa furaha sana na tutashiriki kwa namna yoyote ile ambayo tutatakiwa kushiriki ili kuhakikisha kwamba yanafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningelipenda vile vile niishukuru sana Serikali kwa msaada wa chakula iliyotupatia katika msimu huu uliopita kutokana na tatizo kubwa sana tulilokuwa nalo la njaa katika Wilaya ya Dodoma Vijijini na Mkoa mzima wa Dodoma. Chakula hicho kimekuwa cha msaada sana na wananchi wameshukuru sana na kwa hakika ningelipenda kuihakikishia Serikali kwamba kimetusaidia wote kuvuka salama, hakuna aliyekufa kwa njaa.

Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa msaada huo. Lakini na mimi nisisitize kama wenzangu wengine ambavyo wamesisitiza kwamba katika Wilaya ya Dodoma Vijijini, katika Wilaya mpya ya Bahi na katika Mkoa wote wa Dodoma, bado tunalo tatizo la njaa kwa mwaka huu kutokana na ukame usio wa kawaida uliotukumba katika msimu wa mvua uliopita. Nashukuru sana kwamba taarifa za Serikali zinaonyesha kwamba wanalielewa hili vyema. Kwa hiyo, tunaendelea kuiomba Serikali, kama ilivyotusaidia katika msimu uliopita, basi itusaidie vile vile kwa mwaka huu ili tuweze kuvuka salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mkoa wa Dodoma, kama alivyoeleza vizuri sana Mheshimiwa Degera asubuhi, nadhani tatizo letu la kukumbwa na njaa mara kwa mara inawezekana likawa gumu kulitatua kama Serikali haikutusaidia kuingia katika kilimo cha umwagiliaji kwa sababu ya ukame ambao unatuathiri hapa Dodoma. Ni Mkoa wenye rutuba sana kama wote mnavyofahamu. Udongo wa Dodoma una madini ya kila aina ambayo ni mazuri sana kwa mimea mbalimbali. Kwa hiyo, hatutumii mbolea maeneo mengi wala hatujawahi kutumia mbolea za chumvi chumvi na unaweza kulima nafaka ya aina yoyote hapa Dodoma. Mazao karibu yote yanastawi hapa Dodoma. Lakini tatizo letu ni mvua.

Kwa hiyo, tukiendelea kuitegemea mvua kwa hapa Dodoma hatutafanikiwa. Hata tunapowahimiza wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame, wakati mwingine inashindikana. Kwa mfano, msimu uliopita maeneo mengine hatukupata mvua kabisa. Kwa hiyo, kwa kweli kwa Dodoma ufumbuzi wa suala hili ni kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba niungane na Mheshimiwa Degera kuiomba na kuielekeza Serikali kwenye mradi wa Bonde la Mto Bubu. Eneo la Mto Bubu limefanyiwa utafiti kuanzia Serikali ya Wakoloni kuanzia mwaka 1950 na tafiti nyingi tu zimefanyika hapa katikati na imedhihirika kwamba bonde hili likitumika vizuri linaweza likaukomboa Mkoa huu kutokana na njaa zinazotokana na ukame.

Mheshimiwa Naibu Spika, imeonekana kabisa kwamba kama likijengwa bwawa kubwa maeneo ya Farkwa, linaweza likahudumia kilimo cha umwagiliaji kwa kiwango cha hekta 10,000 ambazo zinaweza zikazalisha zaidi ya tani 25,000 za nafaka mbalimbali.

Lakini vile vile watalaam wameonyesha kwamba tunaweza tukatumia bwawa hilo kuzalisha umeme na likatoa kiasi cha MW 20 kikachangia katika *grid* ya Taifa. Sasa taarifa zote zipo, michoro na kadhalika. Nasema tafiti nyingi sana zimekwishafanywa na imeonekana kwamba kunaweza kuwa na manufaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali, ijielekeze kwenye bonde hilo kwa madhumni ya kuunusuru Mkoa huu. Hekta 10,000 kwa kuanzia zinaweza zikatusaidia sana. Naomba sana, taarifa zote zipo, kuna taarifa zimekwishaandikwa kama hii niliyonayo na ziko nyingine nyingi kuhusiana na hili Bonde la Mto Bubu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuziangalie taarifa hizo na tuone namna ambavyo tunaweza kuzitumia ili kuweza kuunusuru Mkoa wa Dodoma. Kwa gharama za ujenzi za mwaka 1984 ilikadiriwa kwamba bilioni tano zilikuwa zinatosha kujenga bwawa hilo. Kwa sasa hivi kwa vyovyote vile bei hizi zitakuwa zimepanda sana, lakini tunavyozidi kuchelewa ndivyo gharama za ujenzi wa bwawa hili zitakavyozidi kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali, kama inawezekana iamue sasa kabla gharama hazijapanda sana ili tuweze kuutekeleza mradi huu. Kwa upande wetu sisi wananchi wa Wilaya ya Bahi na Jimbo la Bahi, tunaishukuru sana Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo imezichukua katika Wilaya yetu kuanzisha miradi midogo midogo ya umwagiliaji ambayo imekuwa ni ya manufaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi tuna mradi mkongwe wa Bahi wa Umwagiliaji wa Kilimo cha Mpunga, lakini hivi karibuni umeanzishwa mwingine jirani na hapo katika Kijiji cha Uwelela, tunao mwingine Chipanga ‘B’, tunao mwingine Chali Makulu, kuna mwingine upo Chikopelo na mwingine mpya, Mtitaa. Tunashukuru sana kwa jitihada hizo za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sababu pekee ambayo imenifanya nilizungumzie suala hili siku ya leo ni kwamba pamoja na jitihada hizo nzuri sana za Serikali ambazo kwa kweli ni kutekeleza yale ambayo tumeahidi wananchi utekelezaji wa miradi hii, umekuwa sio makini hata kidogo. Miradi yote hii wananchi wameitekeleza kwa kushirikiana na *IFAD*. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba, mpaka sasa hii miradi ambayo nimeitaja, hakuna ambao unafanya kazi vizuri kwa sababu utekelezaji wake umekuwa siyo makini.

Nataka sasa nijielekeze kwa hii mipya ambayo imejengwa hivi karibuni tu, mradi wa umwagiliaji wa Uhelela na mradi wa umwagiliaji wa Mtitaa ambao umejengwa kwa msaada mkubwa sana wa *IFAD*.

Ule wa Uhelela, *IFAD* imetoa Shilingi za Kitanzania milioni 305 na ule wa Mtitaa Shilingi milioni 267 fedha za *IFAD*. Lakini utekelezaji wa miradi umekuwa ni mbaya na

Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi siogopi kusema kwamba kuna harufu mbaya. Siyo tu kwamba kulikuwa na usimamizi mbaya, lakini nafikiri kuna uchafu ndani yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakandarasi walioteuliwa kusimamia miradi hii kama ule wa Mtitaa ni Mkandarasi mmoja kutoka Kenya sijui, nasikia ni mtaalam wa ujenzi wa barabara, kateuliwa kujenga bwawa la mradi wa Mtitaa. Mradi huu ulikuwa uanze mwaka 2004/2005, lakini mvua za kwanza kabisa ziliponyesha tuta likabomoka, ikabidi likarabatiwe. Mradi huu mto wake unaanzia kwenye milima hii inayoonekana hapo Image.

Kule mvua hazikunyesha lakini mto ulipeleka maji, imekuwa hadithi hiyo hiyo, mfereji mkuu umebomoka, mlango wa kupeleka maji kwenye mashamba haufungi, kwa hiyo, bwawa liliingiza maji mara mbili likajaa, lakini hayakudumu, watu wamelima na mazao yote yamekauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uhelela vile vile kuna matatizo makubwa, mifereji iko chini, mashamba yako juu, hakuna kinachoendelea ni kashfa tu. Lakini fedha nyingi zimetolewa na wafadhili, wananchi wamejitahidi sana kutekeleza majukumu yao, lakini usimamizi na utalaam katika ujenzi wa miradi hii umekuwa ni mbaya sana. Hata ile ya nyuma nayo vile vile haifanyi kazi vizuri.

Kwa hiyo, nasema, jitihada nzuri sana za Serikali zimekuwa *frustrated* na usimamizi. Nafikiri kuna mambo ambayo mimi ningeliomba yatazamwe. Mheshimiwa Waziri Mkuu nimelileta kwako makusudi kabisa kwamba sisi ilikuwa tunufaike sana na miradi hii na bado tunaitegemea sana, sasa haifanyi kazi na fedha zimekwisha.

Mwaka 2005 watu wamelima mazao yamekauka yote, sijui nani anawalipa! Lakini ile nia nzuri ya Serikali na matumaini ambayo sisi tulikuwa tunajenga juu ya miradi hii yote yameishia katikati.

Kwa hiyo, mimi nafikiri pamoja na kuiomba Serikali iangalie namna ambavyo itatusaidia ili miradi hii ifanye kazi kama ilivyokusudiwa na wananchi waweze kunufaika kama ilivyokusudiwa, lakini basi hebu litazamwe kwa undani hili suala, kuna nini? Kwa nini utaalam katika ujenzi wa miradi hii umekuwa wa hovyo namna hiyo? Kwa nini tuta libomoke mvua ya kwanza tu? Kwa nini mfereji mkuu ubomoke mvua ya kwanza tu, wakati fedha nyingi zimetumika? Nadhani malengo yote yamekuwa *frustrated*.

Nafikiri kuna haja ya kuyatazama haya ili kama kuna maovu yoyote hapo katikati, basi hatua zinazotakiwa zichukuliwe na sisi tusaidie ili miradi hii ifanye kazi kama ilivyokusudiwa ili tuondokane na tatizo hilo. Kwa Mkoa wa Dodoma kama hatukusaidiwa kilimo cha umwagiliaji, kweli tutaendelea kuwa ombaomba wa chakula mara kwa mara na haitusaidii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu anayeishi karibu na mto au ziwa au bahari, ukitaka anufaike na samaki wa ziwa au bahari, umfundishe avue samaki wake mwenyewe kuliko akisikia hamu ya samaki unampelekea. Haisaidii! Dawa ni kumsaidia ili aweze kuvua samaki wake mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nashukuru sana kwa jitihada zote za kuendelea kutusaidia kwenye tatizo la chakula. Kwa hiyo, naomba tusaidiwe ili tuweze kuzalisha chakula chetu wenyewe. Kwa Dodoma hiyo haina wasi wasi kabisa, kwa sababu mwaka wowote ule ambapo mvua zinanyesha vizuri, wengi ni mashahidi, tunazalisha kuliko mahitaji yetu wenyewe na tunauza hata mikoa mingine hasa Dar es Salaam. Wengi huwa mnaona yale magunia ya mahindi pale Kibaigwa. Huo ndiyo uwezo wa Dodoma, hiyo ndiyo Dodoma inachoweza kufanya, tatizo letu ni ukame. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali iendelee na jitihada hizo za kutusaidia kuanzisha miradi mbalimbali ya umwagiliaji, isimamiwe vizuri iweze kufanya kazi. Ninaamini kabisa kwamba, Dodoma inaweza kuzalisha *surplus* ambayo inaweza kusaidia hata maeneo mengine ya nchi yetu.

Yangu yalikuwa hayo na nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri sana na hoja nzuri sana, imethibitisha tu uwezo wake, kama wote tunavyomfahamu na kwa hiyo ameweza kutoa hoja hiyo nzuri sana, kwa kushirikiana na wataalam wake na sina matatizo nayo kabisa, naiunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuongea jioni hii. Awali ya yote, nami naomba nishirikiane na Wabunge wenzangu, kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuweza kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi na kupata kura nyingi sana. Pili, napenda kuwapongeza viongozi wote ambao wamechaguliwa wa kuambatana naye ili kuweza kuamsha Chama chetu cha Mapinduzi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Pia nawapongeza zaidi Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, waliopiga kura juzi kwa jitihada yao na kwa umahiri wao wa kuweza kupiga kura zote za ndiyo, ni kura moja tu ambayo ilipatikana ya hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba kuchukua nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya na jitihada zake ambazo kwa muda mchache tu zimeonekana kuwa na imani na wananchi wengi wana imani naye sana. *(Makofi)*

Nachukua nafasi hii kuwapongeza Wakuu wa Mikoa, wale wote ambao wameteuliwa na wale ambao walikuwepo katika nafasi zao, ili kuweza kuendelea kufanya kazi katika Mikoa yetu na ninahaadi kuwa, Mkoa wetu wa Tabora tutampa ushirikiano mkubwa sana. *(Makofi)*

Pia nachukua nafasi hii kutoa rambirambi kwa wana-CCM wa Mkoa wa Tabora, hususan Wilaya ya Tabora Mjini, kwa kupata msiba wa Mwenyekti wetu wa UWT, Bi. Mwashamba Songoro, Mwenyezi Mungu, ataiweka roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata nafasi hii kuweza kuchangia katika hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote, naomba kwanza nimpongeze sana Waziri Mkuu na Serikali yake, kwa kuweza kwa awamu ya kwanza tu katika hotuba yake, kukamilisha ahadi ya Mheshimiwa Rais. Ahadi hii ya Mheshimiwa Rais alisema kuwa, watawezeshwa wanawake na vijana. Kweli katika hotuba yao mwanzo wameanza kufanya bila ya kufanya kazi na kuonyesha kuwa yale ambayo walikuwa wakiyatolea ahadi yanakamilishwa. Kwa hiyo, hii ni mojawapo ambayo inaonyesha kuwa ahadi zilizotolewa zote zitakamilika.

Lakini napata wasiwasi kidogo kulinganisha ahadi hizi ambazo zitatolewa na zinakamilika. Je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii tunaisaidiaje ili kuweza kutusaidia katika kukamilisha ahadi zetu na wao waweze kufanya kazi ya kusimamia wale akina mama na vijana? *(Makofi)*

Nilikuwa nadhani Wizara ya Maendeleo ya Jamii, tuweze kuishirikisha kwa ukaribu zaidi ili iweze kuwasaidia, lakini bila kuwashirikisha tu pia hata kuweza kuwaamsha. Wizara hii kwa kweli tunaionea sana, kwa kuipa kiwango kidogo sana cha pesa. Ukizingatia katika Mkoa wa Tabora, bajeti ambayo ilikuwa imepita ya 2005, nilizungumzia kuwa sisi pale Tabora hatuna hata Afisa Maendeleo ya Jamii wa Mkoa. Waziri wa wakati ule, Mheshimiwa Asha-Rose Migiro, akasema utaratibu upo na kweli upo unaendelea. Lakini je, Tabora?

Nimeona, bado maeneo mengine. Lakini bado Afisa Maendeleo ya Jamii kwa kweli hawana nafasi ya kufanya kazi na hawajaamka. Kwa wakati huu wa ari mpya na kasi mpya na wao pia waamshwe ili waweze kufanya kazi. Ukienda katika Wizara ya Maendeleo ya Jamii, una matatizo unataka usaidiwe, unaambiwa wako nje wamesafiri wameenda kwenye kongamano, wameenda kwenye semina, sasa hii inaonekana kuwa wao ni kwenda nje tu, kwenda kusoma wao. Sasa hawa wananchi wetu ambao sisi wa Maendeleo ya Jamii tunawategemea, wanafanya kazi gain? Watoke kule Wizarani na kuacha kwenda kwenye kongamano nje, waache kwenda kwa wananchi, ili kuweza kufanya kazi ambayo imewawezesha kuwepo pale. *(Makofi)*

Lakini la pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa sababu alipokuwa Waziri wa Maji, alifanya kazi moja ya kwenda Misri na baadhi ya Wabunge, walienda wakajionea wenzetu wa Misri jinsi wanavyofanya kazi. Misri kule wanaweza wakakaa miaka miwili mvua haijanyesha, lakini bado wanalima, wanapata chakula kingi na maendeleo yanapatikana katika kilimo. Wanapata chakula kingi na maendeleo yanapatikana katika Mkoa wao, katika nchi yao. Lakini sisi kwetu hapa, mvua ikiacha kunyesha awamu moja, tunapiga kelele mara Mtera, mara chakula hakipatikani; kwa nini tusijilinganishe na wenzetu, ili tuweze kubadilika? *(Makofi)*

Wao wanawezaje na sisi tutashindwaje, ili tuweze kubadilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, yale ambayo uliyaona Misri, ulikuwa na nafasi nzuri ya kuwapeleka na nina imani pengine Mwenyezi Mungu, ndiye aliyekuongoza hukuweza kujua kwamba, utakuwa Waziri Mkuu. Sasa yale ambayo uliyaona kule, ndiyo uyahamishie katika nchi yako. *(Makofi)*

Nilikuwa na ushauri mdogo, kwenye kilimo kutokana na mawazo yangu tu. Kuhusu suala la kilimo, ukilinganisha kwanza katika nchi yetu, kuna mfuko ambao unaitwa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. Kila mmoja anaufahamu sasa hivi hata wana kijiji kule na watoto wadogo wanaufahamu, kwa sababu semina zimepelekwa mpaka kwa wananchi wetu wa vijijini. Kwa hiyo basi, Mfuko huu wa *TASAF* tumeshaona maendeleo yake na unavyowasaidia wananchi kwa shida ambazo wanazihitaji wao maeneo yale waliyopo. Kama watahitaji *dispensar*y, watasaidiana na Mfuko huu kwa kushirikiana ili kuleta maendeleo ya *dispensary*. Kama ni daraja mpaka litapatikana. Basi nilikuwa nashauri katika Ofisi ya Waziri Mkuu, lazima kuwe na Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, ambao utasaidia masuala ya kilimo peke yake na Mfuko huo uweze kuletwa katika Bunge hili, tuweze kuupitisha ili kuwa ni Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo, ambao utafanya kazi hasa kule vijijini na pale Wizarani tubaki na wale ambao wanaandaa sera, wanaoandaa MIKUKUTA, sijui na Mikakati, wao wabaki kule kule lakini pesa nyingi ziweze kuingia katika ule Mfuko ili wananchi waweze kufanya kazi ya kilimo na kuona mafanikio yake. *(Makofi)*

Wananchi wale hawahitaji zile takwimu, mnawapelekea kwamba, mmepata tani ngapi. Wao hawahitaji hayo, ninyi mbaki nayo huko Wizarani, wakija viongozi mtakuwa mnawasomea taarifa na MKURABITA na hiyo inayokuwa kila siku inaongezeka. Lakini wale Wenyeviti wetu, tuweze kuwasaidia ili waweze kuwa na kilimo cha kisasa, waweze kupata matrekta wao wenyewe wataamua sisi kilimo chetu tunataka kiwe cha aina gani. Mfano, naweza kusema kule Tabora kuna tumbaku. Tumbaku ile Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza, ninakuomba kilimo kinachokuja wakishavuna tumbaku lile soko la kwanza watakapoanza kwenda kuuza, uwe mgeni rasmi kwenda kufungua uone bei ambayo wanapangiwa pale. *(Makofi)*

Bei wanazopanga wenye makampuni kuliko bei ya kupanga wale wakulima wenyewe, kwa sababu hawana sauti ya kusema. Watasemea wapi wale ndiyo wamewapa mbolea, wale ndiyo wamewapa mbegu, kwa hiyo, hawana sauti. Kwa hiyo, hii yote watasaidiwa ndani ya ule Mfuko wa Maendeleo ya Jamii ya Kilimo, mle ndiyo kutakuwa na wataalam. Bahati nzuri hapa tuna Kituo cha *SUA*, Morogoro. Wataalam wapo, tuwatumie basi, badala ya kukaa tu pale *SUA* wanafanya kazi za *SUA*, lakini tuwachukue ili waje kutusaidia katika masuala ya kilimo ili wananchi wetu wapate elimu ya kilimo cha biashara pia. Kuliko hawa wanalima mahindi kwa mfano, wakishalima mahindi yao wakianza kuuza yale mahindi yakiwa mabichi, tayari yameshaanza kusimamiwa na ngoma zitapigwa, matangazo msiuze mahindi. Sasa nashangaa, yale mahindi ni yake mwenyewe, kalima kwa pesa yake mwenyewe, sasa wewe unapomkataza kwenda kuuza, ina maana umemsaidia kitu gani pale?

Mwacheni auze kwa sababu yeye anauza ili aweze kununua daftari la mtoto wake la shule. Kwa hiyo, kunakuwa hakuna kitu chochote ambacho kitawasaidia. Laiti kama kungekuwa na wataalam ambao watawasaidia, walime mazao ya biashara na walime na mazao ya chakula, hiyo ni njia mojawapo ambayo itaweza kuwasaidia wakulima wetu.

Lakini bado maeneo mengine ambayo yanaweza yakasaidia, katika nchi yetu kuna kilimo cha mpira. Kilosa, kuna nafasi ya kuweza kulima mpira, wachunguzi wamechunguza wameona pale mpira ukilimwa, unaweza kustawi vizuri, Zanzibar pia mpira ukilimwa unaweza kustawi vizuri, bado na Tanga, mpira ukilimwa utastawi vizuri. Sasa kwani kuna tatizo gani na wananchi wetu kuweza kuwatafutia wataalam na wao wakafanya biashara ile kuliko mpira sasa hivi tunaagiza Malaysia ndiyo unakuja huku kwa bei kubwa zaidi, ambayo wananchi wetu tungewawezesha wangeweza kuendelea na wao kupata pesa zile ambazo tunapeleka Malaysia, zingebaki hapa kwetu katika nchi yetu, wakulima wetu wangeondokana na huo utaratibu ambao tunausema kuwa maisha bora kwa kila Mtanzania, kama hana pesa atakuwa bado hana maisha bora.

Nazungumzia kuhusu masuala ya madini. Wizara ya Madini, nadhani hata hiyo asilimia tatu wanayosema, sikubaliani nayo, katika nchi yetu inabaki na asilimia tatu. Kwa sababu kuna kampuni ambayo inafanya kazi katika Wizara ya Madini, ile Kampuni inayofanya kazi katika Wizara ya Madini, ambayo imetoka nje, wao wanakuja kwetu kama watafiti na wanapokuja kwetu kama watafiti, bado wanalipwa wao na Wizara ya Madini. Kibiashara unasema lazima kuwe na mtaji, pili, kuwe na faida. Sasa ile faida ambayo unaipata bado unairudisha kule kwa ile Kampuni ambayo imetoka nje kuja katika nchi yetu, inayofanya utafiti.

Kwa hiyo, hapa tunaweza tukasema labda tunapata asilimia mbili, siyo asilimia tatu tena, hilo bado ni tatizo, ni suala la Sera ya Madini. Sera ya Madini ililetwa katika Bunge lililopita, walivyoleta tukawaambia kwamba, huyo huyo Mwenyekiti wa Bodi ya Madini na bado wewe Mwenyekiti ndiyo anakwenda kuandaa Sera, hicho ndiyo kitu ambacho hakiwezi kukubalika. Bado sera ya kwanza iliandaliwa na ikaonekana kuwa ina mapungufu na kama bado ina mapungufu, yule Mwenyekiti anaendelea kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya kuandaa Sera ya pili. Nadhani hapo bado hatujaweza kujifunza kuwa yule aliyeandaa wa kwanza, lazima abadilike awepo mwingine tena ili waweze kuleta mabadiliko. Hiyo yote inasumbua katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la elimu, napata wasi wasi kwa sababu kuna shule nyingi sana ambazo zimejitokeza. Shule hizo zimekuwa ni nyingi, ambazo zina ada kubwa sana. Sasa ina maana lazima kuna matabaka mawili na ndiyo maana haya matabaka yametokea tukaleta na utaratibu wa kubadilisha hata mitaala ili mradi tu wale ambao wanafanikiwa kule, wenye pesa, waweze kufanikiwa. Kwa hiyo, mitaala yote ikabadilika.

Halafu pili, lazima tuzingatie kuwa wewe huwezi kuwa Waziri wa Elimu, baadaye na wewe ukaenda kufungua shule yako. Kwa maana hiyo, ile Wizara ambayo tayari unaiongoza ina maana kuwa elimu ile inayotolewa katika Serikali, haikamiliki zaidi ila ile elimu ya kwako kule ndiyo inayofaa zaidi. Hili ni mojawapo ambalo katika utawala bora tuliangalie ili wananchi wetu wasiweze kuwa na kigugumizi au kuweza kuwa na mashaka katika elimu yetu.

Bado migogoro katika Vyuo Vikuu. Vijana wengi sasa hivi tunasema wapate elimu. Kama vijana hawawezi elimu kinachonisumbua sana pale ninapoangalia vijana wengi wanagoma na kupata matatizo sana katika vyuo vikuu. Nina imani kama viongozi

wa vyuo vikuu watakuwa hawana matatizo, vijana nao pia watakuwa hawana matatizo. Lakini kama viongozi watawaanzishia vijana matatizo na vijana na wao lazima wawe na matatizo. Kwa sababu hakuna mtu ambaye anaweza kukubali asome, amepewa ahadi ya kuweza kupewa pesa, baadaye anakuja kuambiwa pesa zile ambazo walikubaliana kupewa, anapewa chache. Hata kama ni mimi, sitoweza kukubali. Wengi wametoka mbali, wazazi wao wamewaleta pale ili waweze kupata elimu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Tekinolojia, iweze kuangalia kuna tatizo gani hapa mpaka hawa vijana wanakuwa wanagoma kila wakati.

Wengine wanasema Wizara hii au shule zile ziweze kuongezewa pesa. Pesa wanapata na kama pesa wanapata zinakwenda wapi? Kwa hiyo, lazima vijana wetu mara nyingi wanaonekana kuwa ni chanzo cha matatizo, wanapenda kugoma, vijana wanapenda matatizo, lakini si hivyo, vijana hawapendi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JUMA HAJI SEREWEJI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika. Kabla sijaanza kuchangia kwanza, ningependa kuunga mkono hotuba hii ya Waziri Mkuu, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Mwanakwerekwe, naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo, nimpongeze Mwenyekiti mpya wa Chama cha Mapinduzi, pamoja na uongozi wote aliouteua Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia jambo hili hapa, ambalo sikukusudia kuchangia kwa sababu ni la zamani kidogo. Lakini ilivyokuwa katika Bunge lako Tukufu leo limetajwa, pamoja na juzi, imebidi na sisi tupige debe, kuhusu ndege ya Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hakuna hata Mbunge mmoja hapa ambaye jimboni kwake anakaa kwenye kibanda cha mgongo na kwa wananchi wengi tu wanakaa humo. Kama anatokezea Mheshimiwa Mbunge huyo, anakaa kwenye kibanda cha mgongo, wananchi wake wote watashangaa na kustaajabu kutokana na hadhi na wadhifa wa uongozi wake.

Kwa hivyo na sisi lazima tuwaenzi viongozi wetu wa juu kama Rais kuwa na ndege kama hii na hasa hivi sasa ilivyokuwa Marais wetu wanakwenda nchi nyingi tu, nao wanaalika wageni wengi tu kuja hapa na tunawaona Marais wakifika hapa wanavyoteremka kwenye ndege zao kwa mbwembwe kabisa kabisa na pengine kabla hawajafika, wanaanza kufika makachero pamoja na ndege zao. Sisi Rais wetu lazima aende vile, sasa itakuwa dhambi ikiwa sisi Wabunge tunakaa hapa, halafu tunasifu kwamba, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete anakwenda vizuri, anafanya kazi nzuri, tunamwuunga mkono halafu tunageuza kwamba, asipande ndege kama ile, wakati anafanya kazi nzuri. Tumwandalie mazingira mazuri, ambayo yanakwenda na wakati, akifika popote ajulikane kwamba, huyu ni Rais wa Tanzania na ni nchi ambayo inatambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Marais wakishastaafu tu, basi Mataifa makubwa yanawatambua. Sasa itakuwa dhambi kwamba, tunawanyanyasa, kwa mfano, wapande ndege ndogo ndogo zisizotambulikana! Hilo la kwanza. *(Makofi*)

Lakini nadhani Mheshimiwa Naibu Spika, msafara au Rais kutumia ndege hiyo ni kazi ya utawala na si lazima atumie ndege ile, ana ndege nyingi tu za Serikali. Kwa hiyo, ikiwa anatumia ndege nyingine, siyo inaashiria kwamba ndege ile ni mbovu. Ana wajibu wa kutumia ndege anayoitaka, kama sisi tunavyotumia ndege yoyote tunayoitaka, kama sisi tunavyoweza kutumia kwenye majimbo yetu *Mark II, Korando* au gari yoyote ile tunayoitaka. Wakati mwingine huwa tunatumia baiskeli tu kwa raha zetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hili ningeomba Waheshimiwa Wabunge, kama kweli tunalipenda Taifa letu, kama linavyopendwa huko nje, tuwapende viongozi wetu na tuwaenzi. Halafu kuna msemo mmoja ambao unasema "kata pua uunge wajihi." Kwa hiyo, ni lazima tujibane lakini mambo ya lazima, yanayokwenda na dunia ya leo, yafanyike. Mojawapo ni hilo, nimemaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye hoja nyingine hii ya kuwapa shukrani Tume yetu ya Uchaguzi *(NEC)* ya Taifa na *(ZEC)* ya Zanzibar. Tunatoa shukrani kubwa sana na hasa aliyeweka lile zoezi la Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, ambalo nathubutu kusema lilikuwa jipya. Lakini limekwenda vizuri na hata uchaguzi ulikwenda vizuri sana, kwa upande wa Zanzibar saa tisa tulishamaliza kila kitu, kwa sababu uchaguzi ulikwenda kileo. Kwa hiyo, Msemaji Mkuu kwa Kambi ya Upinzani, yule aliyesema kwamba, kuna wananchi ambao hawakuwahi kupiga kura wasiopungua milioni tano, kama ni kweli, hili lisitupiwe kwa upande wa Tume yetu ya Uchaguzi. Kwa sababu pale mipaka yote ya uhamasishaji ya kuchangia ili wananchi waende, basi Tume ile ilifanya hivyo. Walihamasisha kuanzia vyombo vya habari, pamoja na mabango kuweka, kila wakati na hata michezo waliwahi kufanya, lakini walibainisha Tume ya Uchaguzi, kwa sababu nchi yetu haina Katiba inayosema kwamba, asiyekwenda kupiga kura ana hatia. Kwa hiyo na wao walikuwa hawajui wawabane wapi watu wao. Walikuwa hawakwenda kwa maslahi yao na utashi wao tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nakuja kwenye Muungano. Wabunge wa Tanzania Zanzibar tuna haki tukiwa hapa tuzungumze mambo ya jimboni, tuzungumze mambo ya Wilaya, tuzungumze mambo ya Mkoa, tuzungumze mambo ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hadi Taifa na ndugu zetu Waheshimiwa Wabunge kutoka Tanzania Bara nao vile vile, wana wajibu huo na wanafanya hivyo. Itakuwa dhambi sisi na hasa Wabunge wa CCM, kutozungumza hapa na halafu tukaanza kuzungumza kwenye majukwaa. Kwa hiyo, tunakuombeni ndugu zetu Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania Bara, tukizungumza hayo, mtusaidie ili tuondoe hizi kero ndogo ndogo zilizopo kwa umoja, tusiwape nafasi wale wasiopenda Muungano wakapata kupiga debe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hii awamu ya nne, naamini kero zitaondoka. Sisi binadamu labda hatuna kumbukumbu, mambo mengi tu yameshakamilishwa. Tumedai Bendera ya Zanzibar, natumaini iko, tumedai bendera ya Rais Zanzibar anayo,

tumedai muziki wa Zanzibar tunao, tumedai timu ya Zanzibar ijitegemee itambulike, hali kadhalika tumefaulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakuhakikishia sisi Wazanzibari tunaupenda sana Muungano, tena sana, kwa kila atakayesoma Katiba, basi ataupenda Muungano. Kwa sababu leo nchi zote, jambo la kwanza kabisa, amani na utulivu. Lakini la pili hakuna nchi moja inayotaka kuchezewa kipande chake au sehemu yake ya ardhi na katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano, imesema ni marufuku sehemu yoyote ya ardhi ya Tanzania, kuchezewa na mtu yeyote. Pia ikasema kiongozi yeyote atakayeruhusu kipande cha ardhi chochote cha Tanzania kukiacha ni haini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ushahidi tosha tuliuona, ndiyo tukaingia mpaka Kampala. Wazanzibari wanasema kama wanajeshi wamechoka tupewe sisi zoezi kwa muda wa dakika 15 tukapigane. Lakini na Tanzania Bara hali kadhalika. Kwa hiyo, tuna sababu zote za kuipenda Jamhuri ya Muungano, lakini kama Chama chetu kinavyosema kwamba, Sera ya Chama cha Mapinduzi, Serikali mbili na hilo halitaondoka abadani kwa sababu Chama cha Mapinduzi ndicho Chama Tawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niupongeze uwekezaji. Naupongeza kwa sehemu ya mafuta ya petroli na umekuwa mzuri kutokana na mashindano ya kibiashara ndani ya petroli, dizeli, pamoja na mafuta ya taa. Nimetembelea sehemu nyingi tu za Mkoa huu na nyingine zikiwa mbali kabisa kama Rudewa, Mkoma Ng'ombe, mote mafuta yamefika, dizeli, pamoja mafuta ya taa na petroli na kwingine hata hakuna *petrol station.* Kwa hiyo, ninaloliomba kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iende na wakati, muwekezaji wa petroli, *Zanzibar Gapco,* ametuchosha. Inafika wakati unakwenda kuweka mafuta, unaambiwa haya ni s*pecial* kwa magari ya watalii. Haichukui mwezi mafuta hayapo, haichukui mwezi mafuta yanapandishwa bei, kwa sababu anatamba yuko peke yake. Kwa leo, tunaiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iende na wakati na ushindani wa kileo, watafutwe wawekezaji wengine kwani yeye ameshashindwa kazi. Kuwe na mashindano kama yeye ameshashindwa kazi. Kwa heshima kabisa naendelea au nazidi kuipongeza huduma hii na kuiunga mkono kwa asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu mchana huu. Awali ya yote, nitamke kwamba, naunga mkono hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kigoma Kusini, nachukua fursa hii vilevile kuwapongeza wale wote waliopata nyadhifa mbalimbali kutokana Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwaka 2005. Lakini vilevile nianze na kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa kuwa Mwenyekiti wetu mpya wa Chama cha Mapinduzi na wale wote waliopata nyadhifa kwa kupitishwa na Halmashauri Kuu, kuingia kwenye sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi. Kama ilivyosemekana kwenye mkutano uliofanyika Dodoma juzi, viti vimepata watu na sisi tunaamini ni kweli kwamba, viti vimepata watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache lakini nianze kwanza kwa kuzungumzia suala la chakula, hali ya njaa na kilimo kama ilivyojitokeza nchini. Naishukuru sana Serikali chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete na usimamizi wa karibu wa Mheshimiwa Edward Lowasa, wakati wa kipindi cha njaa. Harakati zilizofanyika kusimamia upatikanaji na hatimaye ugawaji wa chakula kilichopatikana na kauli iliyotolewa na Serikali ilitimia, hakuna mtu aliyekufa kwa njaa. Hii imedhihirisha umahiri na utendaji wa viongozi wetu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukazia hilo, nipitie hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukarasa wa kumi na moja, amesema Serikali ilitoa pia shilingi bilioni 5.5, kwa ajili ya kugharamia usafirishaji wa chakula na shilingi bilioni 1.5 kwa Halmashauri za Wilaya, kwa ajili ya kununulia mbegu za mazao ya chakula. Naomba nizungumzie hapo, kwa kuainisha na Mikoa mingine inayofanana na Mkoa ninaotoka mimi, nizungumzie kuhusu Mkoa wa Kigoma. Kwa bahati nzuri sisi watu wa Kigoma tangu tumepata uhuru na kabla ya uhuru mpaka sasa, hatujawahi kupata msaada wa chakula na hatujapata sio kwamba wenye kutoa hawapendi kutupa, hapana. Hatujapata kwa sababu hatustahili kupewa, tunajitosheleza kutokana na hali halisi ya mazingira na hali ya hewa iliyoko kule kwetu.

Lakini nilidhani basi wakati Serikali inatoa msaada wa chakula kwenye maeneo haya, sisi tungeenziwa vilevile, tungepewa ruzuku ya mbegu kwa sababu baadhi ya chakula ambacho kimetawanywa katika nchi hii, kimetoka Kigoma. Sasa ingekuwa ni vizuri sisi tunaozalisha chakula ambacho kimewaendea wengine, tuwezeshwe kupata mbegu na pembejeo nyingine tuongeze uzalishaji, ili hao ambao wanaweza kupata matatizo na hatuombi yaendelee, waweze kupata chakula kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la Utawala Bora, niende moja kwa moja kuhusu uendeshaji wa Halmashauri zetu na kwa bahati nzuri TAMISEMI iko moja kwa moja chini ya Waziri Mkuu. Sisi Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kigoma, mwaka 2004 ilipata hati chafu na ninazo nyaraka hapa zinazotokana na ziara ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI alipotembelea Kigoma na kauli alizotoa na maelezo ambayo aliwaeleza Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Mkoa wa Tanga na Mkoa wa Kigoma, alipotualika chakula.

Hali halisi aliyoiona na hisia zake kuhusu uozo ulisababisha pengine hali ya Halmashauri kuwa vile, Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Kigoma, lilitoa Azimio la kumsimamisha kazi Mkurugenzi na likatoa Azimio vilevile la kuwasimamisha kazi na viongozi wengine watano.

Namshukuru Waziri Mkuu na ofisi yake imeundwa Tume ya kwenda kubaini ukweli, lakini ningependa niseme Mheshimiwa Waziri, yapo mambo mengine wakati mwingine hayahitaji Tume. Huhitaji kuunda Tume kujua kwamba, mbili jumlisha mbili ni nne na nieleze waswahili husema zamani wakati dunia inaumbwa, kulikuwa kuna herufi ‘h’ nne, narudia kulikuwa na herufi ‘h’ nne wakati dunia inaumbwa. Kulikuwa na haya na huruma, hila na hadaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunao viongozi ambao haya na huruma kwao imetoka, imebaki hila na hadaa, tunawasimamisha kazi viongozi kwa kufuata miongozo iliyopo, anatokea kiongozi mwingine anawatetea, anajaribu kuonyesha kwamba, sisi katika kuwasimamisha kazi hatukuweza kuheshimu Ilani ya Uchaguzi. Naomba nieleze katika Ilani hii, ni mahali gani pameandikwa kwamba, kiongozi akiwa mbadhirifu, asipoongoza vizuri, aendelee kuwepo tu na Madiwani wapige makofi wamwone ni mwenzao? Mtu akinionyesha ukurasa wowote katika Ilani hii, kwa haya niliyosema kama ni makosa, nitaomba radhi, hakuna katika Ilani hii mahali ambapo panasema kwamba, Mkurugenzi, Afisa Elimu, Bwana Afya, Daktari na Madiwani wapige makofi. *(Makofi*)

Mehshimiwa Naibu Spika, ningeomba Waziri aelewe leo kama pengine taarifa zilikuwa hazijamfikia. Mtihani wa darasa la nne mwaka 2005, ulitakiwa ufanyike nchi nzima tarehe moja tu, ni tarehe ya Kitaifa. Lakini Kigoma mtihani umefanyika Januari mwaka huu, naona hata Waziri Mkuu, anaonekana anakunja sura, ni jambo geni kwake. (*Kicheko*)

Mtihani umefanyika mwezi Januari mwaka huu, utaratibu wa kufanya mitihani kwa Mkoa wetu ni vipi, kwamba Afisa Elimu wa Mkoa anasema, mwaka huu Wilaya ya Kibondo ndio itakayosimamia gharama na uendeshaji wote wa mitihani. Pesa zote zikija anapewa Afisa Elimu wa Wilaya ya Kibondo na mwaka unaofuata ni kwa mzunguko. Kwa mwaka 2005, ilikuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, Afisa Elimu kwa uzembe wake na ninazungumza uzembe kwa makusudi, ameshindwa kutekeleza mambo yaliyotakiwa kufanyika, kukatokea kasoro, mtihani ikabidi ufutwe. Mtihani huo umefanyika Januari mwaka huu, hivi Madiwani wakiamua kumsimamisha kazi Afisa Elimu huyu, anatokea Afisa mwingine anasema tunakiuka Ilani ya Uchaguzi, amelitoa wapi huyu? *(Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipoamua kuwasimamisha watu wale, tulikuwa hatuna kisa wala sababu ya chuki na wao, hatuna nongwa na wao. Tulifuata taratibu zote na mimi naamini Tume ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ofisi yako imeipeleka kule, itabaini ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la rushwa. Zimekuwepo hoja watu wanasema wanapokea rushwa kwa sababu mishahara ni midogo au vipato ni vidogo. Hivi mesenja anasaini Mkataba gani? Maana mesenja ana kipato kidogo na hii rushwa anakutana nayo wapi, lakini ni sisi tuliopewa nyadhifa za kukutana na watu kwenye maeneo tofauti, tunaoweza kuidhinisha vitu vya kuendesha nchi, vya kuendesha Halmashauri, vya kuendesha Mikoa, ndio wenye mamlaka na kutokana na mamlaka tuliyo nayo, ndio tunaoshawishika. Nakuja kwenye ule usemi ulioko kwenye Biblia, japo kuwa mimi si mtaalam mzuri sana wa Biblia, aliyenacho anaongezewa, ndio anaongezewa kwa njia ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila sababu sisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, kuamini kabisa kwamba, upo uchafu ndani ya Halmashauri ile na mimi ningeomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ofisi yako, Tume isiishie pale, iende ndani zaidi.

Unajua wakati mwingine wapo watu wanakatazwa kufanya, lakini unafanya kutokana na mazingira. Mwaka 2005, wakati tunafanya kampeni, nilifika kwenye kijiji fulani, nikakuta yanateremshwa mabomba ya kutoa maji kwenye kijiji hicho, kinaitwa Kijiji cha Kalenge na mimi nikashiriki, nilijipendekeza ili nipate kura, ni mwaka 2005 huo. Lakini kwenye hii taarifa ya Mkaguzi Mkuu kwamba, kwenye kijiji hiki tayari mabomba yalishatandikwa na maji yanapatikana tangu mwaka 2004 na kwenye hati ile kuna zaidi ya shilingi milioni 200, hazina maelezo mazuri ya jinsi zilivyotumika na mkandarasi aliyepewa kazi ya kutandika mabomba amelipwa kabla kazi haijafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa iingie kwa undani, Madiwani wakichachamaa wanaambiwa wanakiuka yaliyoko kwenye Ilani ya Uchaguzi. Mimi ninazo nyaraka hizi na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitakupa ili Waziri yeye mhusika azipate. Nyaraka hizi zinahusu kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu, umeeleza masuala ya ujambazi unaofanywa na raia wageni wanaoingia nchini na hili nizungumze, nina maslahi binafsi na hili ninalotaka kulizungumza. (*Makofi*)

Mimi kwa kabila ni Mbembe, ninajua watu wengi mkisikia hivi wala hamlijui kabila hili. Sasa maafisa uhamiaji mnaowapeleka kwenye mikoa yetu mingine mingine huko, wanadhani kwamba, Mtanzania ni lazima kwamba asili yake kwa vizazi 40 awe alitokea Tanzania. Mimi sioni aibu kusema kwa vizazi, yaani kwa asili tangu kwa baba mpaka kwa mama, kwa asili ni Kongo, kama vilevile Waziri Mkuu, wewe kuna watu wa asili yako wako Kenya, kuna watu hapa kwa asili yao wapo Uganda, wapo Burundi. Lakini inatokea na hii ipo kwenye nyaraka hizi Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni aibu kwa Serikali yetu, kwa sababu wamechukuliwa watu kutoka Kigoma, wanaonekana si raia, wamepelekwa Kongo. Hii *document* ya Serikali ya Tanzani, iliyokuwa *attached* ni *document* ya Serikali ya Kongo, inawakataa watu hawa kwamba tu kwa sababu ni Wabembe na Wabembe asili yao ni Kongo, basi wameonekana sio raia wa Tanzania. Lakini tunao wangapi hapa, tunao Waarabu humu, tunao Wahindi, tuna Wazungu, ni raia wa Tanzania. (*Makofi*)

Sasa ni lazima Serikali iwe makini, isiwe inawatazama watu kwa uasili, hapana, uraia wa mtu utazamwe kwa misingi ya uraia, sio kwa kabila lake kwamba, *original* yake ni wapi. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, nitakupa nyaraka hizi.

La mwisho Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninalo gazeti la leo, nalo vilevile nina maslahi nalo. Hili gazeti, kwa kichwa cha habari huu ni uchochezi, *Bishops warn over Chief Kadhi Courts*.

**NAIBU SPIKA:** Unaomba ruhusa kwa Spika, ukitaka kusoma.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA:** Hapana, silisomi.

**NAIBU SPIKA:** Unasema unaomba kunukuu?

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ruhusa.

**NAIBU SPIKA**: Endelea.

**MHE. MANJU S.O. MSAMBYA**: Katika gazeti hili, tunaelezwa kwamba, Mahakama za Chifu Kadhi hazitakiwi, hivi ni nani anatakiwa kutoa kauli; hivi watu wakitaka kupeana masuala ya kipaimara, BAKWATA wanakauli kwa hilo? Serikali iachwe i-*operate* katika misingi yake, kisitokee chombo kingine kinaishawishi Serikali kwa kutaka, maana hii tayari tunapoambiwa kuna masuala ya mihadhara, yanaweza yakagombanisha watu. Kauli hii vilevile inaonekana kwamba, Serikali inapewa maelekezo kutoka mahali pengine, Serikali ina njia zake za kufanya kazi, ijielekeze, ifanye kama inavyoona kwa mujibu wa Katiba, Sheria na taratibu zilizopo. Sasa sio chombo kingine kionekane kinataka kuisaidia Serikali ku-*operate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, asante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, humu ndani nikisoma zile kanuni zetu inasema Mbunge hatakuwa anasoma wakati anatoa hotuba yake. Kwa hiyo, kama Mheshimiwa amepata gazeti, anataka kunukuu basi anasema kwa ruhusa yako, Mheshimiwa Spika naomba ninukuu, kwa hiyo, anamwambia soma, ndio utaratibu. *(Makofi)*

**MHE. ZULEIKHA YUNUS HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, kama walivyoanza wenzangu. Kwanza, sina budi nami kumpongeza Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa, pamoja na wale wengine wote walioteuliwa, kwa hiyo wote nawapongeza kwa Chama cha Mapinduzi. Vilevile naipongeza hotuba ya Waziri Mkuu, mia juu ya mia, karibuni yote yaliyomo yamefahamika, ya ufasaha na ya ufanisi. Nikianza kuhusu masuala ya *TASAF*, kwa kweli nimefurahi baada ya hii *TASAF* awamu ya pili kwamba, imewashirikisha hata na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Baada ya ile semina tuliyopatiwa mwezi wa nne hapa, Waheshimiwa Wabunge na kule Zanzibar kwa bahati vilevile Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, nao walipatiwa semina. Kwa hiyo, nami niliporudi Zanzibar, nikazungumza na viongozi na watu wenye ulemavu kuhusu *TASAF* awamu ya pili, ili wafuatilie waone na wao watashirikishwa, vipi na hatua wameshazichukua na tayari wanaendelea katika mipango ya ushiriki.

Vilevile kuhusu mpango wa MKUKUTA, ambapo kwa Zanzibar kuna MKUZA. Kwa hiyo, hata kule Zanzibar mimi niliwahi kushiriki kwenye MKUZA, sijui huku Bara, kwa Zanzibar watu wenye ulemavu wameshirikishwa moja kwa moja kwenye masuala ya MKUZA. Sijui huku Bara, labda mwenzangu ataeleza zaidi MKUKUTA umewashirikisha vipi watu wenye ulemavu. Vilevile nimefurahi kwamba, MKUKUTA na MKUZA wana mipango na mashirikiano mazuri katika kuendeleza Mradi huu. *(Makofi)*

Jingine kuhusu masuala ya elimu, naipongeza Serikali kwamba, elimu imezidi kupanuliwa hasa kupitia huu Mradi wa *MEP* na MMES na naunga mkono ujenzi wa Chuo Kikuu cha hapa Dodoma. Lakini kwa upande wa elimu, bado kwa watu wenye ulemavu kuna matatizo, kuna shule za msingi ambazo mwanzoni zilikuwa nyingine za watu wenye ulemavu maalum na nyingine zilikuwa za mchanganyiko *(integration)*.

Kwa mfano, kuna shule moja inaitwa Hombolo hapa Dodoma, shule hii hivi sasa kumekuwa na mabadiliko, watu wenye ulemavu hawafaidiki nayo na ingawa ni ya mchanganyiko, lakini jana tu walinifuata watu wenye ulemavu wa hapa Dodoma, kunieleza kuhusu matatizo ya shule hiyo na wameniomba shule zitakapofunguliwa, nikaitembelee. Wameniomba hilo nilizungumze hapa shule ile ikaangaliwe hayo matatizo wanayoyapata watu wenye ulemavu wanaosoma pale. *(Makofi*)

Kuhusu maendeleo ya wanawake kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na mimi naungana na wenzangu kwamba, Wizara hii ndio jicho la wanawake wa Tanzania. Kwa hiyo, kuna haja hii Wizara kupewa kipaumbele na kupewa bajeti yake, iongezewe ili kuleta maendeleo kwa wanawake wa Tanzania. *(Makofi*)

Kuhusu masuala ya Muungano, kutokana na mkakati uliowekwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwamba, viwe vinakutana vyombo viwili baina ya Waziri Kiongozi wa SMZ na Waziri Mkuu na hatua zimeanza kuchuliwa na mafanikio tumeanza kuyaona. Sasa tunaomba waendelee, kama alivyosema Rais wa Jamhuri, hata kama hawajapata la kulifanyia kazi, wakutane tu kuambizana ile *asalaam alaykum* pia itasaidia. *(Makofi*)

Kwa hiyo, kuhusu suala la Muungano, ni kweli nakumbuka ilikuwa mwezi wa tatu ule, walikutana Watendaji Wakuu wa Wizara ya Elimu Zanzibar na Watendaji Wakuu wa Wizara ya Elimu Bara na walikutana Arusha kule naona waliweka mipango mizuri tu, kwa hiyo, hayo ndio mafanikio. Vilevile nasikitishwa sana na watu hao wanaoutiatia maneno huu Muungano. Kwa hiyo, wananisikitisha sana na ukizunguka bado tunao bado wametuganda. *(Makofi*)

Kuhusu suala lingine la kilimo naomba kulizungumzia. Jana kuna Mbunge fulani alizungumzia masuala ya kilimo kwamba, Wizara ya Kilimo ya Jamhuri ya Muungano iisaidie Wizara ya Kilimo Zanzibar, kuna mambo mbalimbali, suala hili mimi naliunga mkono. Lakini alizungumzia vile vile kuhusu zao letu la karafuu, akasema kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, inawadhulumu, inawaonea wakulima wa karafuu, mimi lile napinga nalo, kwa sababu zao la karafuu linashughulikiwa, kuna chombo maalum kilichoundwa, *Zanzibar State Trading Cooperative (ZSTC)* na kina mipango mizuri tu na mikakati mizuri. Labda wao wenyewe tu kutokana na tamaa zao binafsi, hata hizo karafuu wanaziharibu, mashamba ya karafuu yanachomwa moto, mijini wanazuiwa siku zote wanakamatwa kwa magendo. Siku hizi KMKM imezidi kufanya kazi nzuri, hawapati kuzipeleka, wanahiyari zioze, mradi fujo mbalimbali zinafanywa. Kwa hiyo, mimi hayo ninayapinga. (*Makofi*)

Nikiendelea sasa nakuja upande wa masuala ya watu wenye ulemavu, nimefurahi kwamba, kwenye hotuba yake Waziri Mkuu, kagusia sana masuala ya watu wenye ulemavu na ukija kwenye Ilani ya Uchaguzi yamo na kwenye hotuba ya uzinduzi, Mheshimiwa Rais wakati alipolizindua Bunge yamo. Hivyo basi, nimetumwa na watu wenye ulemavu wa Bara na Visiwani kwamba, sera tayari ilishapitishwa hapa Bunge hata kule Zanzibar kwenye Baraza la Wawakilishi, sera kuhusu watu wenye ulemavu imeshapitishwa na kwenye kikao hiki cha bajeti kule Zanzibar Muswada wa Sheria utapitishwa. Hivyo basi, wameniomba watu wenye ulemavu wa huku Bara wanaulizia ule Muswada wa Sheria ambao tayari umeshafanyiwa kazi, utapitishwa lini hapa Bungeni ili uanze kutumika na kufanyiwa kazi?

Vilevile kuna haya mambo ya Kimataifa, kwenye hotuba yake Waziri Mkuu kuna ukurasa sijaunukuu alizungumzia masuala ya wanawake, pamoja na mikataba yao na akataja walemavu, lakini basi hakumalizia. Kwa hiyo, naomba kukujulisha kwamba, kuna hii *convention* ambayo *finally* yake itafanywa mwezi wa nane, kutakuwa na mkutano ku-*finalize* hiyo *convention* kuhusu *DPI*, yaani watu wenye ulemavu duniani. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, ipeleke mwakilishi ambaye ataridhia kama ilivyoridhiwa haki za watoto, haki za wanawake na vinginevyo. Kwa hiyo, tunaomba hili kwa niaba ya watu wenye ulemavu. Bado muda upo, kwa hiyo, lifuatiliwe ili mwezi wa nane tupate mwakilishi rasmi kutoka Serikalini na yeye akahudhurie na kuridhia Mikataba hiyo ya Haki kwa Wenye Ulemavu Duniani. (*Makofi*)

Vilevile kuna suala hili lingine wanaloliita *African Decade*, ambayo ilifanya *review* yake mwaka 2005 Ethiopia, sasa vilevile watu wanaomba suala hilo nalo, Serikali ilifuatilie. Miongoni mwa yaliojadiliwa kwenye *African Decade* ni kwamba, hivi vyama vya watu wenye ulemavu au masuala ya watu wenye ulemavu, badala kuwa ya chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, yawe chini ya Waziri Mkuu. Kule Zanzibar tayari imeshakubalika na yameshakuwa yapo chini ya Waziri Kiongozi. Kwa hiyo, tunaomba na huku kuwe na uwezekano, masuala ya watu wenye ulemavu yawe chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ili iwe rahisi kama tunavyojua, Ofisi ya Waziri, ndio mratibu wa Wizara zote. Kwa hiyo, itarahisisha kufuatilia masuala ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda usije ukanimalizikia, kwa hiyo, zaidi ya haya ni kwamba, naunga mkono hoja mia juu ya mia, kwa niaba ya watu wenye ulemavu na Chama cha Mapinduzi. Natoa shukrani kwa kutupatia nafasi watu wenye ulemavu kuwemo kwenye chombo hiki cha maamuzi na tunaomba tuzidi kushirikishwa kwenye vyombo mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kuchaguliwa kushika nafasi ya Uenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Hakika tuna kila sababu ya kumpongeza, kwani yeye ni Wazihi wetu wa kisiasa ndani ya Chama cha Mapinduzi katika awamu hii ya nne. Vilevile napenda niwapongeze wale wote walioungana naye, aliyowateua kwa kushirikiana na Kamati Kuu na Halmashauri kuu ya

Chama cha Mapinduzi, kushika zile nafasi kuu katika uongozi wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake mahiri na nzuri, ambayo imekidhi katika awamu hii ya nne. Naipongeza kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu, amekuja na kauli mbiu katika hotuba yake, inasema: “Asiyeweza kucheza ngoma hii kwa mdundo ambao yeye amekuja nao, basi yeye atoke nje, atupishe sisi tuendelee na kazi.” *(Makofi)*

Mimi nakubaliana naye kabisa kwamba safari hii ya awamu hii ya nne ngoma mdundo, lakini je tunaweza kwenda na huo muundo kutokana na matatizo tunayoyapata huko katika maeneo yetu, asante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hotuba ya Waziri Mkuu, aligusia suala la wanawake. Nataka nimtoe wasiwasi Mbunge mmoja aliyesema kwamba, CCM hatuwaangalii wanawake, si kweli tuna asilimia 30 ya viongozi wanawake, akiwemo yeye mwenyewe kutoka katika chama alichokuwa ameteuliwa. Hizo zote ni jitihada za Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, nataka nimtoe wasiwasi na kumwambia kwamba, sisi Chama cha Mapinduzi, tunajali kila mtu, bila kujali itikadi yoyote ile, cheo chochote au elimu yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda haraka haraka ili niweze kukidhi muda wangu. Nataka nigusie suala la Ulinzi na Usalama, ambao umegusiwa katika hotuba. Tunashukuru nchi yetu ni ya amani, utulivu na upendo, lakini bado kuna masuala ambayo yanaleta utata kwa baadhi ya watu, inawezekana kutokana na mila potofu au utashi wao. Suala la ubakaji, suala la unyanyasaji wa watoto wa kike na wazee, kwa kweli bado linahitaji liangaliwe kwa kina zaidi, ili wanawake na watoto waweze kuendelea kuishi kwa amani na usalama kama hapo zamani. *(Makofi)*

Suala lingine, umetufurahisha sana uliposema kwamba, kila Mkoa utapata shilingi milioni 500, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ndio sasa tunakwenda na ule mtundo uliusema. Baada ya kuambiwa tutapewa kila Mkoa shilingi milioni 500, basi naomba tupewe ufafanuzi au utaratibu pesa hizi zitakwenda vipi, tusije tukajikuta huko shilingi milioni 500 zimefika, hatujui zimegawiwa vipi na Mikoa iangaliwe ina Wilaya ngapi. Nimesikia watu wengine wanaanza kupiga kelele wao wana wingi wa watu, si kweli watu wale wengine wanatoka Mkoa wa Pwani.

Kwa hiyo, unaweza kukuta wengine asubuhi wanakwenda kule na jioni wanarudi Mkoa wa Pwani. Naomba tuangalie ukubwa wa Wilaya, lakini la muhimu zaidi katika suala hili, tusiisahau Wizara yetu ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Hii Wizara lazima ipewe kipaumbele katika hizi shilingi milioni 500, ili tuweze kuona maendeleo ya Wanawake na Vijana yanakwenda sambamba na ili kuweza kupata maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la afya pia limegusiwa. Naipongeza Serikali kwa kujali afya za Watanzania lakini nina masikitiko makubwa sana kutoka Mkoa wa Pwani,

ambako nimetumwa na wananchi wa Mkoa wa Pwani na hasa Wanawake. Mkoa wa Pwani kuna wilaya nyingine zinasikitisha, kwa mfano, nikianzia na Wilaya ya Mafia, ina wakazi 20,000 na ina zanahati haina kituo cha afya.

Watendaji na madaktari bingwa hakuna, manesi wako wachache, naomba suala hili tuliangalie ili tuwe na afya bora. Mkuranga hali kadhalika, hakuna hata kituo cha afya, sasa tunapozungumzia maisha bora kwa kila Mtanzania, basi naomba tuangalie katika nyanja zote.

Kuna suala la barabara, hili naomba kwa kusema methali moja, Waswahili wanasema: "Ukiwa karibu na waridi, basi na wewe utanukia waridi." Sasa sisi Mkoa wa Pwani, tupo karibu na Dar es Salaam, ukipita Kibaha utafika Dar es Salaam, ukisema utapitia Bagamoyo utakwenda Dar es Salaam na ukisema wewe unataka upitie Mkuranga, ukitoka Mikoa ya Kusini utafika Dar es Salaam. Lakini cha kusikitisha barabara za Mkoa wa Pwani zinasikitisha sana. Wilaya ya Kisarawe, kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wabunge, imetimiza miaka 100 katika awamu hii. Hivi leo ninavyosema, ndiyo kwanza, tumepata kilomita sita za barabara ya lami, imefika pale Kisarawe kwenye kile *keep left.*

Sasa maendeleo haya sisi yanatupita pembeni, tunahitaji Mkoa wa Pwani, tupate maendeleo endelevu kwa sababu wakulima wanapolima mazao yao, wanahitaji kuyapeleka sokoni lakini unakuta hata barabara zenyewe wakati wa kupeleka mazao hazipitiki. Barabara hazina lami, zinahitaji viungo kwa maana ya kwamba, ukitoka Bagamoyo, uweze kupita ndani kwa ndani utokee Kisarawe. Ule msongamano uliojaa pale Dar es Salaam, nina hakika kama kutakuwa na utaratibu wa kuunganisha barabara kutoka Wilaya moja kwenda nyingine, ndani kwa ndani, nina hakika, msongamano wa magari Dar es Salaam utakwisha. *(Makofi*)

Mfano mzuri, takwimu zinaonyesha kwamba, Mji mmoja pale London, mchana kuna watu milioni tisa, ikifika saa sita mchana, ikifika saa kumi jioni au saa sita usiku wanabaki watu milioni tatu mpaka milioni nne; kwa nini? Kwa sababu wamesambaza maendeleo katika maeneo mengine. Sasa basi na sisi Mkoa wa Pwani, ili tunukie jamani, tusogezeeni viwanda na mtaona hawa watu wote asubuhi wanaelekea hukohuko Mashariki, wengine wanatakiwa waende Magharibi na wengine Mashariki, lakini wote Dar es Salaam wakiamka wanakwenda njia hiyohiyo. Dar es Salaam itaacha kujaa watu? Tusogezeeni viwanda Mkoa wa Pwani ili vijana wetu, akina mama na watu wengine, wapate ajira. Mimi nimetumwa na watu wa Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Kuhusu maji, kwa taarifa Waheshimiwa Wabunge Mkoa wa Pwani ndiyo wenye sifa ya mito mikubwa yote, Mto Rufiji uko Mkoa wa Pwani, Mto Ruvu uko Mkoa wa Pwani, lakini ninavyokwambia palepale Mlandizi tu kama kilomita tano, tone la maji hulipati. Maji yote yamepelekwa Dar es Salaam, sasa kweli sisi tutanukia? Hatuwezi kunukia hata siku moja, tunaomba basi ufanywe utaratibu pale. Mtambo wa maji wa Ruvu umejengwa mwaka 1964, mtambo wa umeme Hare umejengwa mwaka 1954, umepita tu pale umeruka Dar es Salaam. Pwani yenyewe ambapo ndiyo njia imepitia, hatuna umeme maeneo mengine, hatuna maji maeneo mengine. Sasa tunataka kwenda

kwa mdundo wa ngoma itakayopigwa, sisi watu wa Pwani, tupo tayari kucheza hiyo ngoma, lakini tupatieni hayo mahitaji muhimu na mtuhakikishie kwamba, katika suala la kilimo, mmetuhimiza sisi tutalima lakini kama tunalima hatuna viwanda vya kutosha, basi kilimo chetu kitakuwa hakina maana, tuhimize kilimo na tuhimize viwanda.*(Makofi)*

Tuna maeneo makubwa yapo wazi, ambayo mnaweza mkaja kujenga viwanda vya aina mbalimbali, tuna maeneo ambayo mnaweza mkaweka masoko, magari yanayotoka Arusha, Mbeya yakaishia hukuhuku. Sisi tukafaidika pale mkajenga viwanda, masoko ya jumla yakawa yako Mkoa wa Pwani, Wilaya yoyote katika Wilaya zetu sita, mkaweka pale masoko ambayo yataleta manufaa kwa wananchi wa Mkoa wa Pwani na wananchi wa Dar es Salaam. Mazao yakija pale yatakuwa yanafunguliwa kwenye malumbesa yale yanafungwa tena, yale matakataka badala yakuyatupa ovyo, mnahangaika, kwa mfano, Kariakoo Sokoni. Lakini mkiyaweka Mkoa wa Pwani, ile ni mbolea, tutaepukana na mbolea yenye sumu jamani, tukichukua majani yale na mazao yatakayooza, tukiyachanganya tukayatengeneza mboji, hatutaleta maendeleo; hatutawaelimisha watu wetu jinsi ya kufunga mazao yao?

Tuangalie mfano matunda yanayotoka *South Africa*, yale ma-*apple*. Ukiona ma-*apple* yanayolazwa chini sokoni Kariakoo, yanapangwa mafungu, basi ujue hayo yametoka Lushoto Mkoa wa Tanga, huwezi ukakuta *apple* lilitoka *South Africa* limepangwa na Wamachinga chini, kwa sababu tayari wenyewe huko wameshayafunga na yamekuja na huo ustaarabu. Sasa naomba tufikirieni na sisi watu wa Mkoa wa Pwani, kwa kuweka hayo masoko ya jumla na mtufikirie kufungua barabara, tunapokwenda Mkuranga, tunapata tabu sana na wanaotoka Mkuranga kuleta mazao Dar es Salaam, wanapata tabu sana. Kwa sababu njia ni moja, lazima mtu apite Mbagala, apite Mtoni kwa Azizi Ali, anachukua saa sita au saba. Lakini wakati sasa umefika tufikirie kujenga Daraja la Kigamboni, ambalo litasaidia kurahisisha watu wanaokwenda Mkuranga, Rufiji, kwa kipindi cha nusu saa mtu umefika Mkuranga. Naomba sana tuyaangalie haya maeneo ambayo yataleta maendeleo kwa Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, amezungumzia suala la UKIMWI. Mimi nasema hivi, wakati umefika sasa hawa waathirika tuwaangalie vizuri, kwa maana kwamba, tarehe 6 Desemba 2005, zilizinduliwa dawa za kurefusha au kuongeza kinga za mwili kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI. Sasa kama kiwanda tunacho Tanzania, bado watu wanaopewa hizo dawa ni wachache, kweli tunawapenda wananchi wetu wengine?

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara ya Afya, iliangalie suala hili na watu wanaopata hizo dawa ni watu wa Dar es Salaam au wanaoishi mijini, sasa wale wa vijijini tunawaangaliaje? Naomba sana tuokoe maisha ya watu, kwa kuhakikisha dawa tunazozalisha hapa nchini na zinazotoka nje, zinawafikia wananchi wetu ili kuweza kuhakikisha, tuna Taifa ambalo lina afya bora, sisemi kwamba, anayeishi na virusi vya UKIMWI, hana afya bora bali ana afya bora, lakini anahitaji mapenzi, upendo na kuangaliwa ili na yeye awe miongoni mwa wale tunaosema kwamba, maisha bora kwa kila Mtanzania. Tunapomnyima dawa basi tunakuwa hatukumtendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia katika hoja hii ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe pongezi za dhati, kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuvishwa kofia nyingine ya kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, uamuzi ambao ni wa busara na hekima, ambao utaendelea kukiimarisha Chama cha Mapinduzi na utekelezaji mzuri wa Serikali ya Awamu ya Nne. *(Makofi)*

Nawapongeza vilevile wale wote waliopata nyadhifa, kuanzia Katibu Mkuu na wenzake, ambao watasaidiana katika kuendesha Sekretarieti ya Chama cha Mapinduzi. Nawatakia kazi njema na afya njema katika kutekeleza majukumu ya chama chetu, ambacho ni Chama Tawala na Mwenyezi Mungu awasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze kwa dhati, Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa jinsi alivyoiwasilisha hoja yake vizuri, hoja inayolenga kuhakikisha kwamba, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inatekelezwa. Ilani ni ahadi za chama chetu, ilizozitoa wakati inatafuta kuiongoza Serikali. Kwa hiyo, kwa kukubalika kwa asilimia kubwa na Rais akatoka ndani ya Chama cha Mapinduzi, hakuna budi ni lazima kazi ifanyike kuhakikisha kwamba, ahadi hizo zinatekelezwa. Kwa hiyo, kinachotekelezwa ni Ilani ya Chama cha Mapinduzi na mimi naipongeza Serikali, kwa kuweka mkakati mzuri wa kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza Serikali, kwa kufuta *VAT* katika mafuta ya magari na vilevile kupunguza gharama katika matumizi mbalimbali, ama ya gesi, mafuta ya taa, kwa lengo la kuimarisha au kuweka vizuri mazingira yetu na kutunza mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali kuhusu mafuta ya magari na punguzo zilizotolewa tunaomba tuzione. Tunaomba tuone mafuta ya magari kuanzia tarehe 1 Julai, 2007 bei inapungua, isiendelee kupanda ovyo ovyo na kwa maana nyingine basi, naiomba Serikali ijaribu katika hili, kusimamia bei ya mafuta ya *petrol*, *diesel*, mafuta ya taa, gesi na kadhalika. Uzoefu wetu unatuonyesha kwamba, Serikali inapoondoa kodi au inapopunguza ushuru, wale wafanyabiashara wanaendelea kuongeza bei, wanapata faida kubwa huku wananchi waliokusudiwa punguzo hilo, liwasaidie na hawafaidiki nalo. Kuondoa *VAT* katika mafuta, kutasaidia zaidi hata katika viwanda. Kwa hiyo, hata bidhaa zetu zinazozalishwa, bado zitapunguziwa gharama na kwa hiyo, hata wananchi wetu watazitumia kwa unafuu zaidi. Naomba suala hili, Serikali iwe *serious*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la MKUKUTA, naipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametamka bayana kwamba, Benki zitahusika katika kutoa mikopo midogo midogo, kwa riba tofauti. Ninarudia alisema: “Ninaomba Benki za Tanzania, ambazo zinatoa huduma kwa wananchi, kuhakikisha kwamba,

mikopo itakayokuwa inapitishwa kwao, kwa lengo la kusaidia wananchi waliounda vikundi au mmoja mmoja katika suala zima la kupambana na umaskini na kujiongezea kipato, zihakikishwe zimepewa dawati maalum na dawati hilo liweze kuhakikisha kwamba, kila anayefika pale, anapata huduma, maelekezo na elimu ya kutosha, itolewe mapema ili pesa hizi zionekane zimefika kwa walengwa."

Liko tatizo la kuzungusha watu wanaokwenda kuomba pesa hizo, mtu anakwenda mara mbili au tatu. Natoa mfano wa Muleba, kutoka Muleba Kaskazini kwenda Makao Makuu ya Muleba ni shilingi 1,500 hadi 2,000 ya sasa. Kutoka Bukoba kwenda Muleba ni shilingi 1,000 mpaka 1,500 na bei itaongezeka kama udhibiti hautakuwepo. Kinakwenda kikundi cha watu wanne kwenda kufuatilia mkopo zaidi ya mara tano, mwisho wanashindwa kuchukua mkopo huo na wanaishia kuona kwamba, ahadi hii haitekelezeki. Naomba suala hili lizingatiwe ili kuhakikisha kwamba, mikopo iliyolengwa, basi maelekezo yatolewe mapema kabla kikundi hakijakwenda kuchukua pesa zile ili kinapofika iwe siku ya kwanza kikamilishe utaratibu na ikiwezekana siku ya pili, wapate pesa wakaendelee kuzitumia kwa malengo ambayo wamekusudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali kwa kutaka kuanzisha Chuo Kikuu hapa Dodoma. Sasa hivi tupo Wabunge 350, ukweli wenyewe tunatamani kweli kusoma, lakini elimu hii ya kwenda Dar es Salaam ama kwenye *internet* na kadhalika, kwa kiwango kikubwa kweli inatufanya tushindwe kufikia pale ambapo tunaweza kufika. *(Makofi)*

Nami naamini kabisa kwamba, chuo hiki kitakapokuwa kimeanzishwa hapa Dodoma, Wabunge wengi watapenda kujiunga na elimu ya chuo hicho, kitakachokuwa hapa. Kwa hiyo, naomba chuo hicho kianzishwe haraka kwelikweli. *(Makofi)*

Pia nawapa pole wale wanaotangaza kwamba, sera hii ni sera yao, nawaambieni pole sana, sera hii ni ya Chama cha Mapinduzi na ndiyo watakaoitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali sana kwa kuwa na jengo zuri namna hii la Bunge. Namshukuru Mungu na wananchi wa Muleba Kaskazini, kwa kuniwezesha kuwa mmoja katika jengo hili zuri namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokiomba, Bunge letu limewahi kutambua wale waliofanya vizuri mara nyingi katika masomo, michezo na kuiletea nchi yetu heshima. Wale walio-*design* jengo hili na kulisimamia tena ni Watanzania wenzetu, kampuni yetu ya Tanzania hapa. Naomba waje rasmi ndani ya Bunge, nao watambuliwe, kusimama tu pale mbele tukawatambua walau kama heshima, wakati Bunge linaendelea. Itakuwa ni jambo ambalo litabaki ndani ya kumbukumbu za Bunge na hata miaka mingine zaidi itambuliwe kwamba, watu fulani au kampuni fulani ya Kitanzania, ilijenga na hawa walitambuliwa rasmi na Bunge. Nadhani jambo hili ni dogo, lakini ni la heshima kwa wale waliohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende katika kuzungumzia suala zima la Serikali za Mitaa. Hotuba ya Waziri Mkuu, imejaa maelekezo, maazimio na

mapendekezo mazuri mno, lakini kikubwa ambacho ningependa nikiombe na nirudie kukiomba, kwa sababu wenzangu wameshalisema sana hili, ni suala la kusimamia utekelezaji, kudhibiti wale wanaokwenda kutekeleza na katika hili nataka niende moja kwa moja katika suala zima la wenzetu kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ukurasa wa 31, kwa ruhusa yako naomba ninukuu, inasema: "Lengo la Serikali inaendelea kuziimarisha Serikali za Mitaa, ziwe vyombo shirikishi vya wananchi, vinavyotekeleza majukumu yake kwa ufanisi na uadilifu, kwa kiwango cha juu ili Serikali hizi ziweze kuwajibika kikamilifu kwa wananchi."

Mheshimiwa Naibu Spika, ili lengo hili la Serikali liweze kufikiwa, Serikali imetuambia mkakati wake inataka ihakikishe kwamba, inapeleka madaraka mpaka Serikali za Mitaa, inaongeza kuhakikisha kwamba, majukumu na raslimali zaidi kutoka Serikalini zinaongezwa kwenye Serikali za Mitaa. Lakini nilipokuwa najaribu kubadilisha mawazo na wenzangu na kutazama uzoefu, tumekuta kwamba, Halmashauri za Wilaya ambazo zimepewa majukumu makubwa, zimeongezewa madaraka na kazi. Ninaa hakika ninaweza nikasema kwa namna nyingine, ndiyo kama moyo pengine ama uti wa mgongo wa utendaji wa Serikali yetu sasa hivi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuta bado tunayo mapungufu mengi, kwa mfano, napenda nisemee suala zima la mapungufu katika uadilifu na mapungufu katika utendaji. Madiwani ambao wako karibu na Mkurugenzi, hawana wajibu, madaraka, hawakubaliwi kwamba, wao ndio wanaomsimamia Mkurugenzi. Kwa hiyo, yale maazimio yanayotokana na Mabaraza ya Madiwani, kama Madiwani hawawezi kuyasimamia kwa kumuwajibisha Mkurugenzi, sasa nani asimamie pale? Nimekuta kwamba, Wakuu wa Wilaya hawana nafasi ya kumsimamia Mkurugenzi, ni hiari ya Mkurugenzi kuwasiliana na Mkuu wa Wilaya, akipenda anaweza kumpa taarifa anapotaka kusafiri, anaweza kumpa taarifa ya pesa alizopata na jinsi alivyopanga kufanya kazi, anafanya vilevile anavyoona yeye anapenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona huu ni udhaifu mkubwa, madaraka makubwa yamepelekwa kwa watu ambao nani anawadhibiti hawa? Hivi tungojee Waziri kutoka Dar es Salaam ama kutoka Dodoma, ndiye aende akadhibiti Wakurugenzi katika nchi hii? Yule wa Karagwe, Muleba, Lindi? Tarime na hata Kisarawe; kweli inawezekana?

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kabisa kwamba, katika suala hili, kama kweli tumedhamiria kwa makini kuhakikisha kwamba, tunataka Serikali za Mitaa zifanye kazi ni lazima tuseme awepo anayemdhibiti Mkurugenzi na huyo asiwe mwingine, awe ni Mkuu wa Wilaya. Apewe mamlaka ya kuweza kuhakikisha kwamba, anasimamia maendeleo kwa niaba ya Serikali Kuu, ambayo inawajibika kuhakikisha kwamba, hayo yanayotakiwa kutekelezwa kwenye Halmashauri ya Wilaya, yametekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ni muhimu na kama litakuwa halikusimamiwa na wala halikutekelezwa, tusitegemee kwamba, tutaweza kufanikiwa

katika Halmashauri za Wilaya. Lakini vilevile katika suala hili, kuna vikao vya Halmashauri za Wilaya, vinafanyika siku moja tu kuanzia saa nne wakati mwingine mpaka saa saba mchana wamemaliza. Kweli muda huu unatosha kuchambua mikakati, mipango, pesa zilizotoka kwenye Serikali Kuu, Mashirika na kadhalika na kuweza kuendesha Wilaya? Huu muda hautoshi. Hii sheria irekebishwe kuhakikisha kwamba, walau wawe na siku mbili za kuhakikisha kwamba, hotuba za Vikao vya Halmashauri, walau zinapata muda wa kusoma na kuchambua na kuhakikisha kwamba, utekelezaji unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine, wafanyakazi wadogowadogo katika Halmashauri hawajaangaliwa, Wakurugenzi wameboreshewa maslahi, Wakuu wa Idara na kadhalika, lakini wafanyakazi wengine hawajaangaliwa. Kama hao wafanyakazi wadogo wadogo hawaangaliwi, hutaweza kuhakikisha kwamba kuna uadilifu na uaminifu katika suala zima la hawa wanaomsaidia Mkurugenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ninalopenda kulizungumizia ni kwa upande wa vyama vya siasa. Mimi nilikuwa mmojawapo niliyeshiriki katika uchaguzi, nilikuwa nagombea Jimbo mwaka uliopita. Kuna unyanyasaji mkubwa sana wa wagombea wanawake katika Majimbo, wapinzani wetu sisi wanasimama na kuunda hoja za kijinsia, si hoja za kujenga Jimbo, si hoja za kusaidia Jimbo, bali ni hoja za unyanyasaji. Udhalilishaji huu unakuwa ni mkubwa mno, ambapo hakika kwa kiongozi anayetarajiwa kuja kuongoza wananchi, kuja kuwawakilisha, ni udhalilishaji unaoondoa utu wa binadamu. Suala hili Msajili wa Vyama vya Siasa anatuambia nini? Atuambie la kufanya kuwe na sheria.

Nakipongeza Chama cha Mapinduzi, kiliwapeleka wanawake 18, aliyepoteza ni mmoja, kwa hiyo, inaonyesha kwa kiwango gani ambavyo wananchi wanawaunga mkono wanawake. Kwa hali hiyo, kama wananchi wanakubali anayewania sasa kuchukua nafasi ya uongozi awe na lugha ya heshima, staha, lugha ya kujua na yeye anawania kuwa kiongozi, lakini bila kumdhalilisha mwenzake, ambaye wamekuwa wanawania nafasi moja. Jambo hili nilikuwa napendekeza liangaliwe sana na elimu ya siasa itolewe na kuwe na sheria inayodhibiti, kusudi katika kugombea kuwepo na haki sawa kwa wagombea wanawake na wagombea wanaume. Hii itajenga moyo kwa wanawake kuendelea kugombea na kufikia asilimia 50, ambayo Mwenyekiti wetu Mstaafu wa CCM, ameiomba iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninaomba usafiri katika Ziwa Victoria. Ninapozungumzia usafiri katika Ziwa Victoria, simaanishi Mwanza, Bukoba au Ukerewe hata kidogo, ninamaanisha usafiri wa Kisiwa ndani ya Kisiwa, wao kwa wao. Katika Jimbo la Muleba Kaskazini na Wilaya ya Muleba kwa ujumla, tunazo Kata tatu katika Ziwa Victoria na humo kuna jumla ya Visiwa visivyopungua kama 25, kwa upande wa Kaskazini ni 19. Sina hakika upande wa Kusini viko vingapi lakini kwa maana hiyo basi, hakuna usafiri wa ndani kwa ndani. Kwa hiyo, huduma ya afya ni mbovu, huduma ya elimu ni mbovu na huduma nyingine muhimu kwa wananchi wanaoishi katika visiwa hivyo ni mbovu, ninaomba Serikali itambue kwamba, ndani ya Visiwa vile pia wapo

wananchi wake na wananchi hao wanahitaji wapelekewe huduma, kuwe na usafiri kwa wananchi wake walio katika maeneo na katika mazingira magumu.

Kwa hiyo, katika suala zima la kuboresha mazingira ya watu wanaokaa katika Wilaya za mipakani, ninaomba pamoja na wenzetu wanaoishi katika visiwa ni wale walio katika mipaka, wako katika maeneo ambayo ni magumu kufikika. Kwa sababu ya ugumu huo wa usafiri hata watendaji wanaona ugumu wa kufika, kwa sababu ya kuogopa zile *risk* za kusafiri katika maji, kwa vyombo ambavyo havina uhakika. Kwa hali hiyo, hawafikiriwi ipasavyo katika maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, ninaomba katika suala zima la mradi wa kuimarisha chakula, niipongeze mikoa ambayo ni *big five,* ilifanya vizuri, lakini sasa ongezeni mikoa mingine. Mimi nimejiuliza kwa nini Kagera na Kigoma, hazikuingia kwenye programu, wana mvua nzuri za uhakika, mwaka huu hata chakula hawakupata shida sana, ukiondoa maeneo machache ambayo yalikuwa na ukame katika Mkoa wa Kagera, lakini kwa hakika hii ni mikoa ambayo ina uhakika wa mvua. Ninaomba iongezwe katika programu ya chakula, kwa sababu kuna uhakika wa mvua za uhakika na kuweza kuweka akiba kubwa ya chakula. Serikali ijiandae kuhakikisha kwamba, inakusanya akiba ya chakula cha kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi hii na mimi ya kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Lakini kabla sijachangia kwanza, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Pwani, kwa kuniwezesha kufika tena katika Bunge, haswa jengo hili jipya, nami kuwa mmojawapo wa kulizundua katika kuchangia bajeti ya kwanza, ambayo inaongelewa katika jengo jipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, kwa kura mimi nasema zote, labda yule bahati mbaya tu, alichanganyikiwa kidogo akaweka pembeni. Lakini na wale ambao wamekwenda pamoja naye, baada ya yeye kuchaguliwa akapendekeza na wengine wa kumsaidia, kwa hiyo, wote napenda kuwapongeza kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini napenda kuwapongeza viongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne, Viongozi Wakuu, Mheshimiwa Rais, pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Vilevile ningependa kuchukua nafasi hii, kuwapongeza akina mama wale wanaowawezesha viongozi wetu hawa, kwa kuwalea vizuri na kuwatunza ili waweze kufanyakazi zao vizuri; Mama Salma Kikwete na Mama Lowassa. Kwa kweli nimesikiliza wengi tu wakiwapongeza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini wanasahau kwamba, hakuna mafanikio ya mwanaume bila ya kuwa na mwanamke nyuma. Kwa hiyo, mimi nasema nawapongeza sana Mama Salma Kikwete na Mama Edward Lowassa, kwa kweli wenzetu hawa wanatusaidia kuwawezesha hawa wazee waweze kufanya kazi zao bila matatizo. Kwa hiyo, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi kwenye kuchangia hoja, ningeanza kwanza kuongelea kwenye suala zima la Halmashauri zetu. Kwanza, tumeambiwa hapa kutakuwa na fedha ambazo zitatolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Sasa wasiwasi wangu ni jinsi ya kuzigawa hizi pesa, kwa sababu kuna maeneo yatagawiwa pesa kutokana na idadi ya watu, ukubwa wa eneo na mengine mengi. Sasa nikifikiria Mafia, nimewahi kulisema hili kwingine, lakini naona bora niliseme hapa ili nipate jibu na wana-Mafia wasikie.

Mafia idadi yetu ni ndogo na hata tukifanya vipi hatuwezi kufikia Wilaya nyingine hata ya Mkoa wa Pwani tuliyonayo jirani, kutokana na wingi wa watu, lakini mbaya zaidi pia hata eneo letu ni dogo, hata tufanye nini badala ya kuongezeka, mimi nasema linapungua kwa sababu bahari nayo inachukua baadhi ya eneo la Visiwa vya Mafia. Sasa je, tukienda katika hali hiyo, sisi Mafia tutapata senti ngapi za Maendeleo?

Kwa hiyo, ningeomba pamoja na hayo kwamba, yapo yamewekwa katika utaratibu wake, lakini basi kiwepo kifungu kingine cha kutuangalia sisi ambao tupo katika hali ambazo kidogo ni tofauti na hatuna njia ya kuweza kujiendeleza kutokana na sisi tulivyo. Kwa hiyo, nategemea Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Wizara zake, ataona senti ngapi zitaweza kuongezwa ikiondoa huu utaratibu wa asilimia 70, asilimia 10 au asilimia 20 na kadhalika, ili na sisi Mafia tuweze kupata pesa za kutosha kama wenzetu wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine kwenye Halmashauri, ningeenda kwenye suala la watumishi. Nashukuru Waziri Mkuu, ametamka wazi kwamba, ataangalia kuona wenye uwezo kuangalia upya watendaji ambao wanatumikia Halmashauri zetu sasa na hilo nalo naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati mnaliangalia na wakati mnaajiri muangalie baadhi ya Wilaya. Kwa sababu baadhi ya wilaya hata ikitokea nafasi, wanapotangaza wanakuja kufanya *interview,* hawafikii idadi na wakati mwingine anakuja mtu mmoja, sasa akija yule mtu mmoja ana sifa zote, lakini utaratibu uliopo sasa hivi wanasema ni lazima kuwe na ushindani.

Hii iliwahi kutokea Mafia, amekuja mtu ana sifa zote, lakini kwa kuwa alikuwa peke yake, basi ikawa hakuweza kuajiriwa mpaka wawe zaidi ya mmoja. Sasa kwa mazingira ya baadhi ya Wilaya, kuweza kumpata huyo mmoja tu ushukuru.

Kwa hiyo, tunaomba hili nalo wakati mnapanga taratibu zenu za watumishi kwa Wilaya nyingine, mliangalie kwa sura tofauti kwamba, hata akija mmoja na ana sifa za kutosha, basi aweze kupewa nafasi ya ajira, aweze kusaidia maendeleo ya Halmashauri hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ningependa kuongelea juu ya hizi shilingi milioni 500, zitakazotolewa kwenye Mikoa. Tunashukuru sana kwamba, sasa hivi Serikali imeona umuhimu kutuletea fedha moja kwa moja, kwa kiwango kikubwa ili na sisi tuondokane na umaskini, tuweze kupata mikopo ambayo ina masharti nafuu. Lakini zuri zaidi, namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, ametamka wazi kwamba, Waheshimiwa Wabunge washirikishwe. Ni mategemeo yangu kwamba, wanaposemwa

Waheshimiwa Wabunge, basi tusije tukarudi tena tukaambiwa ni Waheshimiwa Wabunge wenye Majimbo, Waheshimiwa Wabunge wa Viti Maalum wasubiri. Maana yake sisi hatuna Majimbo, tuna Mikoa na tunawakilisha Wanawake Kitaifa. Sasa tunaporudi kwenye Mikoa yetu, basi tutambuliwe kwamba, ni Waheshimiwa Wabunge ndani ya Mkoa huo na sisi tushirikishwe kikamilifu katika Mikoa yetu tunayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa narudi kwenye suala zima la wafugaji na machinjio. Tunashukuru baadhi ya maeneo ya wafugaji, kuna machinjio ambayo yameshakuwepo kwa ajili ya kupata usafi wa nyama zetu tunazokula. Lakini pia ningependa kuwapongeza watu wa Dar es Salaam, ambao nao wameanza kuwa na nia ya kujenga machinjio mapya. Lakini bado mwendo ni mdogo mno. Sasa ukiongelea tu mahali pa wafugaji na kuchinjia ng'ombe, lakini ukiangalia Dar es Salaam pamoja na kwamba, hawafugi kiasi hicho, lakini wanachinja ng'ombe wengi kuliko hata hiyo Mikoa mingine na walaji wa nyama wa Dar es Salaam ni wengi na baadhi ya viongozi wengi tu wanaishi Dar es Salaam. Kwa hiyo, nategemea kwamba, Dar es Salaam iende haraka ili waweze kufungua hiyo machinjio mpya, ambayo wenyewe wanayo katika mipango yao, ili tuweze kupata kula nyama safi katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikirudi hapo nakuta wakulima wameongelewa, lakini sijaona mahali kwenye hotuba hii, wakiongelewa wavuvi. Inawezekana wataongelewa au wataongelewa kwingine, lakini sikuona mahali ambapo wavuvi hasa wakitamkwa kwamba, wataendelezwa vipi. Bahati mbaya sisi katika Mkoa wa Pwani, tukisema Pwani tu, *automatically* ni bahari. Kila Wilaya ya Mkoa wa Pwani, ukiondoa labda Kisarawe, inaguswa na bahari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunajiuliza, wenzetu wana maeneo ya kulima katika nchi kavu, sisi wenye maeneo ya kulima baharini tunafanyaje? Sisi hatuhitaji mbolea, hatuhitaji matrekta, ni shamba ambalo linataka kusaidia tu vitu vidogo kama maboti, labda na nyavu ili wenzetu hawa waweze kwenda kuvua na waweze kupata riziki yao. Baadhi ya Wilaya ni visiwa, visiwa ndani ya visiwa, kwa mfano, Kisiwa cha Jibondo hakuna kabisa ardhi ya kulima, zao lao lote liko baharini. Sasa tusipotamkwa na sisi tukajisikia hasa tupo. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais katika hotuba zake nyingine, amesema ataendeleza uvuvi. Lakini tukija kwenye vitabu hatukuti uvuvi, tunakuta wafugaji, tunakuta wakulima, pamoja na pembejeo. Sasa ningeomba na wavuvi nao tuwekwe mahali ili na sisi tuwe na uhakika kwamba, tutasaidiwa katika masuala mazima ya uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua hili limepitwa na wakati, lakini bado sijachelewa. Tumeongelea suala la nishati mbadala, tukaongelea suala la kupunguza bei ya mafuta ya taa na tukaongelea suala la kupunguza bei ya gesi, lakini tunasahau kabisa kwamba, tuna samadi ya ng'ombe na sasa hivi Mikoa mingi tu inafuga ng'ombe. Hata pale Dar es Salaam sasa tuna *biogas,* lakini haikuonekana mahali popote, hata vile vifaa vyake navyo, kwa wale wachache ambao wangependa kutumia *biogas* vifaa vile ni ghali. Sasa tungeomba moja katika nishati mbadala, tuongelee na vifaa vya *biogas,*

kupunguziwa kodi au kupunguzwa bei au vitengenezwe kwa wingi kupitia *SIDO* ili waweze kuvitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona kengele ya kwanza imelia, lakini mwisho kabisa, ningependa kukumbusha ahadi za Mheshimiwa Rais. Ahadi ya Kiwanja cha Ndege Mafia na ahadi ya gati Mafia. Nadhani Watanzania wote walisikia, wakati tunampongeza Mheshimiwa Rais katika Mkoa wa Pwani kwamba, baadhi ya viongozi wa Mkoa wa Pwani, ilibidi waje na helikopita, kiwanja kilikuwa kimefungwa. Sasa tunaomba katika kipindi hiki basi, hizi ahadi mbili tu ya kiwanja cha ndege pamoja na gati kwa Mafia ziweze kutekelezeka. Jamani Mafia tunapata tabu.

Mheshimwia Naibu Spika, bahati mbaya nimemaliza Kamati lakini Bunge halikuweza kunikodia ndege kurudi Jimboni, ikabidi nibaki Dar es Salaam kwa sababu hakukuwa na usafiri. Lakini bado ndugu zetu wanapanda mashua. Sasa mimi Mheshimiwa Mbunge nimekaa Dar es Salaam na ninalindwa na Bunge mpaka kikao kingine; je, hao wenzetu wanaosafiri na mashua, watasafiri nayo mpaka lini au pengine tukimaliza Bunge kama kiwanja cha ndege bado hakijatengenezwa, hivi Bunge litaendelea kuniweka mimi niache kwenda kwangu kwa muda gani? Kwa hiyo, naomba sana tena sana, tumeongea karibu miaka mingi, juu ya gati na kiwanja cha ndege. Jamani mlishawahi kuona ndege inakwama kwenye tope, basi ndege Mafia zinakwama. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana umkumbushe Mheshimiwa Rais na nyie wote, mkikaa kwenye *cabinet* kwamba, watu wa Mafia wanaomba mengine yote watajitegemea, lakini kwenye haya, hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za ndani zina tabu, hatuna vifaa vya kutengeneza barabara sawa tutaenda na baiskeli. Mgonjwa leo yuko Mafia anatakiwa kuletwa Dar es Salaam, hakuna meli, hakuna ndege, tunampakia kwenye mashua, si atafia njiani. Mama mjamzito amepata matatizo, bahati mbaya anatakiwa kupelekwa Muhimbili. Ndugu zangu mimi naomba wengine niwakaribishe Mafia, lakini mpande mashua halafu ndiyo mtajua jinsi gani ya kutuunga mkono, tunapoongelea habari ya gati na habari ya kiwanja cha ndege.

Tunaliongea hili kwa uchungu na tumeliongea kwa muda mrefu, lakini nasema *inshallah,* kwa kauli ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, tunaamini na hasa katika Awamu hii ya Nne ya ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, inawezekana wamesema maisha bora kwa kila Mtanzania. Tanzania yenye neema inawezekana, basi iwezekane kwa Mafia kupata kiwanja cha ndege na kupata gati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, nawashukuru wote na ninawatakia kila la kheri kwenye kazi zenu. Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais, akinamama waendelee kuwatunza na sisi tutaendelea kuwapa moyo, waendelee kuwatunza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuzungumza machache niliyonayo rohoni, yanayonikereketa na yanayowakereketa wananchi wa Jimbo langu la Mkanyageni na Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti mpya, pamoja na timu yake yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, ningeomba nijikite katika suala la kwanza la Utawala Bora, ambalo litaambatana na Usalama wa Raia. Katika nchi hii, inaonekana bado dhuluma zipo nyingi mno na dhuluma ziko za aina nyingi na hatuwezi kujisifu tuna Utawala Bora kwa maneno, bila ya kuonyesha kwa vitendo na kuondoa njia zote zinazoleta dhuluma za namna zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana Mbunge mmoja hapa, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, alizungumzia suala la watu kuwekwa ndani kwa miaka 10 kesi haziendelei, kwa sababu upelelezi unaendelea. Hili ni moja tu, lakini masuala haya yapo Tanzania nzima, huko Visiwani au Tanzania Zanzibar, kuna suala la namna hii, linalotukera na linaudhi na linavunja hadhi ya nchi hii. Suala la watu kuwekwa ndani kwa kesi za visingizio kabla upelelezi haujafanyika. Mtu anawekwa ndani kwa mwaka mmoja, miwili, hadi mitatu na baadaye inathibitika mtu huyo hana kosa na amedhulumiwa na familia yake imeshanyanyasika na hakuna hatua nyingine yoyote inayochukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelewa kwamba, zipo sheria ikiwa kesi haijathibitika Mahakamani, wewe unaweza ukamshtaki aliyekushtaki na ukadai fidia. Lakini hata ukifanya hivyo, hakuna chochote kinachofanyika. Mfano mdogo wala si mdogo ni mkubwa wa walioambiwa ni wahaini na wakashinda kesi, haukuweza kufanyika uhaini Zanzibar na mpaka leo hawajalipwa fidia yao hiyo. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, ni wengi wanaopata matatizo ya namna hii, kwa njia moja au nyingine. Linafanyika kosa au kinafanyika kitendo katika Mtaa fulani, wanakuja kuchukuliwa watu wote wanawekwa ndani, wanapoteza muda. Halafu wanaambiwa hawana makosa, wanatolewa bure bure. Suala hili Usalama wa Raia wanahusika na Serikali zote mbili zinahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taratibu za dunia, ikiwa kosa halijathibitika au huna ushahidi wa kutosha wa nani ukamkamate, inapaswa ufanywe upelelezi wa kutosha kabla na wakati unamkamata mtu, *at least* una ukakika wa asiliamia 80 kwamba, anahusika. Kwa maana hiyo, katika suala hili, ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu, ianzishe Sheria Maalum, ambayo itawasaidia waliokuwa hawafahamu na wale wanaofahamu, ikiwa wamedhulumiwa wakienda wakafungua kesi, sawa. Lakini kuna watu wengi sana hawafahamu, kwa maana hiyo, ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu, ianzishe Sheria ya kwamba, mtu yeyote atakayekamatwa kwa tuhuma za aina yoyote na ikiwa hakupatikana na hatia, basi wahusika waliomkamata, wamlipe fidia bila ya yeye

kushtaki Mahakamani.  Tutakapofanya hivyo, heshima kidogo itapatikana na tutaonyesha ile dhana ya Utawala Bora.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni la kwanza, ambalo nilikusudia kulisema na ninaomba  Mheshimiwa Waziri Mkuu, achukue  *note* kubwa sana juu ya suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, kuhusu Ofisi za Waheshimiwa Wabunge na vitendea kazi ni suala ambalo limeshazungumzwa mara nyingi na katika bajeti ya mwaka 2005/2006, Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala, iliagiza kwamba, suala hili litengewe fedha na zisimamiwe na Ofisi ya Bunge yenyewe, kwa bahati mbaya haijafanyika hivyo. Taarifa niliyonayo ni kwamba, fungu hili limetengewa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa. Sasa ikiwa hivyo ndivyo, je, sisi kule upande wa Zanzibar, limetengwa wapi na itakuwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba katika suala hili, kwa wale wa upande wa Zanzibar, likabidhiwe Ofisi ya Bunge ya Zanzibar na ni suala sugu, kwa sababu sijui kama kuna Mheshimiwa Mbunge hata mmoja, anayetoka upande wa Zanzibar, ambaye ana ofisi iliyokamilika, yenye hadhi ya Kibunge. Kwa hiyo, naomba suala hili, Mheshimiwa Waziri Mkuu, achukue *note* nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la Muungano, lakini mimi nataka kulizungumzia katika upande mwingine.  Migogoro ya Kimuungano, inawezekana watu wengi hawajui Katiba ya Jamhuri ya Muungano na ni kweli huko mitaani, msione sisi Waheshimiwa Wabunge tukifika hapa, tunapewa mara kwa mara Katiba za Jamhuri ya Muungano.  Lakini huko mitaani zinatafutwa Katiba katika *bookshops* nyingi sana, huwezi kuikuta Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.  Watu wengi sana wanapenda wawe nazo wazisome ili wazijue, lakini hazipatikani.  Sijui Serikali inaogopa nini watu wetu kuijua Katiba hii?  Ningependekeza Serikali ifanye juhudi ya kuchapisha hizi Katiba kwa wingi na raia wazipate kwa wingi.

Mheshimwia Naibu Spika, halafu hapo hapo katika suala hili la sheria, sijui katika mfumo wetu wa Elimu ikiwa ni wa kurithi au namna gani, lakini huwa ninajiuliza swali; hivi  ni kwa nini somo la sheria halianzishwi shuleni mapema na  halimo katika *syllabus* za shule za msingi?  Watu wengi wanaanzia vyeti, baada ya kuajiriwa wakawa na kazi muhimu kama Polisi hapo tena ndiyo anakwenda kuchukua *certificate* za sheria na wengine wanaofaulu kuendelea na masomo ya juu, ndiyo wanakwenda kuchukua somo la sheria Chuo Kikuu.  Kwa nini katika *syllabus* yetu hatuanzishi somo la sheria mapema mno ili wanafunzi wakiwa katika *stage* ndogo, wakajua hili somo la sheria. Naomba suala hilo nalo liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningezungumzia upungufu wa chakula. Sote tunakumbuka kutokana na ukame uliotokea hivi karibuni, Tanzania tulipata matatizo ya njaa katika baadhi ya Mikoa.  Kwa bahati mbaya tatizo likatokezea, lakini Serikali ikafanya juhudi kubwa na kuweza kutatua tatizo na tunamshukuru Mungu, hali imetengemaa kwa kiasi fulani.  Kwa bahati nzuri mimi natoka katika Jimbo la Mkanyageni, Pemba. Hivi sasa hakuna kiangazi kikali, lakini bado mvua zinanyesha.

Kumetokea matatizo ya mvua nyingi sana, mashamba yote yameharibika, kiasi cha watu 717 mazao yao yameharibika, milima imekatika na Pemba kama mnavyojua ni milima na mabonde. Mpunga umefukiwa na mchanga, mihogo imeharibika, migomba imeharibika bila ya kiangazi, lakini hivi sasa hali ya Pemba kuna njaa kwa kiasi fulani. Hali hii inategemewa kuwa mbaya zaidi hasa kwa siku zijazo, wakati mazao yote yameshaharibika na mwezi wa Ramadhani unakuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kutokana na hali ya uchumi wa Zanzibar, Ofisi ya Waziri Mkuu, iliangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la *TRA.* Tumesikia hata katika kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Waheshimiwa Wabunge wengi, wamelalamikia suala la *TRA*. Nataka kuongelea suala hili lakini pia katika mfumo mwingine. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na ningeomba ninukuu kwanza, kuna hiki kipengele katika ukurasa wa 23, naomba kunukuu: "Tunakusudia kuongeza mchango wa Serikali ya Muungano katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya Zanzibar, bila kuathiri haki na mamlaka kamili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa mambo ambayo siyo ya Muungano. Lakini naamini uchumi ambao ni mkubwa zaidi, una wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar, ambao ni mdogo."

Kwa maana hiyo, ikiwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ina wajibu wa kusaidia uchumi wa Zanzibar, ambao ni mdogo kwa maana kwamba, Jamhuri ya Muungano inafahamu vilivyo kwamba, uchumi wa Zanzibar ni mdogo na hapa Zanzibar, *at least* ilipokuwa na mapato, tunajua *customs* ni sehemu ya Muungano, lakini viwango vya ushuru haviko sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar viwango vya ushuru, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ilifanya viwe vidogo kwa makusudi ili kuvutia watu kununua bidhaa Zanzibar. Suala au kitendo cha Jamhuri ya Muungano, kuvifanya viwango vile viwe sawa, wamevunja biashara Zanzibar na kuifanya hali ngumu Zanzibar na hii siyo kusaidia uchumi wa Zanzibar. Jamhuri ya Muungano ni nchi kubwa, Tanzania Bara ina vyanzo vingi vya mapato, Zanzibar ni karafuu na utalii peke yake, utakapofanya viwango vya ushuru vya *customs* viwe sawa, unazuia mapato kwa Zanzibar na ndiyo maana Zanzibar hivi sasa imefilisika kibiashara. Watu wote wanakuja Tanzania Bara hapa kununua vitu. Kwa hiyo, kama nia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuisaidia Zanzibar kiuchumi, basi moja ni suala la kutofautisha viwango vya uingizaji wa bidhaa na utoaji bidhaa katika Bandari ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuongelea suala la mwisho. Nataka kuzungumzia habari ya hizi *internet*. Bunge lako Tukufu, tumeshuhudia kwamba ni la *speed* na *standard* na kwa upande wa Serikali ni kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. Sasa basi kwa maana hiyo, katika hali kama hiyo, ningeomba Ofisi ya Waziri Mkuu, iwasaidie Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu wanapaswa kuwa na habari mbalimbali za dunia. Ipatikane *wireless internet* ambayo itakuwa na upungufu wa gharama siyo kama ya hivi sasa inayotozwa, ambayo kodi kwa mwezi ya kulipia ni lazima uwe na hoteli kubwa au uwe na kiwanda, ndiyo uweze kumudu. Waheshimiwa

Wabunge hatutaweza kuimudu, Ofisi ya Waziri Mkuu ifanye juhudi Waheshimiwa Wabunge wawe *na access* ya *wireless internet* ili wapate kujisomea na kupata taaluma mbalimbali za habari katika *internet* hiyo. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nadhani Ofisi ya Spika, inajaribu kuandaa utaratibu wa mafunzo ya *computer* na bado tunaandaa.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie jioni hii ya leo. Awali ya yote, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge lako Tukufu, nikiwa Mbunge wa Jimbo. Namshukuru sana Mwenyezi Mungu, nilikuwa nalilia na sasa nimepata kweli, imekuwa kama kipofu ameona nyota, mwizi au jizi kakabidhiwa mke au mume. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wote walioniwezesha kufika hapa. Kwanza kabisa, lazima niwashukuru wana-CCM wote kwa kunipokea, maana nimemaliza Bunge na papo kwa papo nikaingia CCM, nikabidhiwa kadi yangu tarehe 1 Agosti, 2005 na ni nikaenda kwenye kura ya maoni tarehe 5 Agosti, 2005. Kwa siku nne, nikawa wa pili katika kura za maoni, nawashukuru wote. Pamoja na kwamba, jina likaingia kwenye Kamati Kuu, ninamshukuru kwa aina ya pekee, Mwenyekiti Mstaafu wa Taifa, pamoja *Central Committee* ya CCM, kulirudisha jina langu na kuniwezesha kupita hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru vilevile wapiga kura wa Jimbo la Bukene, vikundi vya kwaya na ngoma, kwa kunisaidia mpaka nikaweza kushinda kwa kishindo. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze kwanza, Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kushinda kwa kishindo, kupata Urais na vilevile nampongeza kwa kuwa Mwenyekiti wa Taifa wa CCM, kwa kura nyingi vilevile kwa kishindo. Nampongeza vilevile kwa kuchagua Mawaziri na Manaibu Waziri, wakiwa wengi Wanawake, maana nilikuwa nazungumza kwamba, ndani ya Bunge hili kuna akina Condolezza Rais humu, lakini ilikuwa maneno na sasa ni kwa vitendo. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais vilevile kwa kuchagua Sekretarieti yake ya utendaji ya CCM, akiwemo Mheshimiwa Yusuf Rajab Makamba, Mheshimiwa Aggrey Mwanri na wengine wote nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa *speech* yake ya Jumatatu na nampongeza kwa sababu ameweza kuwagusa Watanzania wote. Kwa kuwa wakulima wako asilimia 80 ya wananchi wote wa Tanzania, amewagusa katika kuongeza ruzuku ya pembejeo. Kwa hiyo, kila mtu anamtayarisha awe na maisha bora kama falsafa ya kwetu inavyozungumza kwamba,

mwisho wa siku kila mtu awe na maisha bora. Kwa hiyo, nampongeza kwa hilo. Nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, vilevile kwa sababu asilimia 20 ya Watanzania, wafanyakazi na wafanyabiashara na humo ndani kuna vijana na wanawake, kwa hiyo, nampongeza kwa kutoa mikopo ya shilingi milioni 500 katika kila Mkoa. Mikopo hiyo itawasaidia sana vijana na itawasaidia sana akinamama na hata wazee kubuni vitu vya biashara ili waweze kujikwamua kiuchumi na mwisho wa siku wawe na maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, naomba nizungumzie sasa Jimbo langu la Bukene, yale waliyonituma. Tatizo la kwanza, ambalo wanalililia wana-Bukene ni umeme. Naamini kabisa ahadi ya Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, alivyopita siku ile wakati anaomba kura zake za Urais na kutuombea sisi kura Wabunge na Madiwani, kama mafiga matatu, aliahidi katika hadhara alizokutana nazo pale kwamba, atatekeleza ahadi hiyo. Nimeona kwamba, ahadi hiyo itatekelezwa. Kwa hiyo, naishukuru Serikali kwamba, watatupa umeme *in advance*. Naamini kabisa tutapata umeme Bukene.

Mheshimiwa Naibu Spika na mimi nawaambia tukipata umeme sisi wa Bukene, maana yake tumetengeneza ajira kwa vijana. Kwa sababu Bukene *complex*, yaani *magodown* yaliyo pale yataleta ajira. Halafu *Railway Station* itafanya kazi na kwa hiyo, itafufua Bukene. Pale mizigo itakwenda kupitia Stesheni ya Bukene. Mchele, asali, ng’ombe, vyote hivyo vitapitia *Railway Station* kuja Dar e Salaam na vilevile watarudisha mizigo mingine kama *cement* kwa ajili ya kujenga nyumba bora ili tuweze kuweka umeme ule. Kwa hiyo, pale *Railway Station* patakuwa na kazi kwa vijana, tuta-*create jobs*. Kwa hiyo, watu watafanyakazi ya kupakia na kupakua mizigo na *magodown* yale yatajaa mchele. Kwa hiyo, pale patakuwa na *activity* za kila aina. Vilevile na akinamama ambao hawana kisomo chochote au vijana wata-*create jobs* za kupika chakula kwa wale wanaopita, wafanyabiashara wa hapa na pale. Kwa msingi huu, watu wa Bukene watakuwa na maisha bora. Kwa hiyo, nashukuru sana kwamba, mtatupa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ambalo watu wa Bukene wanaomba ni mawasiliano. Ni kitu cha kushangaza sana, mawasiliano kama simu na mimi nimekwenda *Tigo*, nimekwenda *Celtel*, nimekwenda *VODACOM*, nawaambia jamani njooni Bukene mtuletee simu na wenyewe wanafikiri sijui tunawadanganya. Pale mchele tunao tunaweza kuuza, tunapakia mchele tunawaarifu watu ambao wanauchukua mchele wetu kwamba, pokea mizigotumeshapakia leo. Vilevile tuna dhahabututafanya kazi vizuri. Pale ninazungumzia biashara, nashangaa makampuni haya hayaelewi kwamba, mimi nawaitia biashara, hivi mnakataa hela kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wanaonisikia, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, wanisaidie kuhakikisha kwamba, tunapata mawasiliano ya simu pale Bukene. Kwa sababu tunayahitaji na kweli yataleta faida kwa makampuni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine walichoniomba nifikishe hapa ni maji. Kusema kweli kwanza, kabla sijasemea maji, lazima niwashukuru Waziri wa Maji na

Naibu Waziri wa Maji, wameshaniambia kwamba, kuna miradi kama mitano itakuwepo katika Jimbo langu na vilevile nimekwenda pale Nzega nimekuta kwamba ni kweli. Kwa hiyo, naishukuru Serikali, kwa kutuletea maji tena mapema sana. Hii inaonyesha kwamba, tunakwenda kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya. Naamini tukipata maji, tutafanya kazi sana kwa sababu najua ndugu zangu wa Bukene ni wakulima kweli kweli. Kwa hiyo, wakileta maji, wakatufikishia pale, tutakuwa tumepunguza tatizo.

Lakini vilevile, walinituma nije nizungumzie mabwawa. Mabwawa mengine ni ya zamani tangu ukoloni, mabwawa kama yale ya Kagongwa, Ishigamba, Itombo, Mwangoye, Singiri, Malolo, Ikindwa na vilevile kuna sehemu nyingine ambazo tunaweza kutengeneza mabwawa kama vile kwenye njia unapotoka Suti kuja Bukene, pale watu wanashindwa kupita wakati wa mvua hata wajawazito wanashindwa kuwapitisha. Kwa hiyo, naomba wakati wa mvua, waje watuwekee mabwawa yale. Wakikarabati mabwawa haya tuna uhakika kwamba tutafanya kilimo cha umwagiliaji, na tutakuwa na uhakika kwamba ng’ombe wetu watapata majosho na vilevile watapata maji ya kunywa, yuna uhakika kwamba, tutapata maji kwa ajili ya binadamu. Naomba hayo tuyapate.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine waliloniomba ni kwamba, wanataka hospitali zipate *Ambulance.* Tuna matatizo ya *Ambulance*, tunayo moja tu katika Jimbo zima. Kwa hiyo, ningeomba tupate *Ambulance* moja kwa kila Kata na tuna Kata 16 na nyingine ziko mbali sana kama Semembela kule na Mambali. Kwa hiyo, naomba *Ambulance* kwa kila kata na *radio call*. Ikishindikana basi ziwe *Ambulance* moja na *radio call* moja kwa Kata mbili. Kwa mfano, ile ya Semembela ishirikiane na Mambali, ile ya Isengeye ishirikiane na Mambali, ile Isengeye ishirikiane na Katitu, ile ya Bongwa ikishirikiane Bukene, ya Kamaharaga ishirikiane na Ikindwa na hivyo hivyo Singiri ikishirikiane na Mongwa au Igusule. Naomba tupate hizo ili tuweze kuhudumia akinamama na kuzuia vifo vya akinamama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakafanyakazi waliokuwa *East African Community* wamepata shida sana. Wanadai na wengine wameshakufa, wako watoto wao wanaodai mirathi hiyo, lakini mpaka sasa hivi hawajapata. Majina yapo kwenye gazeti wamekwenda Hazina ndogo ya Shinyanga, wengine wameenda Hazina ndogo ya Tabora, lakini hawajalipwa malipo yao. Naomba hao wafanyakazi walipwe ili waweze nao kujikwamua kiuchumi na waweze kuendelea na maisha kwa hicho kidogo. Maana yake *East African Community* ilishavunjika zamani na tumeanza nyingine. Kwa hiyo basi na wao kwa ari mpya hiyo hiyo, kasi mpya na nguvu mpya, walipwe posho zao na pensheni zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ningeomba mbegu. Tunawashukuru *World Vision*, wanatupa mbegu kwa bei rahisi. Lakini naomba Serikali ituletee vilevile mbegu kama zile za mihogo ili tuweze kulima na sisi tuna asili ya kulima chakula na kukiweka ndani. Hata mboga za majani tuko hodari sana sisi Wanyamwezi kukausha na kuweka. Hata mihogo tuko mahodari sana kuikausha na kuiweka. Kwa hiyo, naomba mbegu zote kama zile za mihogo ili tuweze kuzilima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunaomba visima virefu, *World Vision* wametuchimbia, lakini naomba na Serikali itusaidie kuchimbia visima virefu hasa katika Makao Makuu ya Jimbo Bukene ili waweze nao kupata maji. Kwa kweli ni kitu cha kusikitisha, unapofika pale maji hakuna na yanauzwa kwa bei ya juu sana. Kuna vianzo maji pale Mwatoba, lakini vinakauka, kuna chanzo cha maji pale Tanganyika. Kwa hiyo, naomba tupate visima virefu ili tuweze kupata maji ya jumla. Tukipata Maji ya kunywa na tukipata maji ya matumizi ya nyumbani, mabwawa yale yakifufuliwa, kwa kweli mambo yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu bado nina nafasi, naweza kuzungumzia barabara. Barabara ni tatizo kwa sababu wako wakulima wengi sana kwa mfano, katika Kata Semembela, Kata Kamaharaga na Kata ya Ikindwa, mazao yao wanatakiwa kuyapeleka Tinde au Shinganya, sasa hawawezi kupita hapo katikati kwa sababu barabara ni mbaya. Kwa hiyo, naizungumzia barabara hii kwa sababu inaunga Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Shinyanga. Kwa hiyo, naomba basi katika utaratibu wa barabara basi tupate barabara ile inayoitwa *Old Mwanza Road* kutoka Tabora inakuja mpaka Mambali. Nataka iende hiyo ya kikoloni inakwenda Semembela ambako ndiko kwenye mazao mengi na inapitia Kamaharaga ambako kuna mazao mengi, inakuja mpaka Ikindwa kuja kupanda Mwamala na kuteremka Mwangoye kutoka Nata kuja Tinde na kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile barabara nyingine inayotoka Dar es Salaam, magari yote yanayotoka Dar es Salaam yanapita katika barabara hiyo ya *shortcut* kwenda Isaka, lakini ina hali mbaya kwa sababu kuna mahali haipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, nadhani msemaji wetu wa mwisho ndiye huyo. Lakini wakati tunafanya usalama kupitisha mikoba yetu katika vituo vya usalama, kuna Mheshimiwa Mbunge amesahau funguo za gari. Sasa kama kuna mtu anajua hivyo, atazichukua kwa Makatibu wetu pale nje.

Baada ya kusema hilo, naomba niwashukuru sana, kwa kazi tuliyofanya leo, mjadala umekwenda vizuri. Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.38 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 29 Juni, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*